*"Kwenye kila tungo ya kitabu hiki, utasafiri na vijana na kugundua, kusherehekea na kuuelewa ulimwengu kupitia macho yao."*

- Elias Mutani, Mwandishi

*"Hadithi zimejaa mafunzo kwa vijana.... Nimeona pia utofauti wa kiuandishi wa vijana na waandishi watu wazima."*

- Zamda Geuza, Mhadhiri na Mwanafunzi wa Shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Exeter

*"Nimefurahi sana kuufanyia kazi mkusanyiko huu wa tungo. Unavutia, unaelimisha na unatafakarisha...."*

- Dorkas Kissava, Mwanafunzi wa Fasihi, Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam

soma
burudani • utamaduni • maarifa

# MAPENZI KIDIGITALI

## NA HADITHI NYINGINE



Taasisi ya Usomaji kwa Maarifa na Maendeleo

# MAPENZI KIDIGITALI

## NA HADITHI NYINGINE

Taasisi ya Usomaji na Maendeleo--Soma
0673014071
info@soma.or.tz
www.somabookcafe.com

Soma, 2024

*Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili wa*
**The Commonwealth Foundation**

**ISBN: 978-9976-5637-1-9**

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya chapisho hili inayoweza kuzalishwa tena, kusambazwa, au kupitishwa kwa namna yoyote. Aidha hairuhusiwi kunakili, kurudufu au kulitumia kwa njia zingine za elektroniki bila idhini ya maandishi ya Mchapishaji. Hatua za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote atakayekiuka ilani hii.

# Yaliyomo

Utangulizi ........ iv
Shukurani ........ vii
Kuhusu wahariri wanagenzi ........ viii
Mapenzi Kidigitali ........ 1
Mtafutaji Hachoki ........ 8
Chozi Bakuli ........ 12
Kiunzi cha Mwisho ........ 15
Amina Yuko Wapi? ........ 18
Safari ya Mabadiliko ........ 22
Nuru katika Giza ........ 26
Lazima Nifanikiwe ........ 30
Mtaa wa Hekaheka ........ 36
Sintasahau ........ 42
Najuta ........ 43
Harakati ........ 47
Shamba la Dhahabu ........ 50
Kichaka ........ 53
Tabu Tabuni ........ 54
Tone la Damu ........ 60
Uyoga ........ 68
Yote ni Mapito ........ 74
Zawadi ya Mama ........ 76

# Utangulizi

Kitabu hiki ni zao la shughuli za kulea 'kizazi kipya' cha waandishi wa kazi za kubuni; dhima ambayo **Soma** imejitwalia kupitia Mkahawa wa Vitabu **Soma**. Mkahawa huu, wa kwanza wa aina yake, ulikusudia kuwa nafasi ya kuvinjari vitabu na fasihi, na kuchota maarifa, utamaduni na burudani ndani ya furushi moja.

Ni mkusanyiko wa hadithi fupi zilizochaguliwa kutoka kwenye mikusanyiko hadithi kumi bora za mizunguko sita ya Andika na **Soma**, shindano la hadithi fupi kwa wanafunzi wa shule za sekondari (mwaka 2013—2018) na mashairi mawili kutoka kwenye kitabu cha sauti (*audio book*) chenye mkusanyiko wa kazi za kubuni zilizoandikwa na wanafunzi wa kike wa shule za sekondari walioshiriki kwenye mradi wa Thubutu wa kupinga ukatili kwa wasichana (2016).

Lengo mahususi la kuzichapisha tungo hizi ni kuchangia katika upatikanaji wa vitabu vya fasihi vinavyowavutia vijana, vilivyoandikwa na vijana wenzao. Tunaamini njia hii pia itawahamasisha vijana wengi zaidi kusoma na kuandika kazi za kubuni. Ili kutimiza azma hii, tumejitahidi katika uchaguzi, uhariri na usanifu wa kitabu hiki ili kiwe na ubora na hadhi stahiki ya kusomwa na hadhira kubwa; na kwa njia hiyo, kutambulisha vipaji vya utunzi vya waandishi chipukizi wa tungo hizi.

Waandishi wa hadithi kumi bora wa shindano la Andika na Soma walishiriki mafunzo ya uandishi wa kazi za kubuni ambayo yaliwawezesha kuboresha kazi zao; na kuziwasilisha kwenye hadhira siku ya utoaji tunzo. Thubutu ilitumia uandishi wa kazi za kubuni kama nyenzo ya kuibua tafakuri na kuhoji njia zinatumika kuwazoeza wasichana kuona ni jambo la kawaida kutomaswatomaswa na kurushiwa maneno yanayodhalilisha utu na ujinsia wao hata kama mambo hayo yanawakirihisha. Walitumia njia hizohizo kuwasilisha uzoefu na hisia zao kwenye hadhira yenye wanafunzi wenzao wasichana kwa wavulana, walimu na wazazi. Kazi zao zilibainisha jinsi ambavyo kwa kutokukemea vitendo hivyo, jamii inalea na kuchochea ukatili wa kijinsia kwa kuwazoeza wasichana kuyavumilia tangu wanapokuwa vigori.

Mkusanyiko wa hadithi na mashairi yaliyomo kwenye kitabu hii yamebeba maudhui anuai yanayogusa maisha na uzoefu wa vijana katika karne ya 21. Baadhi ya masuala yanayoibuliwa ni kama ifuatazo: athari za kutumia mitandao ya kijamii bila kuchukua tahadhari—Mapenzi Kidigitali ya Jacqueline

Deus Ludege na Najuta ya Suzana Mremi; changamoto za kiuchumi (umasikini, ajira na ujasiriamali)—Mtafutaji Hachoki ya Mary Kisingi, Lazima Nifanikiwe ya Cecilia Mgimbila, Mtaa wa Hekaheka ya Robert Mwijonge, Tone la Damu ya Emmanuel Minja, Yote ni Mapito ya Eliana Swai; uroho wa madaraka, wananchi kuwajibisha viongozi—Chozi Bakuli ya Asha Malolo, Kiunzi cha Mwisho ya Swedi Shauri, Nuru katika Giza ya Aneth Mirambo; harakati za haki, usawa na kupinga udhalimu—Amina yuko Wapi? ya Ngadula Joseph Magaka, Safari ya Mabadiliko ya Irene Sarakikya, Harakati, ya Kulwa Abdallah; ukatili wa jinsia, dhuluma na ukandamizaji—Sintasahau (Thubutu), Najuta ya Suzana Mremi, Kichaka (Thubutu), Tabu Tabuni ya Otilia Angelus Haule, Shamba la Dhahabu ya Aidan Mtura. Masuala mtambuka yanayoingiliana na hayo yaliyojumuishwa hapo juu ni pamoja na changamoto za mihadarati na uhalifu—Tone la Damu; na uadilifu— Zawadi ya Mama ya Maria Makasi. Uyoga ya Zahara Tunda inasawiri utandawazi unavyowavutia vijana bila kuhoji kilichoko nyuma ya pazia. Pamoja na dhamira zilizotajwa, ziko hadithi zinazosawiri alinacha za kimapenzi miongoni mwa vijana balehe, na hali ya umasikini unaofungamana na akina mama wanaolea peke yao wakiwa na fursa chache za kiuchumi. Kwa ujumla maudhui ya tungo hizi ni kioo cha jamii kwa macho, uzoefu na fikra za vijana wa kati ya miaka 14 hadi 18.

Mchakato wa kuandaa mswada wa kitabu hiki ulihusisha wahitimu wa mafunzo ya Andika na **Soma** ambao walipitishwa kwenye mafunzo ya uhariri kwa vitendo kwa mrengo wa jinsia na umajumui wa Afrika.

Elias Mutani, mmoja wa wakufunzi wa Andika na **Soma** ambaye pia ni mwandishi, mhariri, na mwalimu wa uandishi bunifu ndiye aliyekuwa mwezeshaji kiongozi wa wahariri wanagenzi. Kwa maneno yake, "*Kuandaa na kutoa kitabu hiki ni fursa adhimu kwetu ya kusherehekea na kutangaza utajiri wa fikra na hisia za vijana wa Tanzania… katika kuwafunda kiuandishi, tumeamsha ari yao ya kuzivijari fikra za kimageuzi za usawa wa wanawake na umajumui wa Afrika wakati wa kudurusu hadithi zao….*"

Zahara Tunda aliratibu ukusanyaji, mawasiliano na waandishi (kazi hii ilikamilishwa na Viola Masawe na Dorothy Mchatta), na jopo la wahariri, mkufunzi, uandaaji wa warsha za uhariri mafunzo na michakato mingine ya kiuendeshaji. Zahara ni kati ya mhitimu wa nafunzo ya Andika na Soma mwaka 2016, na hadithi yake imo ndani ya kitabu hiki. Hivi sasa ni mwandishi wa habari mkufunzi na mtaalam kwenye mawasiliano kwa umma. Kwa maneno yake, "*Ni furaha kushiriki katika maandalizi ya kuwapata wahariri waandishi waliopata mafunzo na kuchangia katika kuboresha hadithi hizi hadi kupatikana kwa kitabu…. Hadithi hizi zikawe chachu kwa vijana wa rika zote na wote watakaozisoma katika kujenga mstakabali mpya wa jamii bora yenye maendeleo sio tu kiuchumi bali kisiasa, kiutamaduni na kifikra.*"

Katika kuchambua na kuandaa orodha ya kwanza ya hadithi zilizopendekezwa kufanyiwa uhariri, Zahara alisaidiana na Dorcas Kissava, mwanafunzi wa shahada ya kwaza ya fasihi kwa Kiingereza, Chuo Kikuu cha Dar es salaam ambaye alikuwepo Soma akifanya mafunzo ya vitendo. Kwa maneno yake, "*Mchakato huu ulinipanua mawazo na kunipa ladha mpya ya fasihi. Ulinisaidia kutafsiri somo la fasihi ninalolisoma chuoni katika uhalisia….*"

Baaada ya kuupokea mswada kutoka kwa mkufunzi na mratibu, niliupitia tena kubaini na kuziba mapengo ya kimuundo na unyoofu wa lugha. Katika hatua hii ya uhariri, tulilazimika kuziacha baadhi ya hadithi na nyinginezo tukazifanyia uhariri wa kina. Hatua ya uhariri wa kuhakikisha unyoofu wa lugha, sauti na mtiririko ilifanywa na Zamda Geuza, ambaye yuko kwenye hatua ya mwisho ya kuandika tasnifu yake ya uzamivu katika fasihi, Chuo Kikuu cha Exeter. Kwa maneno yake, "*Nimefurahi kuhariri muswada huu, hadithi zimejaa mafunzo kwa vijana.... Nimeona pia utofauti wa kiuandishi kati ya vijana na waandishi watu wazima. Naweza kusema (tungo hizi) ni sauti yao.*"

Usanifu hati na jalada ulifanywa na Reystuta Ben Mtobwa.

Demere Kitunga, Machi, 2024

# Shukurani

Itakuwa vigumu kuwataja watu na mashirika yote yaliyochangia kwenye shughuli za Andika na Soma na Thubutu ziliyowezesha upatikanaji wa tungo zilizo kwenye kitabu hiki.  Tafadhali pokeeni shukurani zetu za dhati nyote kwa ujumla wenu, mliotajwa na ambao hamkutajwa kwa majina.

Kwanza kabisa, tunapenda kuwashukuru wanafunzi wote walioshiriki kwenye shindano la Andika na Soma na mradi wa Thubutu; pamoja na uongozi wa shule zao na walimu waliowahimiza na kuwapa moyo. Tunawashukuru pia wazazi wa wanafunzi kumi bora kuridhia watoto wao washiriki mafunzo ya uandishi; pamoja na wanafunzi hao kwa kuzingatia mafunzo na kuboresha tungo zao ambazo baadhi zimeteuliwa kuwa ndani ya kitabu hiki; na wanafunzi wenzao, walimu na wageni wengine waliohudhuria kwenye hafla ya kutoa tunzo na kuhitimisha mafunzo.

Kwa namna ya pekee tunawashukuru majaji na wakufunzi wote, wakiwakilishwa na Prof. M.M. Mulokozi, Joram Nkya, Elizabeth Mahenge, Elias Mutani, Janeth Namara, Neema Komba, Abia Suleyman, na Layla Ally; pamoja na Mugisha Bassasingohe kwa kusanifu nembo na matangazo yote ya shindano pamoja na vijitabu vya hadithi za kila mzunguko.

Tunawashukuru watendaji na taasisi za ufadhili ziliotoa ruzuku iliyofanikisha utekelezaji wa miradi hii miwili, na hatimaye uandaaji na uchapishaji wa kitabu hiki. Asanteni kwa ukarimu wenu Christoph Londemann na CKU (baadaye Ubalozi wa Denmark); Muadi Mukenge na Global Fund for Women; na Ubalozi wa Ireland kwa kufadhili Andika na Soma. Asanteni Mary Rusimbi na Women Fund Tanzania kwa kufadhili Thubutu. Asanteni Emma D'Costa na Commonwealth Foundation kwa kufadhili uandaaji na uchapishaji wa kitabu hiki kidigitali; pamoja na mafunzo ya uhariri kwa wahitimu wateule wa Andika na Soma kupitia mfuko wa majaribio wa Creative Grants.

Binafsi nawashukuru watendaji wote walioshiriki katika kuwezesha upatikanaji wa kitabu hiki. Waratibu wa Andika na Soma, Rehema Chachage, Safarani Seushi, Jasper Sabuni na Lauwo George; mratibu wa Thubutu, Doris Puja; mratibu wa ukusanyaji, uteuzi na uhariri wa tungo za kitabu hiki ambaye pia ni mhitimu wa Andika na Soma, Zahara Tunda, mratibu wa uenezi na uzinduzi wa kitabu hiki, Viola Massawe na wafanyakazi wote wa Soma walioshiriki kwa nyakato tofauti za uhai wa miradi hii, Paulina George, Invioleta Mwakiwone, Latifa Abdalla na Dorothy Junior Mchatta, na wengine ambao sijawataja. Asanteni sana kwa juhudi zenu.

Mwisho bali si kwa umuhimu, pokeeni shukurani za dhati, nyote mlioshiriki katika kuandaa muswada wa kitabu hiki; wasomaji waliopitia tungo hizi na kutoa maoni ya kuboresha, wahariri ambao majina yao yameorodheswa kwenye kurasa nyingine za kitabu hiki; pamoja na Reystuta Ben Mtobwa, msanifu hati na jalada la kitabu.

# Kuhusu wahariri wanagenzi

## *Zawadi Kondo*

Naitwa Zawadi Selemani Kondo, nina miaka 25, mzaliwa wa Bagamoyo. Nina shahada ya Sanaa na Ualimu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Ni mwandishi wa mashairi na hadithi fupi na mwanaharakati wa haki za wanawake, watoto na vijana. Matamanio yangu ni kujifunza na kupata mafanikio ili niwe mfano wa kuigwa na vijana wenzangu wa kike. Kutekeleza azma hii nafanya uwezeshaji kwenye vituo vya watoto yatima na najitolea kuendesha mafunzo ya jinsia kwa njia za sanaa. Ni mshiriki wa Andika na Soma mwaka 2016/2017

## *Beatrice Mmasa*

Jina langu ni Beatrice Mmasa. Umri wangu ni miaka 29. Mimi ni mwalimu mwenye shahada ya Ualimu ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Ninapendelea kusoma hadithi na kutembelea sehemu mbalimbali. Ni mshiriki wa Andika na Soma mwaka 2014/2015.

## *Swedi Shaury*

Naitwa Swedi Shaury. Nina miaka 27. Nimehitimu elimu ya Chuo Kikuu mwaka 2019 na sasa nafanya biashara ndondogo. Nilianza kazi ya uandishi nikiwa shule ya sekondari mwaka 2013 ambapo nilijikita zaidi kwenye mitandao ya kijamii ili kujenga ukaribu na mashabiki wangu. Ni mshiriki wa Andika na Soma mwaka 2015/2016.

## *Maria Makasi*

Naitwa Maria Makasi, Mtanzania mwenye miaka 30, ninayejivunia kuliita jiji changamfu la Dar es Salaam nyumbani. Ninajua Kiswahili na Kiingereza kwa ufasaha na safari yangu katika ulimwengu wa uhasibu na usimamizi wa fedha imewezekana kutokana na ufanisi huu. Ni mshiriki wa Andika na Soma mwaka 2015/2016.

## *Jackline Kisanga*

Naitwa Jackline R. Kisanga, nimezaliwa mwaka 1998 mkoani Kilimanjaro. Nilipata na kuitambua shauku ya kuandika nilipokuwa Shule ya Sekondari ya Wasichana Machame (2015—2017) ambapo nilipata nafasi ya kueleza fikra na maoni yangu kwenye ubao wa matangazo. Baadaye nilishiriki kwenye shindano la Andika na Soma 2016/2017. Mwaka 2019 nilishiriki kwenye warsha ya uandishi ya *Afro Young Adult* iliyoandaliwa na Taasisi ya Goethe. Nina shahada ya Biashara na Masoko ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mafanikio yangu katika elimu na fasihi ni ushahidi wa juhudi zangu endelevu za kujifunza na ubunifu.

# Mapenzi Kidigitali

Jacqueline Deus Ludege

Miale ya jua ilitoa mng'ao wa dhahabu alasiri ile tulivu. Praygod Mosha, fahari na furaha ya familia yake, alikuwa ndio kwanza amerejea nyumbani baada ya kumaliza kidato cha sita. Alipokaribia lango ya nyumba yao, alisikia vifijo vya furaha vya Bibi na Bwana Mosha, wazazi wake waliokuwa wakisubiri kwa hamu kurejea kwa mwana wao mpendwa. Praygod alipofika mlangoni, alilakiwa na nyuso za furaha na sauti za shangwe zilizovuma kama kinanda cha kwaya siku ya sikukuu. Praygod alikuwa ameitazamia sana siku hii ya kilele cha masomo yake, na alitarajia kufaulu mitihani na kusonga mbele katika hatua inayofuata ya masomo ya chuo kikuu.

Shangwe iliyoambatana na kula na kunywa ilidumu kwa masaa kadhaa, kisha maisha yakarejea katika mkondo wake wa kila siku. Praygod alibaki kuwa yuleyule asiyeonekana kufuatana na marafiki zake katika safari za kusisimua au ushirika wa kutafuta starehe. Rafiki yake wa daima asiyeweza kutenganishwa naye alikuwa ni simu yake ya mkononi. Walikuwa chanda na pete. Rafiki zake walipofurahia mitaa ya ulimwengu mzuri uliowazunguka, yeye alizama katika mitaa ya kidigitali. Wazazi wake, wakihofia uraibu, walimsihi apunguze matumizi ya simu, lakini kwake simu yake ilikuwa ndio ufunguo wa ulimwengu. Hapakuwa na kitu chenye umuhimu zaidi kwake ambacho simu yake isingeweza kumpatia.

"Praygod, mwanangu, huendi kwenye sherehe pamoja nasi?" mama yake aliuliza siku moja jioni, matumaini yakimulika machoni mwake. Siku hiyo, familia yao ilikuwa imealikwa harusini.

"Hapana, Mama," Praygod alijibu, macho akiwa yameganda kwenye kioo cha simu.

"Unaweza kuja baadaye iwapo utabadili mawazo."

Praygod, bila kusema neno, aliinua tu kichwa, kisha alirudisha macho kwenye simu. Mama yake alipotoka nje alijaribu kwa mara nyingine.

"Kumbuka kufunga mlango kama utakuja kuungana nasi."

"Sitakuja huko mama." Praygod alisema kwa mkato kisha akachukua simu na kuzuru mtandao wake pendwa wa Facebook. Alitumia sekunde kadhaa kuikodolea macho picha aliyoipenda sana, akausoma tena wasifu wa mwenye sura

hiyo uliomvutia kila alipoiangalia picha ile. Ulikuwa umepita mwezi mmoja tangu alipomtumia msichana huyo ombi la urafiki na kukubaliwa baada ya dakika mbili tu. Huyu hakuwa aina ya wale wanaochukua siku mbili hadi wiki kujibu. Siku ile ya kukubaliwa ilikuwa ya faraja kubwa moyoni mwake, akaendelea kutuma na kupokea ujumbe kila siku. Sasa alikuwa amechoshwa na ujumbe mfupi; haukumtosha na hakusadiki kuwa uzuri auonao ulikuwa wa msichana yule. Alipomwomba namba yake ya simu, alipewa mara moja kama alivyokubaliwa ombi la urafiki.

"Fatma!" aliita kwa sauti ya kuvutia sana, akasita kidogo, halafu akaendelea kwa msisitizo. "Nafikiri ni wakati sasa kwa kijana aliyesoma hekaya nyingi za uzuri wa msichana nyuma ya kioo cha simu kukutana na mwenye uzuri wake."

"Unamaanisha unataka kukutana na mimi?" Fatma alijibu kwa mshangao.

"Unajua picha ya jalada ni mwanzo tu wa hadithi," alisema Praygod. "Nahitaji kuisoma hadithi yenyewe."

"Basi usijali, utaniona ... ."

Praygod aliruka juu kwa furaha lakini ghafla simu ilikata. Simu ya Fatma ilikuwa na mipango mingine kabisa., Alipopiga tena alijkutana na, "… haipatikani, jaribu tena baadaye." Aliivurumisha simu yake ukutani, akakunja ngumi. Uso wake ulifanana na shamba lililokwatuliwa huku macho yake yalizungukazunguka kama mtalii aliyepotea mbugani. Dunia ya kidigitali ilikuwa na kisasi binafsi dhidi yake, aliwaza; na ulimwengu wa kidigitali ulikuwa umekula njama dhidi ya jitihada zake za kukutana na msichana yule mwenye mvuto.

Akiwa na azma ya kuvunja uhusiano wake na ulimwengu wa kidigitali, Praygod alitoka nje bila kuwaza mara mbili. Kiza kilikua kimeanza kuingia. Alitembea harakaharaka kuelekea mitaa yenye majumba yaliyomulikwa kwa mng'ao wa taa za ukutani na barabarani. Alivuka barabara bila kujali, akipuuza honi kali za madereva wenye hasira waliokerwa na uzembe wake. Mara alimpamia mwanaume mnene aliyekuwa akisubiri gari kituoni, akayaoga matusi ya mtu mzima. Aliyapuuzia, akaendelea mbele, hatua kwa hatua. Hatimaye aliingia katika mitaa yenye nyumba zilizojificha kwenye vivuli vya usiku.

Aliendelea kutembea hadi alipojikuta amesimama mbele ya mlango mdogo wa mbao wa chumba kilichojitenga na nyumba kubwa, akabisha mlangoni kwa fujo.

"Vipi?" sauti iliita kutoka nyuma ya mlango. Alikuwa Justine, aliyehitimu shule pamoja na Praygod. Hawakuwa wakiendana sana, lakini walipokuwa shuleni, daima Justine alikuwa akimwomba Praygod mahitaji ambayo hakuweza kuyamudu. Vilevile, daima Justine alikuwa amezungukwa na marafiki, hasa wasichana; ingawa Praygod alisuasua alipomshawishi kuongea nao.

“Kwa nini hukupiga simu kabla ya kuja?”

“Sina simu.”

“Wewe ni mtu wa kutokuwa na simu?” Justine aliwasha tochi ya simu yake ndogo, akamulika uso wa Praygod, ghafla uso wake pia ukabadilika. “Kulikoni?” aliuliza. Kabla hajajibiwa alisema, “Nitakupeleka mahali upate utulivu.”

Justine alipiga simu. Kufumba na kufumbua iliwasili bajaji, wakaingia na safari ya kurejea mitaa yenye majengo makubwa na taa za barabarani ikaanza. Walisimama katika mkahawa mmoja. Wakati Justine anachagua meza ya kukaa, Praygod alimnong’oneza kwa aibu.

“Sikuja na pesa.”

“Usijali nitalipa, kwa mchezo wa leo, kamari imelipa.”

Praygod alionekana kuchanganyikiwa. “Mchezo?”

“Kila mtu anajua Simba walikuwa wanacheza na Yanga leo!”

Praygod, akijisikia kutengwa kabisa na ulimwengu huu, akajisemea kwa sauti ndogo, “Kila mtu isipokuwa mimi tu.”

Justine akainamisha kichwa chake na kumkumbatia kiubavu, “Nilitabiri matokeo nikapatia.”

Walipokuwa wakisubiri huduma, ghafla harufu nzuri ya uturi ilipenya kwenye pua ya Praygod, akaelekeza macho yake kule ilikotoka. Ndipo alipomuona binti mmoja alikuwa amevaa sketi fupi ya kubana na blauzi ya bluu iliyomkaa vyema maungoni mwake. Sura yake ilirembwa kwa wanja na rangi nyekundu ya mdomo iliyokoza kwa mbali. Praygod alihamanika kidogo. Yule dada alimgeukia na kuachia tabasamu pana lililofanya meno yake meupe kuonekana vizuri.

“S-s-sama-hani nahisi ka-ma naku-fahamu.” Praygod aliuliza kwa kigugumizi.

“Bila samahani kaka.” msichana alijibu, akamkazia macho kidogo na kuipindisha shingo yake kwa madaha.

“Kweli dada au nakufananisha?” kigugumizi kiliyeyuka ghafla kama kilivyokuja.

“Hujanifananisha.” mrembo yule alimjibu huku akiachia kicheko chepesi cha chini chini na kuweka kijitabu cha menu mezani, “Ni mimi Fatma, nikuhudumie chakula au kinywaji gani ?.”

“*Waooo*! Kumbe kweli ni wewe? Umependeza sana.” Praygod alisahau

alikuwa mkahawani pamoja na Justine. Msichana aliyeongea naye saa chache zilizopita sasa alikuwa mbele yake. Aliagiza kuku mzima, sahani ya chipsi na boksi la juisi ya matunda mchanganyiko bila kujali kama rafiki yake alikuwa na uwezo wa kulipia au la. Praygod alimkodolea macho Fatma alipotembea hadi alipopotelea maeneo ya jikoni.

"Vipi mbona hivyo?" Justine aliuliza.

Praygod alimuelezea yote na kusema tokea azaliwe hakuwahi kuona mrembo kama yule dada. Aliishukuru dunia ya kidigitali kumkutanisha na mrembo wa ndoto zake aliyefanya kazi karibu na nyumbani kwao.

Walikula na kunywa huku wakipiga soga.

"Utaenda wapi ukitoka hapa ili nikusindikize?" Praygod alipata ujasiri wa kumuuliza Fatma, wakati Justine alipokuwa analipa bili.

"Siku nyingine Kaka, leo furahi na rafiki yako."

Muda ulishakwenda, magari yalikuwa machache barabarani, na majumba mengi yalikuwa yameshazimwa taa za ndani. Praygod alitembea polepole kuelekea nyumbani baada ya bajaji waliyochukua kuwafikisha nyumbani kwa Justine. Sura ya Fatma ikipita akilini mwake kama video. Mara kwenye kituo cha basi kilichokuwa karibu na nyumbani kwao alishtuka kumuona Fatma mbele yake.

"Wewe tena? Unafanya nini hapa usiku wote huu?"

"Huoni kuwa nasubiri basi?"

"Nikachukue gari nikusindikize?"

"Hata! We nenda zako. Kaka zangu watanipitia tuongozane."

"Sawa, umependeza."

"Asante. Na wewe nenda nyumbani na usitembee usiku sana."

Praygod aliondoka, baada ya hatua chache aligeuka na kumpungia mkono Fatma. Alitamani arudi pale na kumkumbatia. Aliendelea kutembea huku akigeuka nyuma hadi alipopotelea gizani. Sasa aliwaza jinsi gani angemwambia Fatma kuwa alitamani wawe wapenzi. Praygod alirudi chumbani kwake, baada ya kutafuta kwa muda, alipata simu yake. Mipasuko kwenye kioo ilitengeneza mtandao wa nyuzi kama utando ya buibui. Kwa mshangao, ilikuwa inafanya kazi. Alimpigia Justine kumjulisha kuwa amefika nyumbani salama, na alipomaliza, ujumbe ukaingia.

"Nafurahi umefika nyumbani salama."

"Umejuaje?"

“Simu yako haikuwa hewani kabla.”

“Kumbe wewe ni msichana makini sana.”

“Na wewe ni mvulana jasiri usiyeogopa kutembea gizani.”

“Unajua, ninapotembea gizani, sauti yako ndiyo nuru inayoniongoza.”

“Nafurahi kusikia hivyo kama ni kweli, lakini sasa ni muda wa kulala. Usiku mwema!”

“Unaonekana kuniwazia mema daima, kujali kwako kunanipa joto moyoni.”

“Haha! Acha uongo wako. Jaribu kupata usingizi, Praygod.”

“Sawa, naomba tukutane ndotoni kwa mazungumzo matamu.”

“Haha, acha ukorofi! Lala salama!”

Praygod aliendelea kutuma jumbe ila akagundua kuwa simu ya Fatma inaonyesha vema moja hafifu kuashiria kuwa haiko hewani. “Ina maana ameshazima simu mara hii na kulala?” Praygod alijisemea mwenyewe tena, alipojaribu kupiga akaambulia muito wa “haipatikani”. “Mmh! Ila sio mbaya, kesho sio mbali.”

Asubuhi yake, Praygod alichelewa sana kuamka. Aliamkaa saa tatu rafiki yake, Justine alipokuja. Jana yake alikuwa amemuomba amsindikize madukani kwenda kununua simu mpya. Baada ya kujiandaa na kupata kifungua kinywa pamoja, walianza safari huku wakipiga stori nyingi za hapa na pale.

“Yule demu wa jana ni bomba,” Justine aliongea huku akimtazama Praygod kwa jicho la udadisi.

“Yule, ameshakuwa wangu,” Praygod alijisifu.

“Ah wapi! Uwe na demu mkali kama vile si utaringa mshikaji wangu?” Justine alimtania rafiki yake aliyekuwa akiendesha gari. Kila walipowapita wasichana waligeuka na kuwatazama.

“Unajua hujaniambia tunaenda duka gani?” Praygod alihoji baada ya kufika kwenye makutano ya barabara.

“Tunaenda kule niliponunua *kitochi* changu, kuna simu zimeingia jana ndiyo nataka nikakuoneshe.”

“Usijekuwa unanipeleka kwenye *vitochi!*” Praygod alizungumza wakati analirudisha gari nyuma kama wanavyofanya nyota wa filamu za upelelezi.

Punde aliegesha nje ya duka aliloelekezwa. Kumbe lilikuwa ni duka alilolijua kama kiganja cha mkono wake. Hakuhangaika na simu za bei nafuu alizoelekezwa na Junstine. Alinunua simu mpya ya bei mbaya yenye kioo kinachong'aa kama jicho la nyati katika mwanga wa jua. Bila kuchelewa alipakua programu zake zote za mitandao ya kijamii anayoipenda. Hakika himaya yake ya kidigitali ilianza upya.

"Nimefufuka kidigitali!"

"Nilitaka uachane na ulimwengu wa mitandao ya kijamii," Justine aliongea huku anacheka. "Toka tuhitimu, jana ndio tumeonana kwa mara ya kwanza!"

"Ningekutana wapi na msichana mrembo kama Fatma nisingekuwa kwenye mitandao ya kijamii?"

"Una hakika yule ni wako?"

"Kama bado huamini, angalia hii." Praygod alisema huku akipiga simu kwa video. Kwenye kioo ilionekana sura mwanana ya Fatma, ikafuata sauti yake nyororo.

"Vipi Praygod, nakusubiri twende."

Justine alibaki ameduwaa. Hakuwa na cha kusema zaidi ya kumwangalia tu rafiki yake. "Mnaenda wapi?" aliuliza hatimaye.

"Chukua hii uweke laini yako." Praygod alimrushia Justine ile simu iliyokuwa na mipasuko. "Washa data, utajua wapi tulipo." aliondoa gari huku akitabasamu.

Nyuma ya jengo lenye maduka makubwa kulikuwa na jengo lililokuwa na hoteli, Fatma alikuwa amependekeza wakapumzike pale. Praygod alifika na kuchukua chumba, akaingia haraka, sura yake ikidhihirisha wazi faraja ya kuanza uhusiano mpya na Fatma. Hakuwahi kamwe kuchukua chumba cha hoteli hapo awali. Alikuwa mgeni wa mapenzi aliyechukuliwa ghafla na dhoruba ya mahaba ya mwendo kasi, akiishangaa bahati yake ambayo hakuitarajia. Moyo wake ulidunda ngoma ya ushindi wa mapenzi ya msichana yule mrembo kuliko wote duniani tena kwa siku moja tu. Ilikuwa hatua moja ndani ya ulimwengu asioujua. Alisubiri, akamsubiri Fatma kwa hamu.

Alipompigia simu ya video Fatma, alishangaa kumwona akiwa na Justine, wakiwa wamekaa pamoja katika mkahawa ule ule walipokutana jana yake, mikono yao ikiwa na alama za "V".

"Fatma, hii ni dhihaka gani tena?" Praygod alilalamika, uso wake ukiwa umejaa fadhaa.

"Oh, tulikuwa tunakufundisha tu umuhimu wa kutokuwa na uraibu wa

mitandao ya kijamii," Justine alisema kwa sauti ya utani.

Fatma aliongeza, "Pia tulitaka utoke nyumbani na kuishi maisha ya kweli wanayoishi vijana wenzio, sio yale ya kufikirika yanayoonekana kwenye simu yako."

"Justine, yaani umeamua kuniadhibu kwa mtindo wangu wa maisha usiofanana na wako? Fatma, nilidhani nimepata kitu cha maana, kumbe ni mchezo tu kwako?" Praygod alizidi kukasirika.

"Acha hasira, rafiki yangu Praygod," Fatma alisema kwa upole, "Ilikuwa ni kwa nia njema tu."

Justine aliongeza, "Hebu chukulia hii kama changamoto. Umesoma darasa moja na Fatma na bado umeshindwa kumkumbuka ulipomwona mtandaoni."

"Tulisoma darasa moja?"

"Msichana gani mwingine unamkumbuka kama si wale unaokutana nao tu kwenye mitandao?" Fatma alihoji kwa sauti thabiti.

Praygod alichukua muda kufikiria, hasira yake ikianza kupungua. "Fatma," aliita hatimaye. "Tunaweza kuonana tena?"

"Ndiyo, kama utaweza kuishi nje ya mitandao ya kijamii kwa wiki moja tu."

"Wiki moja?"

"Wiki moja."

"Inawezekana kabisa Praygod," Justine alisisitiza. "Ni uamuzi tu."

"Sawa Justine, lakini na wewe uwe tayari kwa changamoto utakazopata kutoka kwangu pia."

Wote walitikisa vichwa wakiashiria kukubaliana.

"Tukutane tena wiki ijayo," Fatma alisema, akicheka. "Kisha tutaona nani atakuwa amejifunza zaidi kutoka kwenye mchezo wetu huu."

# Mtafutaji Hachoki

Mary Kisingi

*Sehemu ya Kwanza: Arusha, Tanzania*

Kaskazini mashariki mwa Tanzania, jiji la Arusha limechipuza katikati ya milima na mabonde. Jijini hapo, katika lindi la ufukara ndipo alipozaliwa Amina. Maisha yake yote ameshuhudia maji ya mvua yakivuja kwenye paa la nyumba yao na kupenya darini. Ugali kwao ulikuwa unalika hata kwa kutowelea maji yaliyotiwa chumvi, ndimu na pilipili tu. Msichana huyu hakupata fursa ya kwenda shule ya gharama kama ilivyo kwa watoto wengi wa umri wake. Daima mama yake alilalamikia maisha kuwa magumu kiasi kwamba asingeweza kumsomesha kwenye shule bora; japo alimpenda kama mboni za macho yake, na Amina alilijua hilo.

Tangu utotoni mwake, Amina alikuwa akijichanganya na watoto wengine. Alipenda kujifunza kila kitu. Licha ya kutokupata elimu bora alijaliwa upeo uliomshangaza kila mtu. Amina alikuwa kama ua lililochanua katika ardhi kavu; na alijaa matumaini na ndoto kubwa.

"Mama, kwa nini tulizaliwa katika dunia yenye vikwazo vingi namna hii?" Amina alimuuliza mama yake siku moja alipokuwa binti mdogo wa miaka sita hivi.

Mama yake, alijibu, "Amina mwanangu, barabara yako ni kama mvua inayonyesha baada ya kiangazi kirefu. Hizi changamoto zitakuimarisha na kukuongezea thamani ya utu."

Amina alivutiwa na maneno yale lakini hakuelewa kitu. Jinsi alivyozidi kukua, ndivyo alivyozidi kuyatafakari, lakini licha ya hekima na busara alizojaaliwa kuwa nazo, hayakumpa majibu ya maswali yake. Alipofikisha umri wa miaka kumi na sita, Amina alianza kutafuta kazi ili kuisaidia familia yake lakini kila alipopiga hodi, alikuta milango ya fursa imefungwa.

Siku moja, aliamua kutafuta ushauri kwa jirani mwenye duka kubwa la vifaa vya ujenzi. Ilisemekana kuwa hapo zamani Bwana Juma, mmiliki wa duka hilo alikuwa fukara kupindukia. Amina alimuendea na kumuuliza, "Bwana Juma, uliwezaje kujenga himaya hii kutoka kwenye mwanzo mgumu?"

Bwana Juma alitabasamu kisha akasema, "Amina, mafanikio ni kama mti.

Lazima uupande, uumwagilie, na kuukinga dhidi ya upepo na dhoruba. Nilianza na biashara ndogo, nikajituma na kufanya kazi kwa bidii."

Maneno ya Bwana Juma yalimtia moyo Amina kwamba kama akianzia mahali hata kama ni padogo na kufanya bidii, atafanikiwa. Siku moja alipokuwa katika mahangaiko ya kusaka ajira alimwona mwanamke mmoja mrembo aliyekuwa kaegesha gari la kifahari. Aliamfuata na bila kusita akamuamkia. "Shkamoo mama. Samahani, nimevutiwa sana na gari lako. Unaweza kuniongoza na mimi nipate mafanikio kama yako?" Amina aliuliza kwa heshima.

Mwanamke huyo alimtazama kwa mshangao na hamaki kidogo, kisha akasema, "Binti, sikiliza. Wewe bado ni msichana mdogo, una mengi ya kujifunza. Mafanikio hayapatikani kirahisi kama unavyofikiria. Isitoshe, mara nyingi mafanikio hayapimiki kwa vitu vinavyoonekana."

Maneno ya mwanamke huyo yalimchanganya Amina. "Kwa hiyo mafanikio ni nini basi?" alijiuliza bila kupata majibu. Lakini hakukata tamaa. Alijua kwamba kuna mengi ya kujifunza na kufanya, hadi ategue kitendawili kile.

Amina aliendelea kutangatanga na njia akitafuta ajira. Jioni baada ya kusaidia kazi za nyumbani alijisomea vitabu ili ajipanue mawazo. Siku moja alipokuwa akipita kwenye bustani ya jiji alikutana na mzee aliyekuwa akipanga maua kwa ustadi mkubwa na kuyaangalia kwa fahari.

"Mzee, unawezaje kuifanya na kuifurahia kazi hii bila kuichoka?" Amina aliuliza. Mzee huyo aligeuka na kumtazama Amina kwa machoyaliyojaa tafakuri akasema, "Kila ua lina hadithi yake. Nafurahia kuona maua yakichanua na kukua. Ni kama maisha, kila siku ina changamoto zake, lakini mwisho wa siku, kuna uzuri unaojificha ndani ya changamoto hizi."

***

*Sehemu ya Pili: Nairobi, Kenya*

Amina alitafuta kazi kwa miaka mitatu bila mafanikio. Sana sana aliambulia vibarua vya hapa na pale mradi mkono uende kinywani. Hatimaye, alifanya maamuzi magumu ya kuondoka Arusha, akavuka mpaka hadi Nairobi. Safari yake ilikuwa ngumu kwa sababu hakuwa na hati ya kusafiria. Alikamatwa mpakani mara mbili na kurejeshwa Arusha, hali iliyomlazimu kutafuta hadi kuipata pasi halali ya kusafiria.

Nairobi, alijikuta katika bahari ya watu asiowajua, naye kama chombo kwenye bahari hiyo, akisukwasukwa na mawimbi ya changamoto mpya za maisha. "Nairobi ni kama msitu usio na mwisho, unaweza kupotea au kupata njia," Amina alijisemea, wakati anatafakari pilikapilika za jiji lile ambalo lilikuwa tofauti kabisa

na Arusha. Jiji lililopambwa na majengo marefu yaliyotenganishwa na barabara pana zenye magari yanayokwenda kasi na sauti mchanganyiko za umati wa watu wenye shughuli nyingi.

Amina hakwenda Nairobi bila malengo. Katika mahangaiko yake alipokuwa Arusha, alipata kibarua kwenye bustani ya maua. Alijifunza kutunza bustani na kupanga maua aliyopeleka maofisini. Hakuishia hapo, bali alitengeneza kadi ya mawasiliano na kuigawa kwa kila aliyemwona ana uwezo wa kulipia huduma yake. Kwenye ofisi mojawapo alikutana na mwanadiplomasia mmoja aliyeipenda kazi yake. Alipohamishiwa jijini Nairobi, mwanadiplomasia yule alimuahidi Amina kazi ya kutunza bustani ya nyumbani kwake kama atakuwa tayari kuhamia Nairobi.

Katika jitihada zake za kuielewa jamii yake mpya, Amina alijitosa kujifunza Kiswahili cha mtaani kilichojulikana kama *sheng*, ambacho kilikuwa na msamiati na lafudhi tofauti na ile ya Arusha. Alivutiwa pia na tamaduni mbalimbali za Kenya, lakini aligundua kwamba haikuwa kazi rahisi kwa sababu wenyeji walimwona kuwa ni mgeni asiyestahili kufundishwa "siri" zao.

Licha ya kupata ujira mnono kuliko aliokuwa anapata Arusha, bado maisha yalikuwa magumu zaidi ya alivyotarajia. Amina alipambana na umaskini mkali, akiishi kwenye chumba kidogo kwenye makazi duni na nyumba yenye vyumba vingi vilivyojaa watu pomoni. Chakula na maji safi vilikuwa adimu, na kila siku ilikuwa ni ya mapambano ya kusaka riziki. Katika wakati huu mgumu, alikumbuka milima na mabonde ya kwao, mama yake na marafiki aliowaacha nyuma. Kuna nyakati alitamani kurudi Arusha lakini alipokumbuka sababu zilizomfanya aondoke nyumbani alighairi.

***

*Sehemu ya Tatu: Johannesburg, Afrika Kusini*

Miaka michache baadae, Amina alifanikiwa kuweka akiba ya kutosha kujinunulia tiketi ya ndege kuelekea Johannesburg, Afrika Kusini. Alikuwa amesikia kuwa huko kuna fursa zaidi za ajira na kujiajiri. Alipowasili, maisha yalimkabili kama anga yenye mawingu mazito na dhoruba kali. Changamoto za huko zilikuwa zaidi ya zile za Arusha pamoja na Nairobi. Alikumbana na ubaguzi na umasikini uliopindukia. Alishangaa waAfrika wa huko wakiwabagua waAfrika wengine na kuwaita '*Makwerekwere*'. Alishuhudia mapambano dhidi ya wageni weusi yaliyosababisha vifo na uharibifu wa mali na makazi. Wakati huo alikuwa hajapata kazi nzuri licha ya kuuza vinyago vichache alivyoingia navyo kutoka Nairobi.

Akiba yake ilikuwa inakauka na umaskini ulimvyemelea kwa kasi. "Mbona

maisha ni magumu hivi?" Amina alijiuliza, akitazama anga la Johannesburg lililokuwa limejaa majengo marefu kama misitu ya chuma na saruji. Kila alipokaribia kukata tamaa, alikumbuka maneno ya mama yake, "Vikwazo ni kama mawe ya kujengea, sio vya kukukwamisha," na moyo wake ulijaa nguvu mpya, akaendelea kupambana.

Hatimaye Amina alipata kazi kama mkalimani katika taasisi moja inayowasaidia vijana waliosafirishwa kwenda Afrika ya Kusini na genge la usafirishaji haramu wa wanadamu. Alijifunza kuwa vijana kutoka nchi mbalimbali walikuwa wakiahidiwa kuwa watapata kazi nzuri ili wakubali kusafiri. Badala yake, wasichana walijikuta wakifanywa kuwa watumwa wa ngono wakitumikishwa kwenye kazi ya ukahaba bila ridhaa yao wala ujira.

Wavulana waliingizwa mwenye mnyororo wa usambazaji wa mihadarati ambapo wengi wao walijikuta mikononi mwa polisi au magenge yenye silaha. Alifurahi kupata fursa ya kutumia kipaji chake cha lugha kuwanusuru vijana wenzake ambao harakati zao za kusaka maisha bora ziliwaingiza pabaya. Matumaini mapya yalizaliwa moyoni mwake na hali yake kiuchumi iliimarika. Alimpigia simu mama yake kumueleza kuhusu mafanikio yake. Hakika aliiona ndoto ya kuwa mkombozi wa familia yake ikitimia na jambo hili lilimpa faraja.

# Chozi Bakuli

Asha Malolo

Kama ndege wanaokusanyika kwenye chemchemi iliyobubujika jangwani, ndivyo wananchi wa jimbo la Sakira walivyojikusanya kwenye uwanja wa wazi siku hiyo. Kila mmoja akitaka kushuhudia ujio wa Mbunge Mwita, uliokuwa umesubiriwa kwa muda mrefu.

Jua la utosi liliangaza mithili ya mshumaa mkubwa unaowaka kwenye sherehe, wakati umati wa watu wa kila rika ulipoanza kumiminika uwanjani. Wanawake kwa wanaume, vijana kwa wazee, na hata watoto pia walifika kwa makundi kama wafanyavyo ndege kwenye msimu wa kuhama.

Vijana walikuwa wakiongea na kucheka, wakiwa na nguvu na matumaini kama machipukizi ya mimea michanga kwenye shamba lenye rutuba. Wazee nao, kama miti mikubwa iliyokomaa, walikaa pamoja wakibainisha busara na uzoefu walipokuwa wanabadilishana mawazo. Watoto hawakutulia. Walikuwa wakiruka-ruka kama ndama katika malisho ya nyasi mpya, wakicheza na kukimbizana kutoka pembe moja ya uwanja hadi nyingine.

Mwita alipowasili, sauti za honi zenye mahadhi ya ngoma za sherehe zilisikika, zikiashiria kuanza kwa tukio la kihistoria. Aliteremka kutoka kwenye gari lake lililong'aa kama lulu ndani ya maji; na kuanza kutembea kuelekea kwenye kundi la watu kwa kujiamini, kama nahodha aliyefanikiwa kuliokoa jahazi lisiende mrama.

"Nataka leo niongee nanyi wanajimbo wangu wapendwa," alisema Mwita, kwa sauti imara yenye msisitizo. Maneno yake yalikuwa kama maji yanayotiririka, yakilenga kugusa na kukata kiu ya wanajimbo wa kila rika.

Wanajimbo walimsikiliza kwa makini, wakiwa wamemkazia macho kama kurunzi zinazomulika njia. Kila neno alilosema lilipokelewa kwa shauku na tafakuri, wakitarajia kwamba safari hii, kama mvua inayonyesha katika ardhi kavu, Mbunge wao angeleta matumaini mapya ya maendeleo katika jimbo la Sakira.

"Wananchi wangu wapendwa, leo nimekuja na habari njema. Nimemleta mkandarasi mahiri kwa ajili ya kujenga barabara yenye kiwango cha hali ya juu katika jimbo letu. Lengo langu ni kuhakikisha hampati tena taabu za usafiri. Nina imani kubwa kwamba mtaupokea mradi huu kwa mikono miwili. Nawahakikishia, barabara hii itakamilika ndani ya mwezi mmoja tu."

“Umuhimu wa barabara hii siyo tu kuwa itarahisisha usafiri, bali pia itachangia ukuaji wa biashara zenu. Mtaona jinsi itakavyorahisisha usafirishaji wa mazao kutoka mashambani hadi sokoni. Pia itawezesha mawasiliano na ushirikiano baina yenu na wananchi wa jimbo jirani; na hatimaye kuimarisha mshikamano na kuongeza fursa za kibiashara kati ya majimbo haya.”

“Niliarifiwa na kujionea mwenyewe namna ambavyo barabara hii haipitiki kabisa wakati wa mvua. Hali hii inasababisha usumbufu mkubwa katika usafirishaji wa bidhaa na watu, na hata kupelekea kutokea kwa ajali. Nimechukua uamuzi huu baada ya kufanya tathmini na kupata maoni kutoka kwenu. Huu sasa ni wakati wa kubadilisha hali hii na kuleta mabadiliko ya kweli katika jimbo letu la Sakira.”

Ghafla, kutoka katikati ya umati, msichana mmoja alinyanyuka na kwa ujasiri wa simba jike akasema, “Mheshimiwa Mwita, miaka mitano ya uwakilishi wako na sasa ndio unawaza kujenga barabara? Je, hili ndilo suluhisho pekee la matatizo yetu? Na kwa nini linakuja wakati huu tunapokaribia uchaguzi mwingine?”

Mwita, alishitushwa na swali hilo, akauliza. “Binti unaitwa nani?”

“Salima.”

“Naomba kujua una umri gani Salima.”

“Nina miaka kumi na tisa.”

Mwita alijibu kwa dharau kidogo, “Ndio, Salima. Barabara ni mwanzo wa maendeleo. Unafikiri nini kingine kinachohitajika zaidi?”

Salima, alijibu, “Mheshimiwa, barabara ni muhimu, lakini tumeishi miaka mitano bila huduma za afya za uhakika, elimu bora kwa vijana, ajira kwa wakazi na miundombinu mibovu ikiwemo barabara. Barabara pekee haiwezi kutatua haya.”

Mwita, akijaribu kujitetea, alisema, “Lakini barabara itasaidia katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo...”

“Maendeleo gani hayo ambayo hayagusi maisha ya kila siku ya mwananchi wa kawaida? Je, barabara pekee itamsaidiaje mama anayehangaika kujifungua bila huduma za afya? Au vijana tunaomaliza shule bila matumaini ya ajira?” Salima alihoji kwa jazba kidogo.

Mwita, alitafakari kwa kina, akajibu, “Ninaelewa wasiwasi wako, Salima. Lakini huu ni mwanzo tu. Tutafanya zaidi.”

Salima, akiwa hajaridhika na majibu yale, alisema, “Mwanzo huu umechelewa mno, nakumbuka ahadi ulizowahi kutoa ambazo hazijawahi kutimia.”

Mara kikundi cha wazee, sura zao zikiwa zimechorwa na mikunjo ya umri na uzoefu wa maisha, kilimsogelea Salima. Kiongozi wao, Mzee Kabwe, alikuwa wa kwanza kuzungumza. Alizungumza kwa sauti iliyojaa mamlaka, "Wanajimbo wenzangu, hii siyo namna ya kumheshimu kiongozi wetu. Binti, ingawa una haki ya kuuliza maswali, umevuka mipaka ya adabu. Lazima tujifunze kujiheshimu, hasa katika mikusanyiko ya umma."

Maneno yake yalipenya kwenye umati, na baadhi ya wanajimbo wakatikisa vichwa vyao kwa kukubaliana naye, nyuso zao zikioneshai heshima na unyenyekevu waliokuwa nao kwa wazee na viongozi.

Lakini, si kila mmoja alikubaliana na maoni hayo. Kutokea kwenye kundi la vijana, Sauti imara ya Juma ilisikika, "Mzee Kabwe, tunaheshimu busara na hekima zenu wazee wetu, lakini huu ni wakati wa mabadiliko. Salima anasema ukweli unaouma. Hatuwezi kukaa kimya wakati maendeleo yetu yanadorora. Heshima haipaswi kuwa kisingizio cha kutokubali ukweli au kuzuia mabadiliko yanayohitajika. Ni wakati wa viongozi wetu kusikiliza sauti za vijana pia."

Maneno ya Juma yaliwasha moto, ukazuka mjadala mkali kati ya vijana na wazee; kila upande ukitoa maoni yake kwa hisia kali. Wazee walisisitiza umuhimu wa heshima na utaratibu, wakati vijana walidai kasi ya maendeleo na sauti zao kusikilizwa na kuheshimiwa.

Salima, kwa kuhofia uwepo wake utasababisha majibizano na Mheshimiwa ugeuke kuwa zogo, aliamua kuondoka. Vijana, waliokuwa wamevutiwa na ujasiri wake, walimfuata nyuma kama kundi la ndege lililopata kiongozi. Kila hatua waliyopiga ilikuwa kama dhihirisho la kupinga uongozi wa Mwita. Wanawake wengi na baadhi ya wanaume waliohudhuria mkutanoni wakaanza kuondoka, kila mtu akichukua njia yake, ama kujirudia nyumbani au kuungana na Salima na vijana wenzake. Meneja wa kampeni, alijaribu kuwashawishi vijana wale na wanakijiji wengine wabaki, lakini walimpuuza.

"Tunamtaka Salima awe Mbunge wetu!" ilisikika sauti moja kutoka kwenye kundi lile la vijana, ikadakiwa na umati ule uliokuwa unamfuata Salima na kupaa kuwa sauti ya kupasua anga.

Mzee mmoja kati ya wananchi waliobaki mkutanoni, akizungumza kwa sauti ya unyenyekevu, aliuliza, "Kama vijana na wanawake hawatakupigia kura, unatarajia nini Mheshimiwa Mwita?"

Sasa meneja wa kampeni aliona hali imezidi kuwa mbaya, akawa hajui aelekee upande upi. Mwita, alikuwa amesalia na watu wachache akiwa na majonzi, na machozi yalianza kumtoka, yakatiririka kama mto wa kujaza bakuli. Aliuona mwisho wake katika macho ya vijana wale pamoja na wanawake na wazee waliochoka na ahadi hewa alizokuwa akizitoa wakati akiomba kura.

## Kiunzi cha Mwisho

Swedi Shauri

Nderemo na shangwe zilitawala kila pembe ya Tingisha, kufuatia ushindi wa Bw. Kwasa, aliyechaguliwa kwa kura za wananchi kuwa Rais wa nchi hiyo. Bw. Kwasa alikuwa amenadi sera za kuvutia kwa sauti inayotoa hakikisho, vitu vilivyomfanya apendwe na wananchi wa kila kundi. Wakulima, wafanyakazi, na hata vijana walimchagua kwa kura nyingi, wakitarajia mabadiliko.

Umati wa watu walijitosa barabarani kushangilia ushindi huo kwa nderemo, wakipiga ngoma, kucheza na kuimba kwa furaha. Lakini, si kila mtu alikuwa na furaha. Kulikuwa na wale waliotilia shaka ushindi huo wa Bw. Kwasa.

"Ameshindaje huyu? Kura zitakuwa zimechakachuliwa tu!" malalamiko ya chini-chini yalisikika kutoka kwa kikundi cha watu.

"Mambo yanazidi kuwa magumu. Tazama bei za bidhaa zinavyopanda. Huyu ataleta nini kipya?" mwingine aliongeza.

"Lakini Bw. Kwasa anaweza kuwa suluhisho la matatizo yetu," mtu mwingine alijitokeza kumtetea, akisema hali ilivyokuwa ilihitajika kubadili uongozi kupisha mawazo mapya.

Malumbano haya yaliendelea, yakionesha mgawanyiko wa maoni kati ya waliokuwa wanamkubali Bw. Kwasa, waliotaka Rais aliyekuwa madarakani aendelee, na waliodhani kura zilistahili kumuangukia kiongozi mwingine wa chama cha upinzani tofauti na Bw. Kwasa. Wakati haya yakiendelea, Bw. Kwasa na familia yake walikuwa wakisherehekea ushindi kwenye hoteli ya kifahari jijini. Walikula na kunywa kwa furaha, wakiwa wamezungukwa na watu waliosuka kampeni zake na mikakati ya ushindi.

Siku chache baadaye, sherehe kubwa ya kuapishwa kwa Bw. Kwasa ilifanyika. Hotuba yake fupi ilifuatiwa na makabidhiano ya madaraka na Rais mstaafu. Wananchi walikuwa na matumaini, lakini pia walikuwa wakitazama kwa makini kila hatua ya serikali yake mpya.

Baraza la mawaziri lilipotangazwa, mashaka ya wale waliokuwa hawana imani naye yaliongezeka. Nafasi ya Waziri wa Fedha iliachwa wazi. Bw. Kwasa akiamua kushikilia wadhifa huo yeye mwenyewe. Haikuishia hapo, mtoto wa kiume wa Bw. Kwasa aliteuliwa kuwa waziri wa mambo ya ndani. Wakati yote haya

yanatokea, Bw. Kwasa na familia yake walibadili mfumo wa maisha, wakisafiri na kujiburudisha nje ya nchi licha ya changamoto zilizokuwa zinawakabili wananchi.

Wakulima walilalamikia kukosekana kwa pembejeo na kudorora kwa bei ya mazao. "hatuna hata fedha za kukodi trekta," baadhi walisemezana kwa huzuni.

Hali ilikuwa ngumu vilevile katika sekta za ajira. Rushwa ilikuwa imekithiri; hakuna aliyeweza kupata kazi bila kutoa hongo.

"Vyeti vyangu viko hapa, nina sifa zote," alisema kijana mmoja kwa mwajiri.

"Hatuna matatizo na vyeti vyako, unachohitaji ni kutoa 'kitu kidogo tu'," mwajiri alijibu.

Mambo yalikuwa mazito zaidi kwa vijana wa kike. Binti mmoja, jina lake Anisa, naye alikuwa akitafuta kazi. Yeye alikutwa na kadhia nzito zaidi.

"Unahitaji kazi, eeh? Jaribu 'kufanya mambo yawe rahisi' basi," mwajiri mtarajiwa alizungumza bila soni. "Una nafasi twende tukapumzike ufukweni jioni hii?"

Anisa alishikwa na hasira. Alikuwa ameshasikia kuhusu rushwa ya ngono lakini alikuwa hajakumbana na tukio la kidhalilishaji namna ile. Alimpokonya mwanaume yule vyeti vyake, akaondoka bila kusema neno. Alichoamua ni kupeleka kisa chake kwenye vyombo vya habari.

Mahojiano yake kwenye televisheni moja ya binafsi yalianza kwa utulivu akisimulia masaibu yake, lakini ghafla yalikatishwa alipoanza tu kutaja jina la mhusika ambaye alikuwa ni afisa wa ngazi ya juu serikalini. Skrini ilipoteza picha, na badala yake, ujumbe ukatokea, ukinadi 'matatizo ya kiufundi'. Lakini madhara yalikuwa yameshafanyika. Maneno yake yalikuwa tayari yamegusa nyoyo za watazamaji.

Kesho yake asubuhi, Anisa alikamatwa akituhumiwa kwa uhaini. Alionekana mbele ya kamera, mikono yake ikiwa imefungwa pingu lakini uso wake ulikuwa umejaa azma na uasi. Serikali ilikusudia kumfanya kuwa mfano, ili kuzima ghadhabu iliyokuwa ikichemka dhidi ya utendaji wa Serikali ya Rais Kwasa.

Taarifa ya kukamatwa kwa Anisa ilizua taharuki. Ilikuwa kana kwamba ujasiri wake uliwapa sauti wasio na sauti na nguvu wasio na nguvu. Maandamano yalizuka nchini kote Tingisha. Yalianza kama mikusanyiko midogo ya kupashana habari lakini haraka sana mikusanyiko hiyo ikageuka kuwa mikutano mikubwa ya hadhara na hatimaye kukawa na maandamano makubwa. Watu wa Tingisha, kutoka vijijini na mijini walishiriki maandamano hayo wakidai haki itendeke.

Wakati mambo haya yanatokea, huko gerezani Anisa alijaribu kutoroka. Jaribio lake la kwanza likipelekea kukamatwa. Picha za kukamatwa kwake zilirushwa mubashara kwenye runinga. Mapambano yake dhidi ya waliomkamata, huku akipiga kelele za uhuru, yalisambaa kwa kasi. Mapambano yake hayakuwa tena ya kwake peke yake; bali yaliunganika na madai ya waandamaji yakawa ya taifa zima.

Maandamano yaliendelea na kutoa shinikizo lililomzidia Rais Kwasa. Ushikaji wake thabiti wa hatamu ya kuongoza taifa ukaanza kulegea. Kashfa za ufisadi, zilizofichwa na kupuuzwa kwa muda mrefu zilianza kuibuka, zikichochea moto wa hasira ya umma iliyokuwa tayari inawaka.

Hatimaye, yasiyofikirika yakatokea. Akiwa amekabiliwa na vita asivyoweza kushinda dhidi ya wananchi wake, Rais Kwasa alijiuzulu na kukimbia nchi. Ilikuwa ni dakika ya ushindi, iliyochukua jitihada na dhabihu kubwa. Barabarani nchini pote Tingisha vilisikika vigelegele na vifijo vya furaha, lakini furaha hiyo ilichanganyika na ufahamu wa mapambano na kafara zilizolifikisha taifa lilipofika.

Anisa, ambaye sasa aliachiliwa huru na kutambulika kama ishara ya mapinduzi, alisimama katikati ya umati uliokuwa unashangilia. Safari yake iliyoanza kwa kupigania haki yake binafsi ilikuwa imeanzisha harakati iliyomwondoa fisadi madarakani na kuhamasisha taifa kusimama kwa ajili ya haki.

# Amina Yuko Wapi?

Ngadula Joseph Magaka

Mzee Mabimbi alikuwa ameketi kwa utulivu nje ya kibanda chake kidogo kilichoezekwa kwa mabati yaliyojaa kutu, mithili ya ngao iliyopoteza hadhi yake. Jua jekundu kama embe dodo lililowiva na kusambaza mwanga hafifu wa dhahabu, lilianza kujificha taratibu nyuma ya vilele vya milima na kuangukia kwenye vilindi. Mkononi, Mzee Mabimbi alishikilia redio ndogo ya rangi nyekundu iliyokuwa inatangaza mechi ya soka ya watani wa jadi, Simba na Yanga. Kama kawaida lilikua pambano lenye upinzani mkali kama mwangaza na giza. Mzee Mabimbi, akiwa amevutiwa na mchezo, aliita kwa sauti iliyoshindana na ile ya mtangaza mechi.

"Mama Amina! Eeh, Mama Amina!"

Hakuna aliyemjibu. Punde si punde alitoka mwanamke aliyejaa kwenye gauni na kupanda juu hewani, akitembea kwa madaha mithili ya twiga. Alimkuta Mzee Mabimbi akiwa amejawa na furaha iliyopindukia, akicheka kwa sauti kubwa na kugonga magoti yake pamoja kama ngoma.

"Simba wamefunga! Wamesawazisha, hahaha!" Alizungumza kwa bashasha, akiwa amesahau kabisa ulimwengu uliomzunguka.

Mama Amina, akiwa amesimama pembeni mwake, mikono kiunoni, alijibu kwa sauti iliyojaa ucheshi uliochanganyika na kejeli, "Haya bwana, Simba wamefunga, lakini je, hiyo itatuletea chakula mezani? Au itamlipia Amina ada ya shule?"

Mzee Mabimbi, bado akiwa kwenye wingu la furaha ya goli la Simba, alimtazama Mama Amina na kucheka kidogo, "Ahh, mke wangu, tuachane kidogo na matatizo, tuupe moyo furaha!"

Lakini Mama Amina hakutikiswa na furaha ya mume wake, uso wake ulitawaliwa na wasiwasi. "Furaha ya mpira haina maana ikiwa Amina hatujamsikia. Ni kama tunapiga ngoma bila ya kujua kama kuna mtu anayeisikia," alisema, sauti yake ikiwa imejaa shaka na hofu, akionesha wasiwasi wake juu ya kimya cha binti yao.

"Usiseme hivyo mke wangu!" Mzee Mabimbi alijibu kwa masihara, akipunguza kidogo sauti ya redio yake bila kuondoa umakini kwenye mechi

iliyokuwa inayoendelea. Alikuwa na tabasamu pana usoni, huku mkewe akiwa amejaa wasiwasi.

"Nisiseme hivyo nini, Mabimbi? Au unafurahia hali yetu ya sasa? Tazama madebe yanavyotuvujia. Hata mijusi inatutembelea. Huu ndio mwelekeo tuliotaka baada ya kumpeleka Amina shule?" Mama Amina aliongeza sauti, ikapaa kuliko ile ya redio. "Tumeuza karibu kila kitu, mashamba yetu yote; na bado hakuna habari kutoka kwa Amina. Si ajabu ameolewa na Mzungu na ametusahau kabisa!"

Mzee Mabimbi, akiendelea kusikiliza mechi yake kwa sikio moja, alimjibu kwa mzaha, "Basi labda ametingwa akijifunza maisha ya kizungu ya kula kwa uma na kisu, au Mungu kamjaalia simu ya dhahabu ambayo mtandao wake haufiki mashambani."

Mama Amina alikasirika na kusema, "Huu si wakati wa utani, Mabimbi! Hatujamsikia binti yetu kwa miezi mitatu. Miezi mitatu, Mabimbi! Na wewe unafikiria tu kuhusu Simba na Yanga."

Mzee Mabimbi, akitambua kuwa mkewe amechukizwa na mzaha wake, alipunguza tena sauti ya redio.

Amina, alikuwa kang'ara kama nyota inayopasua giza, kwa kufanya vizuri mno katika mitihani yake ya kidato cha sita. Ufaulu wake ulimfanya kila mtu astaajabie kipaji chake. Marafiki zake walimshauri kwamba angeweza kufanya vizuri zaidi maishani endapo angejiunga na moja ya vyuo bora duniani. Ushauri huo uliwagusa wazazi wake, ambao walikuwa na ardhi kubwa, wakaamua kuuza sehemu ili kumuwezesha Amina kwenda ng'ambo kupata hiyo elimu bora.

Safari yake ya elimu ilimpeleka hadi Chuo Kikuu cha Oxford nchini Uingereza, ambapo alionyesha uwezo na bidii ya hali ya juu. Alipomaliza masomo yake ya shahada ya kwanza kwa alama za juu, alipewa nafasi ya kipekee ya kuendelea na masomo ya uzamili kwa gharama za chuo.

Miaka mitatu baada ya kuondoka nyumbani, wazazi wake waliojivunia mafanikio yake walikuwa na shauku na hamu kubwa ya kumuona tena. Amina alikuwa akiwasiliana nao kwa kipindi chote cha masomo yake, na alipowajulisha kuwa amehitimu, wazazi wake walifurahi sana. Hata hivyo, ilikuwa ni miezi mitatu sasa hawajasikia chochote kutoka kwake. Hali hii iliwaacha na maswali mengi na wasiwasi juu ya hali na mahali alipo binti yao.

Wakati malumbano ya bibi na bwana yakiendelea, Mika alipita katika vijia vya kijijini kwa uangalifu, akitafuta nyumba ya wazazi wa Amina. Hakuwa mgeni katika kijiji hicho, lakini hakukumbuka vyema njia ya kumfikisha nyumbani kwa Mama na Baba Amina. Alikuwa amevaa suruwali nyeusi na shati la samawati; koti lake likiwa mkononi. Alikuwa amebeba begi zito mgongoni, kichwani kaelemewa

na mawazo. Huku akiangalia kila nyumba kwa makini, alijikuta amefika mbele ya nyumba ile bila kutambua. Sauti kubwa ya redio ikitangaza mechi ya mpira ilisikika upande wa pili wa nyumba.

"Wenyewe?"

Sauti ya Mika ilisababisha taharuki ya ghafla. Mzee Mabimbi aliinuka haraka na kuchomoa panga lililokuwa limefichwa chini ya nyasi karibu na nyumba.

"Nani wewe?" Mzee Mabimbi aliuliza kwa wasiwasi, panga mkononi, tayari kulitumia.

"Samahani, mimi ni Mika, rafiki yake Amina."

Mzee Mabimbi alimwangalia kwa makini. Alipomtambua, uso wake ulibadilika na kuwa wa furaha. "Ah, Mika, karibu sana! Samahani, nilidhani ni hawa vijana wanaosumbuasumbua hapa mtaani."

Mama Amina kuondoa tahayari alisema kwa utani, "Baba Amina acha vituko, hujui labda Mika amekuja kulipa mahari ya Amina."

Mzee Mabimbi akacheka na kuongeza, "Kweli. Tulianza kufikiria umekuwa tajiri sana, huna muda wa kuja kutuona."

"Jamani, sijafika hapa kwa ajili ya mahari," Mika alijitetea huku akicheka. "Huwa natamani kuwaona lakini na mimi nilikuwa Uingereza."

Mika baada ya kunywa glasi ya maji na kufurahia kidogo matangazo ya mpira pamoja na wazazi wa Amina, aliwaambia, "Nina habari njema na mbaya, sijui mnataka kusikia ipi kwanza."

"Bora uanze na habari mbaya," Mzee Mabimbi alisema.

Wasiwasi wa Mama Amina uliongezeka na macho yake yakajaa hofu. "Kwani kuna nini, Mika? Amina yupo salama?

"Ndio, yupo salama, mama," alijibu Mika kwa sauti tulivu. "Hata hivyo, hayupo huru."

"Mwanangu yupo jela?" Mama Amina aliuliza kwa taharuki.

"Hajafungwa jela," Mika alijibu. "Amina aliandaa maandamano makubwa ya kupinga ubaguzi wa rangi. Baadhi ya wazungu wanaotetea ufahari wa watu weupe hawakufurahia na wametishia kumdhuru. Kwa sababu hiyo, wamefungua kesi dhidi yake. Kwa sasa, amezuiliwa kuwasiliana na mtu yeyote isipokuwa wakili wake hadi kesi itakapomalizika."

Mama Amina alishtuka na kusema, "Hii ni habari mbaya sana.

Tunamsaidiaje?"

"Hao wazungu wanafikiri wanaweza kututisha! Tutauza shamba lililobakia kuhakikisha Amina anapata haki yake." Mzee Mabimbi aliongea kwa hasira, kisha akashusha sauti, "Ulisema una habari nyingine pia. Ni ipi hiyo?"

Mika alifungua begi lake na kucheka kidogo kabla ya kujibu, "Begi nililokuja nalo limejaa zawadi kutoka kwa Amina." alitoa mfuko mmoja baada ya mwingine kutoka kwenye begi na kuweka mezani. "Na hii ni hundi ya fedha inayotosha kubadilisha makazi yenu kuwa kasri na bustani yake."

Wakati huo huo, mtangazaji redioni alisikika akitangaza goli. Mzee Mabimbi alipandisha sauti ili kusikia vizuri. Baada ya kusikia Yanga wamepata goli la pili dakika za mwishoni, alipiga miguu chini kwa hasira.

"Wajinga hawa, watarudisha saa ngapi?"

"We mzee nawe punguza huo ushabiki wako!" Mama Amina alikebehi huku akinung'unika,

"Ona, mwanangu kabebeshwa zigo la kesi na bado ametutumia zawadi nyingi namna hii!" "Haki haikai na batili, naamini Amina atashinda vita hii na kuwa huru.

Hakika yeye ni binti jasiri." Mika alisemaa kwa msisitizo.

# Safari ya Mabadiliko

Irene Sarakikya

Saranga, kijiji kilichojificha nyuma ya milima, kilikuwa kimejaa shughuli. Mashamba yalilalamika kwa kiu ya maji, ng'ombe walirudishwa zizini baada ya safari ndefu za kutafuta malisho na safari za kila siku za wanakijiji kwenda mashambani hazikuwahi kwisha. Maji ya mito yalitekwa na kusambazwa katika eneo lote la tambarare. Nyasi ndefu, zilizokauka, zilisikika upepo baridi ulipovuma, ukiwalazimisha wakazi wa Saranga kuvaa makoti na masweta. Nyumba za udongo zilizoezekwa kwa nyasi zilikuwa ndiyo makazi ya wengi. Barabara za vumbi zenye mashimo yaliyojaa maji wakati wa masika zilikuwa ni kawaida; na watoto walilazimika kudamka kabla ya kupambazuka na kutembea umbali mrefu kwenda shule.

Katika watoto hao alikuwemo Halima. Kila siku, alifanya safari ndefu kutoka nyumbani kwao hadi shuleni, akipitia njia zenye vumbi na mashimo, macho yakiwa yamezoea giza lililokuwa sehemu ya maisha yake ya kila siku wakati anakwenda shuleni. Halima alikuwa na umri mdogo lakini mwenye ndoto kubwa. kila siku asubuhi alitoka nyumbani kwao akiwa amebeba ndoo ya maji kichwani na vitabu vya shule mkononi. Alitembea kwa ustadi mkubwa, akipita mashamba na vichaka vya kijiji chao. Ngozi yake laini ya kuteleza ya rangi ya chokoleti na sura yake angavu vilimulikwa na mwanga hafifu wa jua lilipoanza kuchomoza, ukiakisi macho yake maangavu yaliyobeba dhamira thabiti.

Siku moja jioni, baada ya kutoka shule Halima alikuwa akiandaa chakula cha jioni. Kulikuwa na baridi kali, kanga alizovaa hazikuweza kuzuia baridi iliyomkumba. Alipita kwenye kichochoro upenuni mwa nyumba yao akaingia shambani kuchimbua muhogo. Alikumbana na udongo mwekundu uliokauka kama jiwe. Chapuchapu alivuna mihogo ya kutosha kwa mlo wa siku ile, akaingia jikoni kwa kupapasa kuta za udongo ili asijikwae. Macho yake yalipozoea mwanga hafifu uliotoka mekoni alikuchukua sufuria mbili, akaandaa mihogo na chai. Saa moja kamili familia yake ilikusanyika kupata chakula cha jioni. Halima alikula muhogo wake polepole, akashushia na chai ambayo ilisaidia kidogo kumpa joto la muda mfupi. Baada ya kula alikusanya vyombo vichafu akatoka navyo nje kuviosha.

Baba yake Halima alikuwa mkulima na mjenzi. Yeye ndiye aliyefanya ujenzi wa boma wakati serikali ilipowataka wananchi wachangie ujenzi wa shule.

Serikali iliahidi kuezeka majengo hayo na kugharamia mambo mengine kama ripu, milango na madirisha. Mama yake Halima alifanya biashara ndogondogo, kama vile kuuza maandazi na chakula kwa wafanyakazi, na vitafunwa kwa wanafunzi. Halima, pamoja na marafiki zake, Matilda na Banza, walikuwa watoto hodari katika masomo na walijituma pia katika kusaidia kazi za nyumbani.

Siku moja wazazi wa Halima waliitwa shuleni. Walifika bila kuchelewa. Mwalimu aliyekuwa nyuma ya meza iliyotengenezwa kwa mvule aliwakaribisha na kuuliza, "Nyie ndo wazazi wa Halima?". Karatasi zilizagaa mezani, na mwalimu alijaribu kuzipanga wakati akiongea.

"Ndiyo sisi," wazazi walijibu kwa pamoja.

Mwalimu aliendelea, "Kwanza, hongereni kwa kumlea mtoto wenu vizuri. Ana tabia njema na ana bidii katika masomo. Tumeagizwa tupeleke wanafunzi wenye viwango bora wakajiunge na chuo kipya cha teknolojia ya mawasiliano kilichojengwa mjini. Tulimpendekeza Halima na amechaguliwa. Kama wazazi mtaridhia, ataondoka kwenda mjini ili apate nafasi hiyo."

Wazazi wa Halima walijawa na furaha kubwa na walikubali mara moja. Habari kama hiyo zilikuwa zimefika pia kwa wazazi wa Matilda na Baza, na wao pia waliridhia.

Gari lililowabeba Halima, mwalimu, na wanafunzi wenzake Matilda na Banza lilipoingia mjini, Halima alikuwa amezama katika mawazo. Alipotazama nje ya dirisha, macho yake yalikumbana na mandhari ya majengo marefu na maduka yaliyojipanga kwa mistari pembezoni mwa barabara. Alipofika chuoni, alishangazwa na majengo marefu ya rangi nyeupe yaliyozunguka uwanja mkubwa. Maua ya aina mbalimbali na nyasi za kijani ziliipamba bustani. Jua lilikuwa likielekea mapumzikoni upande wa magharibi, na mawingu yakielea huku na kule. Kila mahali alipogeuka aliona ngazi zinazoelekea kwenye majengo mengine. Uwanja ulikuwa umezungukwa na miti iliyoyumba huku na kule ilipopigwa na upepo.

Jua lilipochomoza siku iliyofuata, Makamu Mkuu wa Chuo aliwaita Halima, Matilda, na Banza ofisini. Alikuwa ameketi kwa utulivu nyuma ya meza ya mpingo. Madirisha yalikuwa wazi, yakiruhusu mwanga wa jua la asubuhi kuingia ofisini. Aliwapa Halima, Matilda, na Banza maelekezo ya chuo na kuwatambulisha kwa mtu atakayewaongoza kuyafahamu mazingira.

Siku zilivyopita na miezi ilivyokwenda ndivyo Halima, Matilda, na Banza walivyopata mafanikio makubwa kimasomo, wakipokea tuzo mbalimbali ikiwemo ziara na safari za matembezi sehemu mbalimbali.

Siku moja, Matilda aliamka usiku na alipopita kwenye kitanda cha Halima,

aliona mwanga hafifu wa simu. Alisimama kidogo kujiaminisha kuwa macho yake hayakuwa yanamdanganya, lakini aliamua kuendelea na safari yake. Siku chache baadaye, Matilda alizungumza na Banza kuhusu kile alichokiona. "Unajua Halima ana simu siku hizi?" Matilda alianza.

"Simu?" Banza aliuliza kwa mshangao. Kwa hali yake kiuchumi, ilikuwa haiyumkini Halima kumiliki simu, hivyo rafiki zake walipata wasiwasi kuhusu mwenendo wa mwenzao. Waliamua kumfuata kutaka kujua zaidi. "Mambo Halima," Matilda alianza.

"Poa, hatujaonana muda mko poa?" Halima aliuliza kwa upole.

"Tuko vizuri, wewe tu. Umebadilika sana siku hizi," Matilda alisema.

"Ndiyo, bila shaka nitakuwa nimebadilika. Nimejifunza mengi hapa chuoni, ambayo nataka niyatumie kusaidia wengine, hasa wa kijijini kwetu Saranga," Halima alijibu kwa kujiamini.

Matilda na Banza walitabasamu, wakifurahishwa na majibu ya Halima. Walitazamana bila kusemezana, wakaamua kuvuta subira. Walishindwa kumuuliza kuhusu umiliki wa simu, hivyo waliondoka bila kupata jawabu.

Kitu ambacho hawakubaini ni kwamba Halima alifanikiwa kununua simu kwa kuweka akiba ya posho ya matumizi. Wakati wanachuo wenzake walipofuja posho zao kwa kununua *viwalo* kila uchao na rangi za *ndimi* ili wawe warembo zaidi, yeye alirizika na nguo chache nadhifu alizokuwa nazo na muonekano asilia.

Jumamosi moja adhuhuri, Halima, Banza, na Matilda walikwenda mjini matembezini pamoja na wanafunzi wenzao. Ratiba ya chuo iliruhusu wanafunzi kuwa huru siku za Jumamosi na Jumapili. Walizunguka madukani, wakapitia kwa mchuuzi wa magazeti. Macho yao yalikamatwa na kichwa cha habari cha gazeti moja, 'Mwanafunzi Akamatwa na Madawa ya Kulevya". Matilda alitoa noti ya shilingi mia tano na kununua gazeti hilo. Njaa ilipowakaba, waliingia kwenye mgahawa kupata chochote. Waliagiza chakula na soda. Wakati wanasubiri, walisoma na kujadili ile habari.

Habari ilimhusu mwanafunzi wa chuo chao. Majadiliano kuhusu sakata lile waliibua mjadala na tafakuri kuhusu athari za maamuzi mabaya.

Baada ya kula, waliendelea na mazungumzo yao, wakibadilishana mawazo kuhusu umuhimu wa kufanya maamuzi sahihi. Hapo ndipo Matilda na Banza walipopata fursa ya kumuuliza Halima kuhusu umiliki wa simu.

"Si hivyo mnavyodhani," aliwatuliza akili kwa kuwaambia jinsi alivyoipata simu yake na anavyoitumia kuchochea mabadiliko chanya kwa vijana wenzake.

Miezi kadhaa baadaye, Halima alijiunga na shirika moja linalojishughulisha na kunusuru vijana dhidi ya uraibu wa madawa ya kulevya kama mwanafunzi wa kujitolea. Walipomaliza mafunzo ya stashahada, Banza na Matilda walirudi kijijini kusubiria matokeo, lakini Matilda alijiunga na mafunzo maalum ya uwezeshaji ngazi ya jamii.

Siku moja, kabla ya kupata matokeo, Matilda na Banza walipokea barua ifuatayo,

*Wapendwa Matilda na Banza,*

*Salaam!*

*Natumaini hamjambo na mnaendelea vizuri na shughuli za maendeleo huko nyumbani. Kwa upande wangu, naendelea vizuri. Nimetaka niwaandikie kwa kuwa yanayonitokea hivi sasa si matokeo ya juhudi zangu peke yangu. Yote yalianza siku ile tulipokwenda mjini pamoja. Ile habari tuliyoisoma gazetini na mazungumzo yetu vilinipa hamasa ya kufanya jambo.*

*Mazungumzo yetu siku ile yalinipa mwanga mpya. Badala ya kujitafutia umaarufu, niliamua kutumia mitandao ya kijamii kushirikiana maarifa na kuwatia moyo vijana wenzangu. Safari yangu hii ilinipelekea kufahamiana na watu mbalimbali, wakiwemo wale walio katika mapambano dhidi ya madawa ya kulevya.*

*Katika kazi yangu ya kujitolea, nimeshirikiana na wenzangu kuwaelimisha vijana kuhusu madhara ya madawa ya kulevya, na kushiriki katika mikakati ya kuyadhibiti. Hii pamoja na kozi fupi niliyofanya, vilinipa uelewa mpana na kunikuza kama kiongozi. Matokeo yake, nimepata nafasi ya kuendelea na masomo ya uongozi kwenye fani ya maendeleo ya jamii. Masomo yangu yatachukua miaka mitatu.*

*Ninawashukuru kwa kunipa moyo na kunisaidia kufikia hapa. Msisahau kunifikishia salaam zangu kwa wazazi na vijana wenzetu huko Saranga.*

*Nawatakia kila la kheri.*

*Wasalaam mimi rafiki yenu, Halima.*

# Nuru katika Giza

Aneth Mirambo

Ilikuwa asubuhi tulivu katika jimbo la Weno. Mwanga wa jua ulipenya dirishani mwa ofisi ya Bwana Jabilo. Jabilo alikuwa mfanyabiashara maarufu mwenye ushawishi na mmiliki wa hoteli maarufu ya Jabilo Resort. Mezani pake palisheheni makabrasha na mapambo anuai yaliyoendana na hadhi yake. Ghafla, simu yake ya kiganjani iliita, ikavunja kimya kilichokuwepo. Sauti ya Yoki, mmoja wa wafanyakazi wake wa siri ilisikika upande wa pili.

"Halo, Jabilo hapa," aliitika kwa sauti yenye mamlaka.

"Eeh, Bwana Jabilo," Yoki alijibu harakaharaka. "Tumekamilisha kazi uliyotuagiza."

"Vizuri, vizuri sana. Tutakutana baadaye kwa maelezo zaidi," Jabilo alijibu, akitabasamu kwa kuridhika.

Kwenye kona ya ukumbi, nje ya mlango wa ofisi, Bi. Nuru alisimama akiwa ameshikilia sinia lenye vikombe vya chai na mikate. Alikuwa amevalia aproni nyeupe iliyoakisi mwanga wa jua. Nywele zake nyeusi zilivutwa nyuma na kufungwa kishungi cha duara. Macho yake makali yalikuwa yanasoma kila kitu kilichokuwa kikiendelea ndani ya ofisi, na uso wake ulionesha azimio la siri alilokuwa nalo moyoni. Aliganda pale aliposimama juu ya sakafu iliyong'aa kwa usafi kama mlinzi mwaminifu wa hoteli hiyo.

Siku iliyofuata, habari za kutia wasiwasi zinazohusu kifo cha Mheshimiwa Kabino Mbunge wa Weno, kiongozi shujaa mpendwa na watu zilisambaa. Bi. Nuru, alihudhuria mazishi na alihisi kulikuwa na kitu kisicho cha kawaida kuhusiana na kifo kile. Katikati ya mazishi yenye kuhuzunisha moyo, alijiinamia mbali na umati uliokusanyika kutoa heshima zao za mwisho. Bi. Nuru aliamua kufanya uchunguzi wa siri ili kufichua ukweli juu ya kifo hicho.

Baada ya wiki nne, Tume ya Uchaguzi ilitangaza uchaguzi mdogo wa kujaza nafasi iliyoachwa wazi na marehemu. Jabilo alikuwa wa kwanza kujitokeza kutangaza azma yake ya kugombea nafasi hiyo. Bi. Nuru naye, akiwa amechukizwa na kifo cha ghafla cha Mbunge wake mpendwa, aliamua kuchukua fomu kuchuana na bosi wake ambaye alimuhisi kuhusika na kifo kile.

Bi Nuru alipoanza kampeni yake yenye lengo la kuendeleza mabadiliko na uadilifu aliouanzisha Mbunge Kabino, Jabilo alimfukuza kazi bila notisi. Licha

ya kumfukuza, alimkejeli, "Wewe una sifa gani ya kukuwezesha kufanya siasa!" alisema Jabilo kwa kejeli.

"Na kwa nini siwezi?" Bi. Nuru alijibu kwa ujasiri.

"Kwa sababu wewe ni mwanamke usiyejua chochote kuhusiana na siasa, mfanyakazi duni ambaye hata ungeachiwa ofisi tu uiendeshe, huna huo uwezo. Ondoa jina lako nikurudishe kazini usije ukatuharibia jimbo."

"Kufukejeli zako hazinizuii kugombea na hakutanizuia kushinda!" Bi. Nuru alisema akimkazia macho Jabilo.

Jabilo alicheka kwa dharau. "Tutaona kama wapiga kura watamchagua mfanyakazi wa zamani wa Jabilo."

Licha ya kejeli na dharau kutoka kwa Jabilo, Bi. Nuru hakurudi nyuma. Kampeni yake ilizidi kukua, ikiwavutia wengi waliotamani mabadiliko. Mojawapo ya ahadi kuu katika kampeni yake ilikuwa ni kufichua ukweli kuhusu kifo cha Kabino. Akihutubia mikutano ya hadhara kwa hamasa kubwa, aliwahimiza watu kufikiria kuhusu mustakabali wa jamii yao.

"Ni wakati wa mabadiliko," Bi. Nuru aliwaambia wananchi kwa msisitizo. "Ni wakati wa kuwa na sauti katika siasa yetu, bila kujali jinsia au asili, na ni wakati wa kufichua ukweli kuhusu kifo cha Mbunge Kabino."

Jumapili moja tulivu, mitaa ilikuwa kimya, watu wengi wakifurahia mapumziko baada ya kutoka kwenye pilikapilika za kampeni. Lakini Bi. Nuru alikuwa na mpango tofauti. Alipenya kimyakimya kwenye korido zilizokuwa tupu za jengo la hoteli ya Jabilo. Kwa hatua za kunyata alielekea ofisini kwa Jabilo. Hakukuwa na mtu yeyote karibu. "Hii ni fursa nzuri," aliwaza. "Natumaini hajabadili nywila ya kufungulia mlango." Alipofika ofisini kwa Jabilo, aliweka tarakimu alizokuwa anazikumbuka vema akakinyonga kitasa kikaachia, mlango ukafunguka taratibu bila kelele.

Mara baada ya kuingia, haraka aliwasha kompyuta ya Jabilo. Vidole vyake vilicheza juu ya kicharazio huku akihangaika kuruka viunzi vya kiusalama, akiwa amebana pumzi yake. Hatimaye, aliweza kufungua barua pepe na kupata mawasiliano mengi kati ya Jabilo na Yoki. Yaliyomo yalikuwa ya kushangaza. Yalisheheni maelezo ya kina ya mipango ya shughuli zao haramu ikiwemo viashiria vya kilichotokea kwa Kabino.

Moyo wake ulidunda kwa nguvu. Alishindwa kuamini upeo wa njama zao.

Akiwa bado katika mshtuko kutokana na ufunuo huo, Bi. Nuru haraka alituma ujumbe kwa mwandani wake kuomba msaada kutokana na hatari aliyohisi iko mbele yake. Mikono yake ikitetemeka, alihifadhi kila kitu kwenye diski yake

harakaharaka. Alipokuwa karibu kuondoka, alisikia sauti ya gari likiwasili nje. Ilikuwa ni Jabilo.

Bi Nuru alirudishia kila kitu upesi akakimbilia mlangoni ili atoke bila kushtukiwa. Alipofika mlangoni tu, alikutana uso kwa uso na Jabilo.

"Unafanya nini hapa?!" Jabilo aliuliza kwa hamaki.

Bi. Nuru, alikuwa ameganda kwa hofu, lakini alijikaza, akajibu, "Ninatafuta ukweli, Jabilo."

Jabilo alimkodolea macho, kisha akapiga kelele kuwaita walinzi, "Hiki ni nini, mnalinda nini hapa?!"

Walinzi wakionekana kuchanganyikiwa. "Lakini, Bi. Nuru ni..."

"Alifutwa kazi wiki mbili zilizopita!" Jabilo aliwakatiza kwa hasira.

"Samahani, Bwana Jabilo, hatukujua..."

"Hakuna samahani! Mshughulikieni sasa hivi!" Jabilo aliamuru. "Mpelekeni alikokwenda Kabino. Hakikisheni hamuachi ushahidi."

Walinzi walimkamata Bi. Nuru na kuanza kumshambulia kwa makonde mazito na mateke yaliyolenga kummaliza kabisa. Bi. Nuru alijaribu kujikinga, lakini walinzi hao walimzidi nguvu. Kila pigo lililompata lilimfanya ahisi kama mwili wake unavunjika vipandevipande. Kilio chake cha maumivu kiliishia kwenye korido tupu za jengo hilo.

Baada ya muda usiojulikana wa kupigwa, Bi. Nuru alipoteza fahamu. Mwili wake uliokuwa unavuja damu ulilegea. Walinzi, waliona hawana tena haja ya kuendelea. Mwili wake ukiwa unaning'inia na kutepeta kama mlenda, walimbeba mpaka nje ya jengo.

Nje, gari lilikuwa linawasubiri. Walimkunja Bi. Nuru kama mzigo, wakamtupa kwenye buti la gari bila kujali utu wala huruma. Sauti ya buti likifungwa ilikuwa kama alama ya mwisho ya hatua yao ya kikatili na maisha ya Bi. Nuru. Gari likaondoka kwa kasi kuelekea kusikojulikana, Bi. Nuru akiwa amelala tuli kama nusu mfu.

Alipozinduka, Bi. Nuru hakujua ni saa au siku ngapi zilikuwa zimepita tangu aingie ofisini mwa Jabilo na kukutana na kipigo cha mbwa mwizi. Alikuwa kwenye kitanda cha hospitali, na pembeni yake alisimama muuguzi aliyetabasamu na kusema;

"Umeamka hatimaye, hongera Mheshimiwa Mbunge."

“Nimefikaje hapa?” Bi. Nuru aliuliza kwa sauti dhaifu.

“Ujumbe ulioutuma ndio uliokoa maisha yako,” muuguzi alijibu.

“Nani aliniokoa?” Bi. Nuru aliuliza, akihangaika kuvuta kumbukumbu.

“Aliyepokea ujumbe wako aliwatumia polisi, wakaenda kumkamata Jabilo. Alipobaini kuwa kila kitu kimejulikana, Jabilo aliwapigia simu walinzi wake akawaamuru wakurudishe, ukawahishwa hospitali.” muuguzi alifafanua.

“Na vipi kuhusu uchaguzi?” Bi. Nuru aliuliza, macho yake yakionyesha wasiwasi.

“Nimekupa hongera, hukusikia?” muuguzi alisema kwa tabasamu. “Wapiga kura waliposikia umepatikana na umelazwa hapa, waliamua kukupigia kura.”

“Ina maana nilipoteza fahamu kwa zaidi ya wiki mbili?” Bi. Nuru aliongea kwa mshangao.

Muuguzi alimuitikia. “Pole, Mheshimiwa Mbunge.” alisema kwa heshima, akaendelea, “Lakini sasa uko salama, na umekuwa chaguo la watu.”

# Lazima Nifanikiwe

Cecilia Mgimbila

Helena aliketi chini ya kivuli cha mti mkubwa karibu na jiwe kubwa ililokuwa pembeni kidogo mwa nyumba yao. Eneo hili lilibeba kumbukumbu za tukio la kusikitisha lililotokea miezi michache iliyopita na kusababisha kifo cha baba yake mpendwa. Akiwa analitafakari tukio lile, alijiuliza kwa sauti, "Kwa nini nyoka yule alimgonga baba yangu lakini?" Alihisi kuna mchezo uliochezwa nyuma ya pazia. Helena alitamani angekuwepo pale wakati baba yake aliposhambuliwa na nyoka, labda angebaini kitu. Kifo cha baba yake kilikuwa kimeondoa furaha ndani ya familia yao. "Laiti baba angalikuwa hai, angeyashughulikia yote yanayotusibu." Helena aliendelea kuwaza kwa majonzi.

Kwa mbali alikuwa akimtazama mama yake, ambaye alikuwa na tumbo kubwa lenye kiumbe kinachokua ndani yake. Mama alikuwa ameketi kwenye mkeka akiwa kaegemea mikono yake na kuvuta pumzi kwa shida. Helena alijaribu kulinganisha majukumu makubwa yaliyokuwa mbele yake na umri wake wa miaka kumi na sita. Alikumbuka jinsi baba yake alivyokuwa mwepesi wa kushughulikia kila jambo gumu lilipotokea. Lakini sasa, majukumu yote yalimwangukia yeye na mama yake.

"Helena, Helena!" sauti ya Mama ilimtoa Helena katika lindi la mawazo.

"Helena!" Mama aliita tena.

"Naam!" Helena aliitika huku akishuka juu ya jiwe na kuelekea alikokuwa ameketi mama yake.

"Helena inabidi umkamate kuku mmoja ukamuuze." aliongea Mama huku akiwa ameipakata mikono yake na kumtazama mwanae usoni.

"Kuku tena! Ndio mali pekee tuliyobakiwa nayo, mama."

"Ukichelewa tutampoteza," mama yake alimjibu kisha akatema mate chini.

"Tutampoteza nani?" aliuliza Helena.

Mama Helena alimkazia macho huku akilipapasa tumbo lake. Hali ile ilimuonesha Helena ya kuwa mama yake hakuhitaji mzahamzaha wakati ule.

"Sawa Mama." Helena alijibu kinyonge akaondoka kuelekea nyuma

ya nyumba yao kutekeleza agizo la mama yake. Aliwakuta kuku watatu wakidonodonoa na kuparuaparua ardhini. Aliwatazama kwa makini ili kujua yupi angeuzika kwa urahisi. Aliamua kumkimbiza jogoo mmoja aliyenona. Jogoo alikimbia lakini alinasa kwenye miiba. Helena alimrukia kama paka shume lakini jogoo alifurukuta akawahi kutoka na kumuacha Helena akiwa amejikwaa na kuangukia kwenye miiba.

"Aaaah asiii...!" aliguna Helena wakati anajizoazoa. Alinyanyuka na kuchomoa miiba iliyokuwa mwilini mwake iliyopenya kwa urahisi kwenye shati la mikono mifupi na kaptula aliyokuwa amevaa. Aliendelea kumkimbiza jogoo ambaye alikwishaingia kwenye vichaka vikavu vilivyoparua mwili wake.

"Nikikushika nitakufundisha adabu," Helena alijisemea akiwa amekunja ndita. Jogoo alikimbia na kuingia jikoni akajificha kwenye rundo la kuni zilizokuwa karibu na jiko la mafiga matatu. Helena alimfuata hukohuko jikoni, akafunga mlango wa bati lenye kutu na kuanza kuzipangua kuni zile. Jogoo aliruka lakini Helena alimuwahi akamrukia na kumkamata mguu. Jogoo alipigapiga mbawa zake lakini Helena alimbana kwapani akamfunga mguu yote miwili kwa kamba.

Sauti yenye maumivu makali ilimvamia Helena masikioni mwake, ikamshitua kutoka katikati ya harakati za kukamatana na kuku. Alimweka chini kuku na kukimbia nje alipokuwepo mama yake. Alimkuta akiwa ameegemea ukuta, akiwa anapumua kwa shida, mkono mmoja umeshikilia tumbo lake na mwingine unakipapasa kiuno chake. Helena aliita kwa hofu, "Mama, Mama?"

"Ti…Helena!?" mama yake alikuwa anagugumia kwa maumivu.

"Hah! hah! hah! Mama, Mama?" Helena aliendelea kumwita mama yake huku akihema kwa hofu.

"Mh! Helena...!!!, Kaombe-e…" Mama Helena alijaribu kutoa maelekezo lakini yaliishia njiani.

"Ni... nikaombe nini?" Machozi yalianza kumtoka Helena, akamkumbatia mama yake na kumhoji apate kujua nini kilimpasa afanye.

"Msa-a-ada mwanangu mmh! Aahah!"

Helena aliutoa taratibu mkono wake mabegani mwa mama yake na kutimua mbio, akashika njia nyembamba iliyosongwa na nyasi ndefu kiasi. Kwa mbali ilionekana nyumba ya msonge iliyoezekwa kwa nyasi. Mzee wa makamo alikuwa ameketi kwenye kigoda mbele ya nyumba hiyo. Chini alikuwa amejifunga msuli, juu amevalia fulana na koti la mikono mirefu na baraghashia kichwani.

Helena alifika kwenye nyumba ile akihema. Bila hata salaam, Helena alimvuta yule mzee mkono akasema, "Twendeehhh!"

“Wapi?” alihoji Mzee Jumbe huku akimtazama Helena kwa macho yenye viulizo vingi.

“Mama aaah, mama aaah, nyumbani!” Helena alijibu huku akimvuta. Mzee Jumbe hakuongeza neno. Alimfuata Helena kuelekea kwao. Walifika nyumbani wakamkuta mama Helena jasho linamtoka, anagugumia akiwa ameuma meno. Helena aliingia ndani na kutoa baiskeli.

“Shika vizuri.” Mzee Jumbe alimwambia Helena alipomuona akitoa baiskeli. Helena alikamata usukani wa baiskeli na kulibana tairi la mbele kwa miguu yake.

Mzee Jumbe alimwinua Mama Helena taratibu, akamkongoja na kumpakia kwenye baiskeli.

“Njoo huku umshike.” Mzee Jumbe alisema akiwa ameshika kitako cha baiskeli kwa mkono mmoja na mwingine akiwa amemshika mama Helena. Helena aliutoa mguu wake taratibu kwenye tairi na kuachia usukani huku akiwa ameshika koti alilokuwa amevaa Mzee Jumbe. Alirudi nyuma taratibu akamwachia Mzee Jumbe ashike usukani na kuikokota baiskeli kuelekea zahanati.

Walipofika zahanati, Mzee Jumbe alimwagiza Helena aende mapokezi akamwite nesi. Helena alitimua mbio akaingia ndani akasimama mkabala na mlango wenye kibao kilichoandikwa MAPOKEZI. Alimkuta muuguzi aliyevalia gauni fupi la kijani aliyekuwa anafunuafunua karatasi zilizokuwa juu ya meza.

“Dada! Dada! Kuna mgonjwa nje kazidiwa.” Helena alisema kwa sauti ya juu huku akitweta kwa taharuki.

“Punguza sauti kuna wagonjwa wengine wenye maumivu humu.” alisema yule dada akiendelea kufungua karatasi. Helena aliangaza macho huku na kule lakini hakuona mgonjwa mwingine zaidi ya mama yake. Taratibu nesi alisimama akafungua mlango na kutoka nje.

“Yuko wapi huyo mgonjwa mwenyewe?” aliuliza yule nesi akiwa ameshika kiuno.

“Yupo huku.” Helena alijibu akiwa amenyoosha kidole kuelekea alipokuwepo mama yake. Yule nesi akamfuata nyuma hadi mahali alipokuwepo Mama Helena na Mzee Jumbe.

“Pole kwa safari baba.” alisema yule nesi na kusogea moja kwa moja hadi alipokuwa Mama Helena. Alikuwa ameegemea ukuta na ameshika kiuno kwa mkono mmoja mwingine ukiwa unalisuguasugua tumbo lake.

“Asante Mama.” alijibu Mzee Jumbe.

“Njoo tusaidiane kumuingiza ndani,” aliongea nesi akiwa anajaribu kumkongoja Mama Helena. Mzee Jumbe alisaidiana naye wakaenda hadi kwenye mlango wenye kibao kilichoandikwa WAZAZI. Waliingia ndani huku Helena akifuata nyuma. Ndani ya chumba kulikuwa na chumba kingine kilichoandikwa LEBA. Ndani kulikuwa na kitanda cha chuma na godoro lililokuwa limetandikwa shuka la kijani. Walimkalisha Mama Helena kitandani kisha nesi akasema, “Mzee unaweza kwenda nje.”

“Sawa Mama.” alisema Mzee Jumbe akatoka nje.

“Na wewe unasubiri nini? Nenda nje.” Nesi alimwambia Helena.

Helena aliinamisha kichwa chini na kutoka nje. Alimkuta Mzee Jumbe akiwa amekaa juu ya jiwe lililokuwa chini ya mti nje ya zahanati.

“Helena njoo.” Mzee Jumbe alimwita kwa sauti na kwa ishara ya mkono. Helena alisogea taratibu akiwa ameinamisha kichwa chini. Mzee Jumbe alimshika mkono na kumvuta aketi karibu naye.

“Mama atakuwa salama usiwe na wasiwasi. Halafu wewe ni msichana mkubwa sasa, jikaze.” Mzee Jumbe alimfariji Helena huku akimpapasa mgongoni na kumuaga.

Helena alitikisa kichwa, akafuta machozi yaliyokuwa yakimbubujika. Mzee Jumbe alipanda baiskeli na kuondoka huku Helena akiwa kimya, anamtazama.

Helena akiendelea kusubiri. Nusu saa baadaye alimwona nesi akitoka akiwa anatoa mipira aliyokuwa amevaa mikononi na kuitupa ndani ya ndoo ya taka. Helena alinyanyuka na kumfuata nesi ili aulizie hali ya mama yake. Nesi aliingia moja kwa moja hadi kwenye chumba cha mapokezi. Helena alimfuata na kumuuliza,” Naruhusiwa kumuona?”

“Bado. Kwanza kamwite baba yako.” alijibu yule nesi kwa mkato.

Kwa unyonge Helena akajibu, “Hayupo.”

“Kaenda wapi?”

“Alishafariki.”

“Na yule uliyekuja nae ni nani?”

“Ni jirani yetu.”

“Hee makubwa! Sasa pesa anatoa nani?” Nesi alihoji akiwa ameshika kiuno.

“Hela ya nini?”

“We mtoto, sihitaji maswali,” alisema yule nesi akimnyooshea kidole Helena ambaye alikuwa anamkodolea macho tu pasipo kuwa na jibu la kumpa. “Kimbia kawaambie ndugu zako inahitajika elfu sitini sasa hivi.”

“Ya nini?” alihoji Helena kwani hakujua kiasi kikubwa hivyo cha pesa ni cha nini na angekipata vipi.

“Sihitaji maswali fanya nilichokwambia,” alifoka yule nesi.

“*Asa* wakiniuliza ya nini niwaambiaje?” Helena aliendelea kuhoji akiwa amemkodolea macho nesi yule,

“Nenda kawaambie ndugu zako inahitajika hela kwa ajili ya vifaa vya kujifungulia mama na hela ya kitanda kwa sababu atatakiwa kukaa hapa kwa muda baada ya kujifungua, haya nenda upesi.”

“Lakini...!!!”

“Lakini nini?” nesi alimkata kauli.

“Akina mama wajawazito na wazee wanapatiwa huduma bure.” Helena *alikomaa*.

“Nani kakwambia? Nenda kachukue hela acha kufanya mzaha.”

“Mimi nilisikia redioni.”

“Ukiendelea kufanya ubishi utampoteza mama yako bure. Fanya hima, hakuna muda wa kupoteza.” Helena alilia aliposikia maneno ya kifo. Alipiga magoti na kushika pindo la gauni la nesi.

“Nakuomba umsaidie mama yangu, hatuna hela.”

“We hebu niachie!” alisema nesi huku akivuta gauni lake lililokuwa limeng’ang’ania mikononi mwa Helena.

“Lakini mama yangu anapaswa kutibiwa bure.”

Nesi alimtazama Helena na kubetua midomo yake.

“Mama yangu lazima atibiwe. Haiwezekani.” Helena aliendelea kulalama.

“Sipendi kubishana na watoto. Toka ukapigie kelele zako huko nje.” Nesi alisema akaanza kumsukuma Helena atoke nje.

Helena alipepesuka lakini hakudondoka na hakuondoka. Machozi yaliendelea kumtoka lakini aliendelea kumuelimisha nesi yule.

“Wajawazito wanatakiwa kutibiwa bure, usitoe wala kudai fedha. Hivyo

ndivyo nilivyosikia redioni." Hakutaka kumpa yule nesi nafasi nyingine ya kuzungumza. "Sasa nitatembea kwa mguu hadi ikulu nikaulize kama taarifa hizi ni za uongo. Mama yangu akifa mikononi mwako, ujue na wewe huna maisha . . ."

"Fumba mdomo wako," nesi alifoka, lakini akionekana kutishika. "Usiniletee uchuro mimi. Mama yako atatibiwa, kaa kitako hapo chini usubiri." Nesi alimtazama Helena na kuingia kwenye chumba kimojawapo. Hatimaye aliibuka na kisahani chenye vifaa vya kujifungulia. Aliingia nacho chumba cha kujifungulia. Muda si mrefu sauti ya kichanga ilisikika kutoka kwenye kile chumba alichoingizwa Mama Helena. Helena alisimama akatazama angani na uso wake ukavaa tabasamu.

# Mtaa wa Hekaheka

Robert Mwijonge

Naomi aliingia kwenye mgahawa uliokuwa na wateja wengi. Alisimama kwa dakika kadhaa akipepesa macho huku na kule kakini hakumuona anayekuwa akimtafuta. Mhudumu aliyevaa sketi fupi ya kitenge na shati jeupe lenye nembo ya mgahawa kifuani mwake alimsogelea na kumkaribisha akae kwenye meza iliyokuwa haina mtu. Mezani kulikuwa na sahani nne pana na kila sahani ilikuwa imetengewa kisu pamoja na uma wa shaba wenye kung'aa.

Tumbo lake lilinguruma kama simba lakini mfukoni alikuwa hana kitu. Alitazama huku na kule, akaachia mwayo mrefu. Alibaki kimya kwa muda mfupi, kisha akamwambia mhudumu, "Nahitaji kumuona Bwana Kilonzo."

Mhudumu alimtazama Naomi juu mpaka chini kwa macho ya usaili na hatimaye akamjibu kwa swali; "Kwa nini unadhani Mkurugenzi atakuwa na muda ya kuonana nawe?"

"Ananifahamu," Naomi alisema huku akimtazama mhudumu machoni. Alimeza funda la mate akaendelea kusema, "Mwambie mtoto wa Mama Naomi anataka kukuona."

"Meneja!" Mhudumu aliita kwa sauti kubwa iliyowafanya wateja kugeuka upande ule. "Eti huyu msichana anataka kumwona Mkurugenzi!"

Kijana wa makamo aliyevalia suruali nyeusi na shati la kitenge kama kile cha sketi ya mhudumu, aliachia kitasa cha mlango na kugeuka kuwatazama. Kabla hajazungumza chochote mlango ulifunguliwa kwa ndani, akatoka mzee aliyejaa mvi kichwani. Alikuwa amevaa koti ambalo halikufungwa vifungo na kuacha shati jeupe la hariri lililofunika kitambi kikubwa kama mimba ya miezi tisa kuonekana.

Naomi alipiga hatua kumfuata yule mzee, macho yote ya wateja yakisafiri pamoja naye. Mzee Kilonzo alipunga mkono. Alipoushusha, kila mhudumu alirudi kwenye kazi yake. Alimpisha Naomi apite mlangoni kisha naye akafuata nyuma kuingia ofisini kwake. Taratibu, alielekea kwenye kiti chake cheusi akaketi na kujizungusha kulia na kushoto akiwa anamkagua Naomi kwa macho.

"Najua una matatizo gani," sauti ya chini iliyochanganya mngurumo na manung'uniko ilimtoka yule mzee. Akiwa bado anamtazama Naomi aliendelea kusema, "Mmeishiwa chakula nyumbani?" Naomi alitulia tuli kama sanamu pale

alipokuwa amesimama akisubiri kauli ya pili toka kwa mzee Kilonzo.

"Umekuja mwenyewe au mama yako amekutuma?" Mzee Kilonzo aliuliza swali jingine.

"Nimekuja mwenyewe." Naomi alijibu.

Mzee Kilonzo alitabasamu akainuka taratibu na kumsogelea Naomi, akaegemeza mikono yake mizito juu ya mabega yake. "Nitakusaidia chochote unachotaka kama utanisaidia ninachokitaka." Mzee Kilonzo alizungumza kwa sauti ya chini huku akimminyaminya Naomi mabegani.

Naomi alishusha macho yake yakatua kwenye viatu vyeusi vyenye mng'aro vya Mzee Kilonzo. Hakukosa kuiona pia suruali yake nyeusi, iliyoshikiliwa vema kiunoni kwa mkanda ambao kwa mbele ulikuwa umefichwa na kitambi kilichomwagika.

Kauli yake ingetosha kumaliza shida zake aweze kupata pesa ya kula, pango na mapambo ya mwili. Aliukumbuka uso wa mama yake ulivyokuwa umejaa simanzi walipoagana asubuhi. Akakumbuka usiku wa jana walivyolala bila kupitisha chochote tumboni, koo lilimkauka mate. Akamtazama yule mzee ambaye waziwazi alionesha tamaa ya kimwili usoni.

"Eeh! Mungu niepushe na hili pepo la huyu mzee," Naomi alijisemea kimoyomoyo huku akimtazama Mzee Kilonzo kwa majonzi.

"Hii iwe siri yetu," Kilonzo alinong'ona sikioni mwa Naomi.

Naomi alifumba macho, akazikumbuka siku zile Kilonzo alipokuwa anawaletea mapochopocho toka mgahawani, walivyokuwa hawapungukiwi pesa wala furaha. Pia akakumbuka siku ambayo alimshuhudia mama yake na mwanamke mwingine wakizipiga kavukavu mbele ya kadamnasi kila mmoja akimgombania Kilonzo.

Aliishika mikono ya mzee Kilonzo akainyanyua taratibu kutoka kwenye mabega yake na kuishusha chini. Naomi akaikunja mikono yake kifuani pake, akapiga hatua moja nyuma. Moyo ulifukuta kwa woga na uzito wa jambo lililomleta pale.

"Ninaomba kazi," hatimaye akasema.

"Hata hii pia ni kazi. Tena itakulipa zaidi." Mzee Kilonzo alisema, akiwa anaendelea kumkazia macho kwa uchu.

Naomi alitikisa kichwa, naye akamkazia macho Kilonzo. "Naomba kazi ya kupika, kupiga deki au kuhudumia wateja." Naomi alizungumza kwa sauti ya chini huku akiminyaminya vifundo vya vidole vyake vya mikononi, vikawa

vinatoka sauti ya kuvunjika.

"Kazi iliyopo ni ya kuhudumia moyo wangu." Mzee Kilonzo aliongea huku akimsogelea Naomi akitaka amkumbatie, lakini kabla hajamgusa, Naomi alipiga hatua moja nyuma tena, akakifikia kitasa na kukibinjua.

"Acha kuchezea bahati wewe utabaki na umasikini wako. Naomi, Naomi?" Mzee Kilonzo aliita lakini Naomi alikuwa amekwishaufungua mlango na kutokomea.

Naomi alitoka ofisini kwa Kilonzo akiwa amekunja sura. Macho ya wateja yalimpokea tena na kumsindikiza hadi alipovuka kizingiti cha lango la mbele na kutoka nje.

Naomi alitembea kwa kuvuta hatua, akakatisha mitaa miwili hadi akaingia mtaa wa Hekaheka. Tumbo lilinguruma na minyoo ilikuwa inamsokota bila huruma.

Hatua za Naomi zilitua kwenye banda la mama lishe aliyependwa sana na vibarua wa ujenzi, makondakta, wapiga debe, na wateja wengine wengi kutokana vyakula vyake kuwa bei poa aliyejulikana kama Mama Inno.

Alijibwaga kwenye kiti na kutupa mikono yake juu ya meza kwa dakika chache. Mama Inno alivuta kiti na kuketi kando yake akamwinua uso na macho yao yakagongana.

"Kulikoni Naomi?"

"Sijala toka jana." Naomi alijibu kwa sauti.

"Nilidhani ni makubwa zaidi kumbe hilo tu?" Mama Inno aliamka na kuingia kwenye chumba cha ndani. Baada ya dakika chache alirejea na sahani iliyojaa wali na maharage, akampatia Naomi atulize njaa.

Naomi alianza kukifakamia chakula. Baada ya vijiko viwili vitatu hivi akakumbuka kunawa. Kisha akatazama huku na kule akagundua kuwa chakula pekee walichokuwa wanakula wateja ni wali maharage. Alimgeukia Mama Inno akauliza kwa mshangao, "Mama Inno, naona unauza wali na maharage pekee. Kwa nini usiongeze viazi mbatata au mihogo ya kukaanga? Pia, unaweza kujaribu kuweka samaki au dagaa kwa kuanzia."

Mama Inno alimkodolea Naomi macho; na mshangao wake uliuzidi ule wa Naomi mara dufu! Aliiweka mikono yake kiunoni akauliza, "Yaani baada ya kushiba wali wa bure na maharage, ndio unajifanya mtaalamu wa biashara hii?"

Hilo *dongo* halikumkatisha tamaa Naomi. Aliendelea, "Na maharage haya ukiyatia nazi, naamini utavutia wateja wengi zaidi."

Mama Inno, akionekana kuchukizwa kidogo, alimjibu kwa sauti ya kebehi, "Ningejua ningekutoza pesa na njaa yako."

"Unaweza kuweka hata mishikaki inayopendwa na wateja wenye hela," Naomi alitiririka utadhani hakumsikia Mama Inno. Usoni alibeba tabasamu kidogo alipokuwa anavuta taswira ya jinsi banda la Mama Inno litakavyokuwa kama akitekeleza mapendekezo yake.

Mama Inno alizidi kukereka. "Wateja wangu ni hohehahe, unataka nifilisike?"

Naomi, alibainisha tatizo lingine. "Halafu viti, ungevipangilia kama kule kule kwa Kilonzo."

"Mbona hukwenda kuomba wali maharage kwa Kilonzo?" Mama Inno alifoka, akiwa amechoshwa na maoni ya Naomi ambayo hakuyaomba wala kuyahitaji. Alivua aproni yake na kumvisha Naomi. "Naona unajifanya mwerevu sana wa kazi hii, haya nakuachia uifanye angalau ulipie sahani yako ya wali maharage."

Mteja mmoja aliyekuwa akisikiliza mazungumzo hayo alisema kwa sauti ya chini, "Lakini yote aliyoyasema msichana huyu yana ukweli."

Mama Inno alimtazama yule aliyezungumza akatingisha kichwa. Maneno yake yalimkera, lakini alijizuia kujibu. Hakuwa na nia ya kupoteza mteja. Macho yake yalirudi kwa Naomi, ambaye sasa alikuwa anamalizia tonge lake la mwisho la wali. Kitu fulani ndani ya Mama Inno kilibadilika alipotazama macho ya Naomi, macho yaliyosheheni nia njema na shukrani.

Kitu kilimsukuma Mama Inno kumsogelea Naomi, na kumshika mkono kwa upole. Bila kusema neno, akaenda naye mkono kwa mkono hadi jikoni. Naomi alijikuta akisukumwa na mkondo wa ambako palijaa harufu ya viungo na rundo la vyombo vilivyopandiana.

Wakiwa jikoni kwa Mama Inno, ukurasa mpya ulifunguliwa. Naomi aliamua kazi kwa majaribio.

Naomi akiendelea na njozi zake za maboresho alisema, "Tunaweza kuboresha banda hili. Nakushauri uchukue mkopo maalum kwa ajili ya wanawake wajasiriamali. Utatuwezesha kununua viti bora na kufanya maboresho machache."

Mama Inno, akiwa amezoea maisha yake, alionekana kuwa na wasiwasi. "Naomi, hizi ni ndoto kubwa. Mkopo? Itakuwaje nikishindwa kulipa?"

"Mama, nimefanya mahesabu. Tukiongeza aina za vyakula, kuboresha viti na kuingiza huduma za kisasa kama malipo kwa njia ya simu, tutavutia wateja

zaidi. Hii itaongeza mapato yako."

Baada ya muda mfupi walifanikiwa kupata mkopo, mara banda la Mama Inno lilianza kubadilika. Naomi alianzisha vyakula vipya, kama mihogo ya kukaanga na samaki, na hata maharage yaliyopikwa na nazi. Wateja hasa wale waliokuwa wanatafuta chakula cha bei nafuu lakini chenye ladha na afya walivutiwa na *menu* mpya.

Maboresho ya viti na mazingira ya mgahawa yalikuwa ya kuvutia lakini ya gharama nafuu, yakiendana na uwezo wa Mama Inno. Naomi alisisitiza umuhimu wa usafi na mwonekano wa kuvutia, huku akiepuka gharama kubwa zisizo za lazima. Alianzisha mfumo wa kuagiza na kulipa kwa njia simu, na kupelekewa chakula hadi mteja alipo kwa gharama ndogo ya bodaboda. Naomi alitumia Instagram na Facebook kutuma picha za vyakula, ofa maalum, na kupata maoni ya wateja. Hii ilivutia wateja wapya, hasa vijana.

Mama Inno mara kadhaa alionyesha wasiwasi wake kuhusu mkopo. "Naomi, una uhakika hii itatulipa?" aliuliza kwa wasiwasi.

Kila mara Naomi alijibu, "Ndiyo, Mama. Tumeongeza wateja, na mapato yanaongezeka. Utalipa mkopo huu na kubaki na faida."

Mabadiliko hayo yalianza kuzaa matunda. Banda la Mama Inno lilianza kujaza wateja zaidi, na mapato yalizidi kuongezeka. Wakati mwingine watu walikosa mahali pa kukaa, wakala wakiwa wamesimama. Watu wakadai Mama Inno anatumia mizizi. Mama Inno alipata tumaini jipya, na wasiwasi wake kuhusu mkopo ukaanza kutoweka.

Mwaka mmoja baada ya maboresho makubwa katika mgahawa wa Mama Inno, habari zilizagaa mjini kuwa umaarufu wa mgahawa wa Kilonzo umeporomoka. Wateja waliokuwa waaminifu kwa Kilonzo sasa walikuwa wakimiminika kwa Mama Inno, wengine wakiagiza chakula kupitia mtandao.

Siku moja, meneja wa benki alifika kwa Mama Inno. "Baada ya kumaliza mkopo wako tunakushauri uchukue mkopo mkubwa zaidi," alisema kwa msisitizo.

Mama Inno alimgeukia Naomi. "Unasemaje, Naomi?"

Naomi alitafakari kwa makini ofa za benki, akachagua kutumia akiba yao. Upanuzi wa biashara ulihitaji kuongeza wafanyakazi. Ilikuwa ni jambo la kushangaza kuona wafanyakazi wa mgahawa wa Kilonzo wakija kuomba kazi kwa Naomi. Na hata meneja wao alifika siku moja asubuhi. "Utakuwa mfanyakazi wa kawaida, siyo meneja," Naomi alimwambia meneja huyo wa zamani wa Kilonzo.

"Sawa tu Dada, ninachohitaji ni kazi," alijibu kwa unyenyekevu.

Lakini tukio la kilele lilikuja pale Kilonzo mwenyewe alipofika. Alimuahidi Mama Inno kitita kikubwa cha fedha ili anunue mgahawa wake. Mama Inno, kwa dakika kadhaa alionekana kuingia tamaa lakini Naomi alipinga vikali.

"Mama Inno, miaka michache ijayo tukitaka tutakuwa na uwezo wa kununua mgahawa wa Kilonzo, viti vyake, wafanyakazi wake . . ." alisema Naomi kwa ujasiri.

Mama Inno, akitabasamu kwa udadisi, alidakia, "Na hata Kilonzo mwenyewe . . ."

Kilonzo, alijiondokea, uso kauinamisha chini kwa aibu.

## Sintasahau

Ni vigumu kusahau, yaliyonitokea,
Juu ya unyama huu, kovu walilonitia,
Vijana wenye makuu, tena waliokomaa,
Ubaya walinitenda, bila hata huruma,

Ilikuwa Ijumaa, asubuhi na mapema,
Shuleni naelekea, mara ghafla kasimama,
Nyuma nikaangalia, thibitisha usalama,
Mara wakanivamia, vijana wenye miraba.

Kwa nguvu kunikamata, jumba bovu kuniweka,
Kelele wakanikata, kwa manguo nipachika,
Na chini wakanitupa, wakaanza kunibaka,
Sana nilitapatapa, bali sikuchoropoka.

Nilishindwa kutembea, nikawa nachechemea,
Watu wakanishangaa, vidole kuninyoshea,
Chini niliinamia, majonzi yakanivaa,
Uchungu ukanijaa, watu kuninyanyapaa

Niliwaza akilini, wapi pa kuelekea,
Ndipo nilipobaini, polisi patanifaa,
Nilisema kwa yakini, hata wao watalia,
Hatua watachukua, wahalifu fatilia,

Nilienda zahanati, kupima kama ni kwema,
Majibu kama mtiti, nikashindwa kupumua,
UKIMWI ni kizingiti, kilinirudisha nyuma,
Mwisho nikajikubali, Msongo kuuepuka

Kupita miaka miwili, hukumu ilitolewa,
Miaka kumi mbili, jela walihukumiwa,
Na faini laki mbili, kizimbani ililipwa,
Nilishindwa kufurahi, machungu kunipungua.

# Najuta

Suzana Mremi

Chumbani kulikuwa na giza totoro. Milio ya jumbe za simu ililia mfululizo mithili ya matone ya mvua majira ya masika. Johari alikuwa amejilaza kwenye kitanda chake akiwa amejipinda kama ua lililoelemewa na uzito wa umande. Alikuwa amezama katika mazungumzo ya WhatsApp na Joshua, kijana ambaye walikutana Facebook hivi karibuni na kupeana namba za simu. Mwanga wa simu yake ndio pekee uliokinzana na kiza kilichotawala mle chumbani. Mwanga huo hafifu, uliangazia kwenye uso maridadi rangi ya machweo, macho maangavu na kope ndefu zilizopinda kama mbawa za kipepeo.

Akiwa amezama kwenye mazungumzo, Johari hakusikia nyayo za mama yake, aliyetembea kwa kunyata kama mwizi stadi nyakati za usiku. Mama yake alifungua mlango kwa umakini wa askari mwenye azma ya kumtia mhalifu mbaroni. Ghafla, Johari alibaini uwepo wa mama yake chumbani, akakurupuka na kuifutika simu yake chini ya mto; akavuta shuka na kujifunika gubigubi.

"We Johari, wewe!" mama yake aliita, "Yaani toka upate hiyo simu hulali, huna kazi nyingine zaidi ya kuperuzi tu. Unaperuzi mpaka saa nane hii!?"

Johari alijikausha kimya kabisa. Mama yake aliwasha taa, akaendelea kusema, "Hili kabati nilikwambia ulifute ndani, hujalifuta. Chumbani umejaza nguo kila kona, hukunji wala hupangi, unang'ang'ana tu na simu. Hivi una mpango gani na maisha yako wewe?" Wakati anayasema hayo, Mama Johari alikuwa anatoka kuelekea chumbani kwake. Johari aliposikia mlango umefungwa, alinyanyuka upesi akachukua simu yake. Alijifunika gubigubi ili mwanga wa simu usipenye. Mara akampigia simu Joshua na kuongea naye kwa kunong'ona, "Usiku mwema *my sweet love. My mummy* anazingua nitakucheki kesho."

Joshua alimjibu, "Sawa mpenzi ulale salama. Nakupenda sana waridi la moyo wangu."

Johari aliendelea kumuwaza Joshua mpaka pale alipopitiwa na usingizi. Alilala hadi alipoamshwa na mlio wa simu majira ya saa nne asubuhi. Ilikuwa ni namba ya ofisini kwa mama yake. "Vipi bado umelala?" mama yake aligomba. "Haya ndio matokeo ya kukesha mitandaoni mpaka usiku wa manane."

Johari aliamka akakuta furushi la jumbe limejaa kwenye simu yake, kila mmoja ukidai kusomwa. Alijizoazoa kutoka kitandani, macho yake yakiwa hayatoki kwenye kioo cha simu, akisoma ujumbe baada ya ujumbe, kila mmoja

ukiibua hisia tofauti. Hata alipoelekea sebuleni kupata kifungua kinywa, simu yake ilibaki kuwa mwenza wa karibu, akifungua na kufunga ujumbe mmoja baada ya mwingine na kwa kufanya hivyo akawa anafungua na kufunga milango yake ya fikra. Ghafla, mwito wa simu ulisikika. Alipopokea, kwenye kioo cha simu yake alionekana mwanaume mtanashati mwenye sharubu na ndevu zilizonyolewa maridadi na kurutubishwa kwa mafuta ya gharama. Uso ule wa kuvutia alikuwa amepiga tabasamu. Johari alipomuona Joshua, moyo wake ulicheza rumba. Alijisemea kimoyomoyo, "Mungu hakuumba wasichana tu! Hata wanaume pia wameumbika, Mashallah!" aliongea na Joshua huku akitabasamu kwa furaha na deko.

Vumi, mdogo wake, alipoingia sebuleni kuangalia televisheni, alimkuta Johari bado ameganda kwenye simu yake. Alipogundua Vumi anamkodolea macho, Johari alijibaraguza, akaficha uso wa simu yake, akitaka mdogo wake asijue kinachoendelea. "Endelea tu na mambo yako mdogo wangu, mimi naangaliaangalia picha tu huku mtandaoni," alimwambia Vumi kwa kujihami, kisha akainuka na kurudi chumbani mwake.

Johari na Joshua waliendeleza mazungumzo yao wakafanya mpango wa kukutana. Walikubaliana kuwa Joshua amtumie Johari tiketi ya ndege asafiri hadi Mwanza. Haikuchukua muda, Johari akapokea tiketi ya ndege kwenye simu yake, ikimtaka awe uwanja wa ndege saa sita mchana wa siku iliyofuata. Alirukaruka kwa furaha huku akibusu simu yake, mwaa! mwaa!

Huku akiwa na msisimko wa *kukwea pipa* kwa mara ya kwanza, Johari alianza maandalizi ya safari kwa kuchagua na kupanga vitu atakavyovihitaji kwa safari.

Kesho yake, teksi aliyoagiziwa na Joshua ilifika nyumbani kwao kumchukua. Johari alichukua begi lake dogo akamuaga mdogo wake, "Vumi, naenda kwa akina Lareen mara moja, mama akija mwambie sitakawia sana kurudi."

Akiwa na shauku kubwa ya kukutana na Joshua, alipanda kwenye teksi, na kuianza safari. Vumi akimsindikiza kwa macho hadi gari aliyoipanda ilipotokomea.

Johari, alipokaribia kufika uwanja wa ndege alitaka ampigia Joshua simu kumfahamisha kuwa ameshaanza safari. Mapigo ya moyo wake yalisimama kwa sekunde kadhaa alipogundua kuwa hakubeba simu yake. Alimgeukia dereva akamsihi warudi nyumbani hima akaichukue, lakini dereva alitingisha kichwa na macho yake yalionyesha ukweli mchungu, "Hata ukitumia bodaboda, huwezi kurudi nyumbani uje na kuiwahi ndege yako."

Johari alichanganyikiwa. Alianza kuona ndoto yake ya kuanza maisha mapya na Joshua ikiyeyuka. Walikuwa wameshafika uwanja wa ndege. Kwa

wasiwasi mkubwa aliagana na dereva wa teksi, akamfuata mhudumu mmoja wa uwanja huo na kumweleza shida yake.

"Unaweza kusafiri hata bila simu yako," alimhakikishia.

"Lakini tiketi yangu ipo kwenye simu ..."

Mfanyakazi huyo alitabasamu, "Tiketi yako ipo kwenye mfumo. Twende ndani kwenye kaunta ya wasafiri nitakuelekeza." Walipofika ndani alimuomba jina na kitambulisho.

Johari alipata ahueni kubwa; na haraka akatii. Punde si punde utambulisho wake ukamfungulia mlango wa safari aliyodhani imeota mbawa. Alipokaa kwenye kiti chake ndani ya ndege hatimaye, moyo wake ulidunda kwa msisimko wa msafiri wa anga kwa mara ya kwanza. Akiangalia nje kupitia dirishani, mawazo yake yakampelekea kutafakari atokako na aendako pamoja na maamuzi aliyofanya ya kuondoka nyumbani bila kuaga. Alipata wasiwasi pia akiwazia makutano yake na Joshua bila mawasiliano ya simu.

Ndege ilipotua Mwanza na abiria kutoka nje, hofu yake ilitoweka mara alipomtambua Joshua katikati ya umati wa watu waliokuwa wanawasubiri wageni. Moyo wake uliruka, akamkimbilia, wakakumbatiana kwa furaha.

Joshua alikuwa amevalia shati la drafti na suruali ya 'jinzi' iliyombana kiasi cha kuonesha umbo lake lililomvutia sana Johari. Kwa muda alisahau kabisa wasiwasi aliokuwa nao baada ya kutoroka nyumbani na kujikuta hana mawasiliano na mwenyeji wake.

Joshua alikuwa amechagua wakae kwenye chumba chenye utulivu kwenye hoteli ndogo yenye mandhari nzuri. Kwa muda wa wiki mbili walizokaa pamoja, Johari alijikuta akiishi katika ndoto, kila siku ikileta uzoefu mpya wa kusisimua. Alitumia muda mwingi kuuchunguza mji, kula vinono na kunywa vitamu, akasahau kabisa yote yaliyoyaacha nyumbani. Kadri siku zilivyopita, alizidi kuzama katika mapenzi na Joshua.

Wiki ya tatu, Joshua alimwambia Johari kuwa alikuwa amemtafutia kazi. Walielekea kwenye jengo moja la kifahari lililojitenga. Walipofika mbele ya jengo hilo, Joshua alisimama akamwambia kwa tabasamu, "Hapa patakuwa ndio ofisini kwako."

Johari alirukaruka kwa furaha. 'Sasa nitaweza kuwasiliana na wazazi wangu kuwafahamisha kuwa niliondoka nyumbani kwenda kutafuta ajira," aliwaza.

Walipoingia ndani, walipokelewa na mama mmoja mnene mwenye sura ya kujiamini. Alionekana kana kwamba alikuwa anategemea ujio wao. Aliwaangalia kwa makini, akamkagua Johari kuanzia juu hadi chini, kisha akamwambia,

“Nifuate.” Aliongoza njia bila kugeuka nyuma.

Johari alifuata kwa moyo uliojaa mchanganyiko wa matarajio na wasiwasi, akijiuliza aina gani ya kazi angepewa katika mazingira yale ambayo hayakukaa kiofisiofisi. Walipanda ngazi kuelekea ghorofani, wakaingia kwenye chumba kilichoonekana kama chumba cha hoteli, akaambiwa asubiri. Wasiwasi wa Johari sasa ulipiku matarajio. Baada ya dakika tano hivi alitoka nje akaenda kwenye chumba alichoingia mwanzo akitaka apate maelezo mazuri kutoka kwa Joshua, lakini badala yake akakutana tena na yule mama peke yake.

“Mpenzi wangu yupo wapi?” Johari aliuliza kwa sauti iliyojaa taharuki.

“Amerudi kwa mke na watoto wake,” mama yule alijibu kwa sauti isiyo na hisia. “Na wewe rudi chumbani kwako, muda wa kuanza kazi umekaribia.”

Maneno hayo yalimtia Johari yabisi moyoni. Ghafla aliipata picha. “Nimedanganywa!” matukio yaliyomfikisha alipo yalipita akilini mwake kama sinema ya kutisha. Alifungua mlango akatoka nje akitaka kutoroka lakini nje alikabiliana na lango la chuma na mlinzi getini. Johari alipiga yowe lakini hakuna aliyemsikiliza. Yule mama alimtazama akasema kwa kejeli, “Wote huanza hivyo. Utazoea tu. Halafu ukizoea hutatamani kuondoka.”

Johari aliporejea kwenye chumba chake alifungua pazia akagundua mahali penye upenyo katikati ya nondo za dirisha. Tatizo likawa kwamba chumba kilikuwa ghorofani. “Potelea mbali,” alijisemea na bila kufikiria sana, alipenya kwenye nondo, akashikilia nguzo na kutanguliza miguu chini. Alipofika chini, alihisi amevunjika mguu, kutokana na maumivu makali aliyokuwa nayo kwenye kifundo cha mguu. Alijiburuta, akaparamia ukuta wa nyuma wa uzio kurukia upande wa pili, bila kujali vipande vya chupa vilivyowekwa juu ya ukuta ule vilivyokatakata viganja vya mikono yake.

Kwa mbali aliona magari yakipita kwenye barabara iliyokuwa na taa za barabarani, na nyuma ukuta wa kasri ambayo kwa muda mfupi aliokuwamo humo, haikuwa tofauti na jehanam. Alijikongoja hadi barabarani akiwa na majuto tele moyoni. Nia yake sasa ilikuwa ni moja tu, kurudi nyumbani na kuyarekebisha mapito yake.

# Harakati

Kulwa Abdallah

Ilikuwa asubuhi na Jessica alikuwa anaelekea kisimani kuchota maji. Njiani alikutana na rafiki yake, Viviani ambaye pia alikuwa anaelekea kisimani, wakaongozana. Walipofika walikuta watu wengi wakisubiri kuchota maji, ikawabidi wasubiri zamu yao. Watu hao walikuwa wanapiga gumzo.

"Hivi jamani tumejipanga vipi kuhusu hili suala la kuyahama makazi yetu?" aliuliza mama mmoja.

"Hata sielewi, wapo wanaogoma kuondoka na wengine wanaogopa kugoma." mama mwingine alidakia.

"Mimi naona ni bora kuondoka kwa sababu serikali ikija hapa na zoazoa lao hakuna kitakachosalia. Bora tuondoke mapema kuepusha uharibifu wa mali zetu." mama mwingine alisema.

Jessica aliyekuwa anawasikiliza kwa makini aliamua kuchangia kwenye mazungumzo yale, "Hapana mama zangu, hatupaswi kuwa na uoga katika kusimamia haki zetu. Msiangalie tu uharibifu wa mali bali pia tujiulize ni wapi tutaishi baada ya kuondoka hapa?"

"Je, tutafanya nini kujihakikishia hilo unalosema?" aliuliza mama aliyeongea mwisho.

"Sikiliza mama yangu, ni rahisi sana kama tutakuwa na ushirikiano. Tunaweza kuandamana hadi kwa Mwenyekiti atuambie nini hatima yetu baada ya kutuondosha hapa."

"Itawezekana kweli mwanangu?"

Mazungumzo yaliendelea hadi Jessica na Viviani walipojaza ndoo zao na kuondoka.

Jioni ile baada ya chakula, Jessica alijitupa kitandani kwake akitafakari mazungumzo ya mchana ule. Aligutushwa na sauti ya shangazi yake akimuuliza; "Mwenzetu vipi, mbona upo mbali sana?"

"Shangazi," alijibu. "Hivi tukiondolewa hapa tutaishi wapi?"

"Serikali itaamua," alijibu shangazi yake kwa sauti ya kukata tamaa. "Kwani wewe unahisi tunaweza kufanya nini ili kuzuia tusihamishwe?"

"Bado natafakari, ndio maana nimekuuliza."

"We mtoto mimi nakujua. Ukishaanza hivyo sijui utakapoishia. Wacha kabisa! Usijitafutie matatizo." shangazi alionya huku akielekea chumbani kwake kulala.

***

Kijiji cha Makamba kimekuwa katika mgogoro wa ardhi kwa zaidi ya miaka kumi sasa. Serikali imewataka wanakijiji waondoke eneo hilo ili kumpisha mwekezaji. Miaka yote ya nyuma wanakijiji waligoma kuondoka lakini mwaka huu, serikali imetoa kauli yake ya mwisho. Ama waondoke kwa hiari, au waondolewe kwa nguvu.

Siku iliyofuata Jessica aliamka asubuhi sana akaondoka nyumbani bila kuaga. Alimpitia Viviani akamuomba amsindikize mahali, wakaongozana hadi nyumbani kwa rafiki yao Bazil, waliyekuwa wanasoma naye. Walipokutana naye, Jessica alianza kuongea.

"Kwa nini sisi tusiwe mstari wa mbele kuhakikisha sauti na maslahi ya watu yanazingatiwa kijijini kwetu?"

"Kivipi?" rafiki zake walimuuliza kwa pamoja.

"Tuandamane," Jessica alipendekeza kwa shauku ya mapinduzi.

Viviani alipandisha mabega, "Kuandamana? Unaijua serikali kweli wewe? Nina miaka kumi na tisa tu, sijajiandaa kuwa *shahidi* bado."

Jessica akamgeukia Bazil. "Na wewe Bazil, unasemaje?"

"Sipo mbali nawe, Jessica, ila naona tutafakari zaidi kabla ya kukabiliana na nguvu za dola."

"Nimekueleweni, lakini mnafikiri tufanyeje sasa?" Jessica aliuliza kwa tafakuri.

Baada ya mashauriano marefu, waliamua kuhamasisha wanakijiji kufanya mazungumzo ya kina na viongozi wa serikali za mtaa na mwakilishi wa mwekezaji ili wajaribu kupata muafaka wenye manufaa kwa pande zote.

Walitembea nyumba kwa nyumba, wakisikiliza hoja za kila mwanakijiji, wanawake kwa wanaume, vijana kwa wazee. Hatimaye vijana thelathini na wawili walijiunga nao. Wajigawa katika makundi, wengine wasikilize hoja za wawekezaji na kuzichambua, wengine za wananchi kwa makundi ya jinsia, rika na shughuli, na wengine waongee na viongozi wa serikali, mila na imani. Jioni ilipofika, kikundi cha vijana thelathini na wawili, wakiwemo Jessica, Bazil na Viviani, walikusanyika

kwa mazungumzo ya kina. Walijadili matokeo ya utafiti na ushawishi waliofanya ambapo walibaini kuwa, wako wanakijiji walio tayari kumwaga damu kutetea ardhi yao. Wakapanga mikakati ya kuyaunganisha makundi hasimu ili kuzuia janga hili lisiikumbe jamii yao. Waliita kundi lao 'Nguvu ya Vijana' na kauli mbiu yao ilikuwa "Vijana Tunajenga Daraja."

Wiki mbili kabla ya tarehe ya mwisho ya kuondoka kwa hiari na wakati vuguvugu la mageuzi likiwa linachemka, Mwenyekiti msaliti aliwatelekeza wanakijiji. Jessica ambaye alikuwa amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa kundi la Nguvu ya Vijana aliitisha mkutano wa hadhara uliohudhuriwa na wanakijiji wa rika zote. Aliwakaribisha wawakilishi wa kamati za utafiti na uchambuzi kuanika matokeo ya uchambuzi wao. Mmojammoja waliwasilisha taarifa zao, zote zikiashiria kuwa chanzo cha tatizo ni kuvunjika kwa mawasiliano baina ya wanakijiji na mwekezaji kutokana na upotoshaji uliofanywa na Mwenyekiti wa Kijiji.

Wanakijiji walipata ari mpya, lakini hawakujua waanzie wapi. Ili kuondoa mzizi wa fitina, waliamua kutuma ujumbe wilayani kuripoti kutoweka kwa Mwenyekiti wao ambaye pia walikuwa hawana imani naye. Msafara huo uliomba pia kufungua milango ya mawasiliano kati yao na mwekezaji yatakaoshuhudiwa na viongozi wa kata na wa wilaya.

Siku moja kabla ya kikao na mwekezaji, hali ya wasiwasi ilitanda kijijini Makamba. Mwenyekiti na kundi la wanamgambo walikuja na kuvuruga hali ya hewa. Waliharibu mali za watu na makazi wakidai siku walizopewa wanakijiji kuhama kwa hiari zilikuwa zimekwisha. Wanakijiji waliokuwa na hasira na taharuki walijibu mapigo, kukatokea vurumai, uharibifu na majeruhi kadhaa. Jessica na wenzake walitoa ripoti polisi kwa njia ya mtandao na wakati huohuo wakijaribu kuwatuliza wanakijiji wasijishirikishe katika uvunjifu wa amani. Hali ilikuja kuwa shwari Mwenyekiti na kundi lake walipotiwa mbaroni kwa tuhuma za uharibifu wa mali, kujeruhi na kuhatarisha maisha.

Hatimaye siku ya mkutano na mwekezaji ilipowadia, wananchi walihudhuria kama ilivyokuwa jana yake, kila mtu akiwa amejihami na silaha za jadi huku wakiimba,

"Tumechoka kuonewa! Tunataka haki zetu!"

Viongozi wa serikali walipowasili waliwatoa hofu wananchi na kuwataka waweke silaha chini ili mazungumzo yafanyike kwa amani. Walikuwa wameshapata taarifa ya matukio ya jana yake. Viongozi wa Nguvu ya Vijana ambao walikwishajenga hoja kwa viongozi hao, walipita huku na huko miongoni mwa wanakijiji wakiwasihi wajenge daraja la maelewano kwa kujikita kwenye madai yao na si vinginevyo.

# Shamba la Dhahabu

Aidan Mtura

Nchi ya Mbugani ilikuwa ni nchi yenye giza nene kwa mtoto Swala siku hiyo. Alikuwa na majonzi na huzuni kubwa. Aliketi kati ya makaburi ya wazazi wake, waliofariki dunia na kuzikwa mapema siku hiyohiyo. Uchungu ulimkaba kama jiwe kooni, na machozi yalimlengalenga. Alijitupa katikati ya matuta mawili yaliyofunika miili ya wazazi wake. Alisambaza vizuri udongo juu ya yale makaburi huku akiomba kwa namna yake wazazi wake wasafiri salama kurudi kwa Muumba.

Hakujua kama angerejea tena kuyaona makaburi yale, maana tayari mkuu wa ukoo wa nyika Mzee Tembo, alishatoa amri ya kumtoa roho kama asubuhi ingemkuta kwenye kiwanja chake cha urithi. Aliweka vibuyu viwili kwenye makaburi ya wazazi wake akaiomba mizimu yao imuongoze huko aendako.

Ile amri ya kutotakiwa pale kijijini alihalalisha kifo chake endapo angeikaidi. Mali zote ikiwemo ardhi pamoja na kibanda cha wazazi wake, hazikuwa mali zake tena, zilikwishataifishwa na mkuu wao kwa kosa ambalo wazazi wake walilifanya na kuwasababishia hukumu ya kifo mbele ya kadamnasi. Hakuwa na muda wa kupoteza, ilimpasa asalimishe uhai wake. Akachukua mihogo miwili na kibuyu cha maji na kuanza safari.

Njiani, mtoto Swala alitembea kwa hofu kubwa. Sauti mbalimbali za wanyama wakali hasahasa mbwa mwitu, zilimuogopesha. Alikiona kifo kikimnyemelea. Alijua muda si muda atakuwa kitoweo. Kila alipopiga hatua mbili tatu alisimama na kuangaza macho yake pande zote. Baada ya kutembea kwa masafa marefu, mtoto Swala aliona ni kheri apumzike kichakani, mahali ambapo wanyama wakali wasingeweza kumuona kirahisi.

Pale kichakani mawazo yakamkumba. Haikumuingia akilini kabisa kuwa kosa lile la wazazi wake lilistahili hukumu ya kifo. Alikumbuka siku ile ambapo yeye, baba na mama yake, walipokurupushana na mlinzi wa nyika ile bwana simba aliyekuwa na njaa kali. Katika kumchenga simba yule, baba yake ambaye ndiye alikuwa ageuzwe kitoweo alipiga chenga kali, simba akapiga mwereka na kujikita tumboni kwenye kisiki kilichochongoka sana. Ilikuwa bahati kwa upande wao siku ile kunusurika kuliwa. Tukio lile aliliona mtoto tembo ambaye alikuwa anakunywa maji karibu na hapo, ndipo alipokwenda kuhadithia mkasa ule kwa mkuu wa nyika, Mzee Tembo. Taarifa zilisambaa asubuhi yake kwamba, Mzee Swala na familia yake imechangiana kumuua mlinzi wa nyika kikatili na kutokomea.

Ndipo msako dhidi yao ulipoanza. Baada ya masaa kadhaa Baba na Mama Swala walipatikana lakini mtoto Swala hakuwepo. Walijitahidi kujitetea lakini wananyika hawakuridhika na utetezi wao. Iliamuliwa wauawe mbele ya umati.

Utekelezaji wa hukumu ilikuwa ni tendo la dakika chache sana. Tembo mmoja aliyejaza, aliinua mkonga wake na kuwatandika kwa pamoja. Kila mmoja akiangukia mbali kama gunia la mawe. Mara kifo kikawatenganisha na mtoto wao mpendwa.

Baada ya mtoto Swala kupata taarifa kuwa wazazi wake wameuliwa na wamezikwa siku ile ile, aliamua kuyazuru makaburi yao kuwapa buriani huku akichukua tahadhari ya kutokuonekana tena kwenye jamii ile.

Alitembea kwa siku tatu bila mwelekeo. Alinyeshewa na mvua za masika zilizoambatana na upepo na baridi kali iliyopenya hadi kwenye mifupa. Usiku roho yake ilikuwa juujuu, asiweze kupata hata lepe la usingizi. Akili yake ilivuta taswira ya kifo cha wazazi wake. Nguvu zilipomuishia kutokana na uchovu, kiu na njaa, aliamua kujificha kwenye kichaka chenye miiba ili apate japo usingizi kidogo kabla hajaendelea na safari yake. Lakini siku hiyo, alipata ndoto isiyo ya kawaida.

Mama yake alimtokea ndotoni na kumpa ujumbe mzito.

“Hapana!” Niacheni tafadhali, niacheni nikamuone mama’ngu.”

Alisikia sauti iliyoishia na mwangwi. Aliona mwanga mkali mbele yake. Alipogeuka alimuona mama yake akiwa ameketi kwenye gogo. Pembeni kulikuwa na kibuyu na mkuki; na alikuwa akibubujika damu mdomoni na machoni.

“Amka mwanangu amka upesi. Chukua kibuyu hiki, ukakifungulie shambani, kisha utavuna dhahabu mwanangu. Tafadhali usiache mkuki huu. Utakulinda. Mwanangu, kamwe mkuki huu usitumike kutoa uhai.” sauti iliishia na kutokomea mitini.

Mtoto Swala alizinduka toka usingizini kwa mshtuko, huku mapigo ya moyo yakimuenda mbio. Pembeni yake alikiona kibuyu pamoja na mkuki. Hakika ilikuwa si ndoto bali kweli.

“Ina maana mama kanitokea kweli jamani?” aliwaza huku akiinuka na kuchukua kile kibuyu na mkuki.

Safari siku hiyo ilikuwa na baraka tele. Alitembea kwa muda kidogo kisha kwa mbali akaona vibanda. Alifurahi akijua kuwa ameachana na msitu. Alipofika kijijini hapo, familia moja ilimkaribisha kwa ukarimu. Baada ya kusimulia maswaibu yake, walimpa kibanda kidogo cha kuishi pamoja na shamba ili aanze maisha mapya. Mtoto Swala alifurahi sana, akilini akijua fika kuwa mzimu wa mama yake ulikuwa unamuongoza mahali salama.

“Hatimaye mizimu ya wazazi wangu imenisaidia.” alijisemea peke yake akiwa kibandani kwake huku akikitazama kile kibuyu. Akakumbuka ya kuwa, hakuwahi kabisa kukifungua kile kibuyu tangu akabidhiwe kule kichakani. Akakifungua, akakutana na mbegu za mpunga.

Msimu wa kilimo ulipoanza, Mtoto Swala alisaidiana na wenyeji wake kupanda mbegu shambani kwake. Walikuwa hawajapata kuiona kabisa mbegu ya aina ile kabla ya hapo. Mpunga ulikuwa zao jipya kwao. Alijitahidi kuwaelewesha namna mbegu ile inavyokua mpaka kuvunwa na kutengenezwa kuwa chakula. Wenyeji wake wakaingiwa na shauku ya kutaka kuonja chakula hicho kipya.

Baada ya miezi kadhaa, mpunga uliokuwa umefikia hatua ya kuvunwa ulinawiri shambani na kumeremeta juani kama dhahabu. Mtoto Swala alisaidiana na wenyeji wake kuvuna mpunga na kuweka ghalani. Siku moja aliandaa chakula cha wali na mbaazi za nazi na kuwakaribisha wenyeji wake pamoja na majirani.

“Mmh jamani ndiyo kitamu hivi kumbe?” jirani mmojawapo aliuliza huku akiwa na tabasamu usoni.

Wenyeji wake na wanajamii waliowazunguka walianza kumiminika kuja kubadilishana mpunga na vitu mbalimbali. Ghafla Mtoto Swala akawa maarufu. Shamba la mpunga lilimpa heshima na thamani miongoni mwa wanajamii; wenyewe wakiliita shamba la dhahabu.

# Kichaka

Nakichukia kichaka,
Cha majani marefu,
Na majani mafupi,
Ndoo iloporomoka,
Nguo nazo kuchanika,
Kama panya wamepita.

Mtama niliukatwa,
Ndipo chini nikawekwa,
Heshima nikaishushwa,
Kwa mambo yaliyofanywa,
Kilio kilisikiwa,
Bali hakukuitikiwa.

Nyumbani nilipofika,
Mjinga nikaambiwa,
Shada la kujitakia,
Nalo nikalivalishwa,
Hakika ‘medhalilika,
Roho sina pakuweka.

Eti hiyo ni dunia,
Majanga ni kawaida,
Mama wewe vumilia,
*Vidume* unawajua?
Maneno ya kunipoza,
Wakubwa waliusia.

# Tabu Tabuni

Otilia Angelus Haule

Siku ile ilikuwa ni siku yenye changamoto kubwa zaidi kwa Tabu, aliyekuwa na historia ya kuchelewa shuleni kila siku. Mara nyingi alifanikiwa kuepuka adhabu lakini siku ile alinasa kwenye mtego wa Mwalimu Nali.

Mwalimu Nali, alijulikana kama 'Mbogo wa Shule ya Sekondari Tujijenge'. Alikuwa na sifa ya kutoa adhabu kali kwa wanafunzi wanaochelewa darasani. Aliweka amri zake kumi na kuzitangaza kuwa ni sheria zisizovunjika. Alisema, "Atakayevunja sheria hizi, ataliona bonde la mto wa kuzimu."

Wanafunzi wote walizishika amri zile kama hesabu za kichwa; na kila alipoingia darasani aliwataka wazitaje sheria hizo kabla ya kuanza kufundisha. Hakuna mwanafunzi aliyethubutu kusahau sheria hizo kwa sababu adhabu ya Mwalimu Nali mtu anapozivunja ilikuwa ya kiwango cha lami.

Alipofika shuleni wenzake walikuwa tayari wako madarasani. Tabu aligundua kuwa hana budi ila kujiandaa kukabiliana na Mbogo yule. Akiwa kwenye geti la shule, aliwaza jinsi ya kupata msamaha kutoka kwa Mwalimu Nali. Aliwaza jinsi adhabu zake zilivyokuwa kali na hakuwa tayari kupambana nazo. Hatimaye alijongea na kujibanza nje ya mlango wa darasa lake akavuta pumzi ndefu.

Mwalimu Nali alipomuona Tabu amesimama nje ya darasa, uso wake ulionyesha ghadhabu. "Tabu, njoo hapa!" aliita kwa kukaripia.

Tabu aliingia darasani kwa tahadhari. Wanafunzi wote walimtazama kwa macho yenye mchanganyiko wa huruma na mshangao. Tabu alipofika mbele ya darasa, alijihisi kana kwamba amesimama kwenye kilele cha mlima mrefu. Mwalimu Nali alimtazama kwa macho makali na kumwambia; "Tabu nitajie sheria zangu kumi kabla sijakuadhibu." Jinsi Tabu alivyokuwa anazitamka, ndivyo Mwalimu Nali alivyoonekana kupandisha hasira." Tabu, umekuwa ukichelewa kila siku! Leo ni siku yako ya mwisho ya kuona jua kwenye kipindi changu!" alisema kwa ghadhabu.

Tabu alijitahidi kujieleza, "Mwalimu, naomba msamaha. Sitachelewa tena." jasho jembamba lilimtiririka kwapani, mgongoni na kwenye viganja vya mikono yake. Aliifuta mikono yake midogo kwenye sketi aliyovaa.

"Hii shule ni ya baba yako?" mwalimu alifoka huku akimtazama Tabu.

“Sitaki tena kusikia kelele zako.” aliendelea kufoka na kumsogelea. “Unaenda wapi?” aliuliza huku akimfuata Tabu aliyekuwa akirudi kinyumenyume, uso wake ukiwa ameukunja kama amekula ndimu. “Toka nje, hukunisikia?” mwalimu aliongea na kumvuta Tabu shavu, kulekea nje. Tabu alikunja uso kwa maumivu, huku mkono wake wa kulia ukijaribu kusukuma mkono wa mwalimu wake utoke shavuni kwake. Walipofika mlangoni mwalimu alimsukuma Tabu nje akarudishia mlango na kusema; “Piga magoti hapo nje mpaka nitakapotoka.”

Tabu alipiga magoti kwa saa moja akimsubiri mwalimu wake amuamulie hatma yake. Mlango ulipofunguliwa, Mwalimu Nali alitoka nje. Machozi yalimtiririka Tabu alipomtia tena machoni.

“*Stupid!* Tena unyamaze. Kweli aliyekupa hilo jina hakukosea.” mwalimu alisema huku akimpigapiga Tabu kichwani. Tabu alinyanyua macho yake na kumtazama mwalimu wake usoni. Macho ya mwalimu yalikuwa yameiva na kuwa mekundu kama nyanya. Matundu ya pua yaliyofunuka yalimfanya Tabu aogope zaidi. Hata hivyo alijikaza na kusema;

“Mwalimu naomba unisamehe! Nisamehe, nisamehe, nisamehe! Nitajita...”

Mwalimu alimkatisha, akatoa kitambaa kidogo kutoka kwenye mfuko wa suruali yake na kujifuta jasho. Kisha akamuinamia Tabu, akamshika bega, akausogeza mdomo wake karibu na sikio. “Hivi ninavyoongea hapa nyanyuka ukajaze kokoto kwenye chumba kile cha darasa.” aliyoosha mkono kuonyesha jengo lililokuwepo pembeni kabisa na pale walipokuwepo. Wanafunzi walichungulia madirishani na wengine walitoka nje kushuhudia kinachoendelea. Wapo waliokuwa wakicheka na wengine walihuzunika. Tabu hakuyajali yote hayo. Alinyanyuka na kufuata maagizo.

Baada ya dakika mbili Tabu alitoka na ndoo mbili na jembe. Safari ya kuelekea machimboni ilianza. Hapakuwa mbali na shule yao ila ugumu ulikuwa kwenye kupandisha kilima. Mashimo na mawe makubwa ndiyo yaliyoonekana hapo. Kulikuwa na watu, wake kwa waume wakichakarika kuponda mawe. Magari makubwa kwa madogo yalionekana yakitoka na kuingia kwa ajili ya kubeba kokoto. Tabu aliangaza macho huku na huko akitafuta sehemu yenye mabaki ya kokoto na mawe madogo madogo. Haikuchukua muda Tabu alipata sehemu nzuri yenye kokoto kubwa na ndogo.

Alifanya kazi kama siafu ili aweze kumaliza na kurudi nyumbani. Siku ile Tabu hakuweza kuhudhuria kipindi hata kimoja. Kazi ilikuwa ngumu sana. Tabu alionekana kuchoka. Mikono yake ilitoka malengelenge. Jasho lilimtoka kwa wingi na tumbo lilinguruma kuashiria kuwa ni muda wa kuweka chochote kitu mdomoni lakini hakuwa na la kufanya. Hatimaye, alipomaliza adhabu ile, nguvu zilimwishia, akashusha pumzi kwa nguvu.

Safari ya kuelekea nyumbani ilikuwa ndefu, nayo ilizidi kumchosha. Alitembea kama kinyonga huku amebeba mfuko wa madaftari kwapani.

Alifika nyumbani kwao bila kujua. Ilibaki kidogo apitilize kwa mawazo na uchovu aliokuwa nao. Alivuka barabara na kuifikia nyumba yao. Aliangaza huku na huko hakuona mtu. Alisukuma mlango na kuingia ndani.

"Nilikuwa nakusubiri. Yani wewe tokea saa nane ndio unarudi muda huu! Unajua nakutegemea wewe tu, siwezi kutembea na miguu yangu hii mibovu!" Mama Tabu alisema huku akimwangalia Tabu kwa macho yaliyojaa lawama.

"Shikamoo Mama!" Tabu alisema kinyonge huku akimsogelea mama yake jikoni.

"Marahaba umechelewa wapi? Unieleze kwanza!" Mama Tabu alihoji huku akiendelea kukaangaa maandazi yaliyokuwa jikoni. Tabu alimeza funda la mate na kumuomba mama yake amtazame aone jinsi alivyochafuka. Alimweleza jinsi alivyopewa adhabu kwa sababu ya kuchelewa shule.

"Wewe Tabu kama unaona mambo yamekuwa magumu bora uache tu hiyo shule maana huko ni kuteseka tu. Isitoshe Mwanangu nimepokea barua ya posa kutoka kwa Mjomba wako..." kabla mama yake hajamalizia usemi wake, Tabu alimkatisha na kujibu kwa sauti ya mshangao,"Posa! Yaani Mama pamoja na yote ninayofanya unataka niolewe kweli?" machozi yalianza kumtiririka tena.

"Ndio mwanangu, elimu yenyewe hii ya kijijini unadhani utafika wapi? Isitoshe hakuna aliyewahi kufaulu kwenye shule ya Tujijenge tangu ianze mwaka wa kumi sasa. Heri tupate mahari yako itanisaidia kwenda kutibiwa na nyumbani tutapata mwanaume wa kuangalia familia."

"Hapana mama mimi sipo tayari kabisa kuolewa nina ndoto nyingi nahitaji kuzitimiza."

"Hebu ongea taratibu kwani kila mtu anaitamani posa hii ya Mwalimu Nali. Mjomba amesema yeye ndiye atakayefanya maamuzi yote. Mimi na wewe hatuna lolote la kuongea. Isitoshe kwa umri wako zamani mtu alikuwa ana watoto wawili tayari."

"Nini...? Mwalimu Nali?" Tabu alijibu kwa sauti na kudondosha madaftari ambayo bado alikuwa kayashikilia.

"Nini? Hutaki kuishi maisha mazuri wewe? Mimi najuta kwa nini niliolewa na baba yako. Alikuwa mzee akaishia kufariki na kuniachia majukumu ya kukulea peke yangu. Wewe leo unampata kijana tena mwalimu unasema unachagua masomo?" mama aliongea huku akiyaweka maandazi yake ya kesho ndani. "Elimu hiyo ya mahangaiko haitakusaidia chochote unapoteza muda tu."

Siku ya Tabu iliishia kwa majonzi lakini alijipa moyo kuwa huenda kesho yake mambo yangeweza kubadilika. Alijilaza kitandani akiwa na mawazo mengi asijue wapi ataanzia kuitetea hatima yake.

Saa kumi na moja alfajiri siku iliyofwata, Tabu alishitushwa na sauti ya adhana. Aliamka na kuketi. Alitumbua macho yake gizani na hatimaye akanyanyuka na kuelekea bafuni. Alioga haraka haraka, akaanua nguo alizozilaza jana kweye kamba na kuingia nazo chumbani. Alipaka mafuta kisha akavaa harakaharaka na kutoka sebuleni. Aliusogelea mlango wa chumba cha mama yake na kuita;

"Mama, Mama?"

"Bee!" Mama Tabu aliitikia huku akijinyoosha.

"Shikamoo. Ndoo ipi nichukue?"

"Marahaba! Chukua yenye maandazi, hiyo yenye keki iache nitauzia hapahapa nje. Halafu chenchi pia ipo hapohapo kwenye ndoo ya keki." alijibu Mama Tabu na kujigeuza upande wa pili wa kitanda akavuta shuka na kujifunika vizuri.

"Sawa," Tabu alijibu na kurudishia mlango taratibu. Alibeba mandazi na kuanza safari. Alipofika njiani alianza kuyanadi kwa sauti, "Maandazi, maandazi ya moto moto…" aliendelea kuimba akivutia wateja.

"Oya Sista nipe matatu mia tano hii hapa mia moja chukua kwa konda." sauti ilimshtua Tabu na kumfanya aache kuimba na kukimbia pembezoni mwa gari kumfuata mteja ambaye alikuwa dereva wa gari.

"Na mimi nipe manne, hela hii hapa, changamka basi." alisema abiria aliyekuwa ndani ya gari na kumpa pesa dirishani.

"Usiondoke broo fasta nakupa *just wait*."

"Huku nipe matatu changamka gari linasepa." abiria mwingine alidakia akimkodolea macho Tabu.

Saa mbili kamili maandazi yalikuwa yamekwisha. Aliamua kusogea kwenye banda mojawapo ili aweze kuhesabu fedha alizopata. Mara akasikia sauti; "Aanh! Tabu nakuona mshiko kama wote."

"Wapi wewe kwa pesa hii ya maandazi au?" alijibu na kutabasamu.

"Wewe acha zako mtoto una hela siku hizi." alijibu yule kijana na kuanza kumsogelea.

"Hela wapi bwana! Acha kunipanga."

“Acha uongo taratibutaratibu tu hadi shule utaacha kama mimi.” alisema Sadiki na kuangalia kwa makini mfuko aliokuwa nao Tabu. “Heri uamue jambo moja Tabu mimi nahisi bishara itakutoa.” Sadiki aliendelea kunasihi huku akifuatana na Tabu njia moja kuelekea nyumbani.

“Bwana we… embu acha zako! Yaani niache kusoma nifanye biashara? Kama biashara inalipa mngekwishaendelea sana ninyi. Ona pale stendi mnavyohangaika kutoa chenchi.” Tabu alijibu kwa sauti huku akipunga mkono wake kupinga hoja za Sadiki.

“Ni kweli Tabu, lakini mtu utawezaje kusoma huku unafanya biashara?” alisema kijana mwingine aliyefuatana na Sadiki.

“Ni shida tu rafiki zinatufikisha huku.” alijibu Tabu.

Baada ya kuachana na kina Sadiki, Tabu aliendelea hadi nyumbani akiwa na mawazo mengi. Alipofika mlangoni, alipokelewa na macho ya mama yake, ambaye alikuwa akisubiri kwa hamu mapato ambayo angeleta Tabu.

“Tabu, wewe na mawazo yako ya shule. Kama usingepoteza muda wako na masomo, tungekuwa tunapata hela nyingi sana.” mama yake alisema.

“Maisha ni magumu mama, nataka kujaribu kuboresha hali yetu,” Tabu alijibu kwa unyenyekevu.

“Mwanaume aliyeletwa na mjomba wako anasubiri majibu yako. Fanya uamuzi mzuri kwa maisha yako,” Mama Tabu alisema akijaribu kumshawishi mwanae kukubaliana na mpango wa ndoa.

Tabu alijikaza kutoonyesha udhaifu mbele ya mama yake, lakini ndani ya moyo wake, alijawa na huzuni na hasira. Alipofika chumbani kwake, aliangua kilio. Hakuwa na hakika jinsi gani angeendelea na ndoto zake za kupata elimu katika mazingira kama yale. Hata hivyo, hakukata tamaa. Aliketi kitandani kwake na kufikiria njia za kuendelea na masomo yake bila kuingiliwa na shinikizo la ndoa na adhabu za Mwalimu Nali.

Usiku ulipokucha, Tabu aliamua kufanya uamuzi mgumu. Alichukua karatasi na kalamu na akaandika barua kwa Afisa Elimu wa Kata. Katika barua hiyo, alieleza kwa ujasiri azma yake ya kuendelea na masomo licha ya shinikizo la kuolewa. Alitoa sababu zake na kuomba asaidiwe ili aweze kuendelea na elimu yake.

Asubuhi iliyofuata, Tabu aliipeleka barua ile kwenye ofisi za kata na nyingine aliituma kwenye sanduku la posta la kituo cha habari. Aliamini angeweza kupata msaada wa haraka kwani maji yalishamfika shingoni. Aliamini moja ya sababu zilizomrudisha nyuma ni adhabu kali wanazopata wanafunzi kutoka kwa

walimu pamoja na umaskini unaopelekea wanafunzi wengi kuacha masomo na kuanza kutafuta kazi au kuolewa.

Tabu alihesabu siku akisubiri miujiza itakayomwokoa, wakati wote huo akiishi na hofu. Siku zilipita polepole huku akiendelea na biashara ya maandazi kama njia ya kuongeza kipato cha familia. Wakati huo huo, alifanya bidii katika masomo yake, akijitahidi kuwahi ili kuepuka adhabu ambazo zingemkosesha masomo.

Wiki kadhaa baadaye, Tabu alipokea barua kutoka kwa Afisa Elimu. Alikuwa na wasiwasi alipokuwa akiifungua, lakini moyo wake ulijaa furaha barua ilipomwambia kwamba ombi lake limepokelewa vizuri na kwamba watafanya kila wawezalo kumsaidia. Kupitia programu za elimu na msaada wa wachangiaji wa elimu katika eneo hilo, Tabu alipata fursa ya kupata ufadhili wa masomo. Hii ilikuwa habari njema kwake. Kwa mara ya kwanza, alihisi kuwa juhudi zake za kufikia ndoto zake hazikuwa kazi bure.

# Tone la Damu

Emmanuel Minja

Katikati ya kijiji kimoja huko Igunga, kulikuwa na dunia iliyokuwa bado haijaguswa na harakati za maisha ya mijini. Mashamba yalikuwa na mimea dhaifu isiyoweza kuulisha ulimwengu. Katikati ya mandhari hii tulivu, alikaa Rehema, akiwa ametazama hadi upeo wa macho, akili yake ikiwa imegeuka kuwa kimbunga cha mawazo. Alikuwa amemaliza elimu ya sekondari hivi karibuni, akiwa na ndoto kubwa kuliko mashamba yaliyomzunguka. Ugumu wa maisha ya kilimo uliovikuza vizazi vilivyomtangulia ulimwita, lakini ulipingana na hamu iliyowaka ndani ya roho yake ya kuutoroka. Jua lilipochomoza na kutupa miale yake ya dhahabu juu ya ardhi, moyo wa Rehema ulipambana na ukweli mgumu wa fursa chache katika kona hii ya dunia; ukweli ulioelemea mabega ya vijana kama yeye.

"Hapana, kwa nini dunia igeuke dhidi yangu?" sauti ya ndani ilinong'ona, akijipa matumaini katikati ya kukata tamaa. "Lazima kuna njia ya kutoka hapa."

Macho yake yalichunguza ardhi kavu ya Igunga. "Mwaka mzima umepita, nimekosa nini hadi nistahili adhabu hii?" alijiuliza akitikisa kichwa. "Siwezi kunyauka kama mimea hii inayochipuza kwenye udongo huu mkavu ulio chini ya miguu yangu."

Mawazo yake yalirejea nyuma wakati alipokuwa shule. 'Yaani kufeli kidato cha nne kunanidhalilisha hivi? Kwa nini kuteleza mara moja kuamue safari ya maisha yangu yote?' Sasa aliwakazia macho watu waliopita na majembe mikononi na kujiuliza, "Je, kilimo cha aina hii kinaweza kweli kuwa wokovu wangu katika nchi hii iliyokumbwa na ukame?"

Kwa mbali alisikia harufu ya kitu kinachoungua. Ilikuwa ni maharage aliyoyaacha jikoni kabla hajaelekea shamba kutafuta karanga za kuungia mboga. Alikiinua kiuno chake kama mjusi wa kondeni aonapo windo nono, haraka akafyatuka hadi jikoni. Bila kupepesa jicho, alikiepua chungu kile cha moto akakiweka chini upesi kabla hakijamuunguza!

"Ah! Maharage yenyewe yamengua *kiduchu* tu, nilifikiri jungu zima!"

Alibadilisha chungu akamiminia maji kutoka kwenye jagi na kukirudisha chungu mekoni. Alipomaliza, mawazo yake yalihamia katika simu. "Nimeiacha wapi?" Alikuna kichwa huku akivuta kumbukumbu kuwa mara ya mwisho

alipoitumia alimpigia nani na alikuwa wapi. Alikumbuka kuwa aliitumia kumtumia ujumbe Rajabu na alikuwa akiosha vyombo. "Huenda nitakuwa nimeiacha kwenye kichanja cha vyombo; na pengine Rajabu ameshaujibu ujumbe wangu." aliwaza. Ilibidi akiache kigoda chake aifuate simu ili kujua kilichojiri. Aliikuta kwenye kichanja akaanza kusogoa na Rajabu akimweleza jinsi shughuli za kijijini zilivyomuelemea bila kumpa faida yoyote. "Katika kipindi kifupi baada ya wazazi wangu kufariki, uso wangu ulizidi kukondeana na mwili wangu kusadifu umbile la mnazi. Nimeendelea kufanya kazi ngumu shambani bila mafanikio na hali yangu ya kimwili inazidi kudhoofika," alimweleza rafiki yake huyo.

Baada ya mazungumzo marefu ya takribani dakika saba, Rajab aliahidi kumsaidia Rehema. Alimwambia juu ya mipango kambambe wa kusafiri kuelekea jijini Dar es Salaam kuanzisha biashara mpya.

"Mungu si Athumani! Waliotabiri anguko langu sasa yatawapwaya." alijisemea kimoyomoyo wakati anakula ugali kwa furaha mchana ule, "*sio kwa suprise* ile ya Rajabu!"

Machweo matatu tokea siku ile, Rehema hakuwa anaihisi baridi kali ya Igunga tena. Alihisi yuko Dar tayari. Rajabu alikuwa amekwishawasili Igunga, wakawa wanapanga namna watakavyosafiri kuelekea Dar es salaam. Pamoja na taswira ya Jiji la Dar ambayo ilimuongezea Rehema morali ya safari, Rajabu alimkosha zaidi pale alipomwambia, "Kuna njia rahisi ya kufika Dar es Salaam. Kuna uwezekano wa kupata usafiri wa malori ya mizigo kwa gharama nafuu au bure kabisa. Cha msingi ni *kuset* muda mzuri na mahali poa."

Rehema alitabasamu kwa furaha na kushukuru bahati yake. "Mungu ni mwema," alisema kwa sauti ndogo. "Naona maisha mapya yanakaribia, na nina matumaini makubwa."

Baada ya kuweka mipango sawa, siku ya safari iliwadia. Ilianza kwa kutafuta magari ya mizigo. Rehema na Rajabu walisimama pembeni mwa barabara wakisubiri malori yanayopita wayasimamishe kuomba *lift*. Pandisha mikono, shusha, pandisha, shusha, pandisha shusha, wapi! Hakuna lori lililosimama. Taa ziliwapita na upepo wa mwendo kasi ukizipangusa nyuso zao. Hatimaye Rehema alikata tamaa. Alidhani labda haikuwa siku ama saa sahihi ya wao kuondoka Igunga. Alisogea nyuma kidogo lakini Rajabu hakukata tamaa. Yeye aliendelea kukaa kando ya barabara huku akiutizama mkono wenye saa yake kila mara kama mtu aliyeumizwa na kitu. Alipungia mkono kila lori lililopita kwa kubahatisha!

Usiku ukaendelea kuwa mwingi na kupiga giza totoro. Ghafla mwanga mkali ulionekana kutokea upande wa barabara itokayo Geita kwenda Singida. Bila kufahamu ilikuwa ni muda gani, Rehema alitamani amuulize Rajabu ambaye aliendelea kuitazama saa yake na kujisogeza karibu zaidi na barabara ili apunge

tena mkono. Rehema hakutegemea matokeo tofauti, akiwa tayari amekata tamaa akidhani safari imeyeyuka kama barafu au kupeperuka kama karatasi. "Huyu hatasimama na muda umekwenda sana. Labda tujaribu siku nyingine." aliyaumba maneno hayo kichwani akidhani ndiyo yatakayozaliwa kinywani mwa Rajabu. Taa zilivyosogea karibu, naye Rajabu alisogea zaidi barabarani. Safari hii alitembea hadi katikati ya barabara. "Ha! Ana akili kweli huyu?" Rehema alihamaki. Bila kufikiri alijikuta ameshafika barabarani na kumkwapua Rajabu pale alipokua amejiezeka, akamkokota hadi kando ya barabara.

Rajabu alimgeukia Rehema na bila kusema lolote, akaukwida mkono wake, akachoropoka na kurudi barabarani, akainyoosha mikono yake yote miwili. Alichoreka kama mtu anayetaka msaada wa haraka, ama kumuashiria dereva kuwa mbele kuna hatari. Rehema alihisi mikono ya Rajabu ikimsukuma pembeni huku akisema; "Huyu atasimama."

"Wewe, unafanya nini?" Rehema aliuliza kwa sauti ya kukaripia iliyochanganyika na woga.

"Tulia, *gemu* nililocheza lazima asimame." Alipomaliza kusema hayo, Grrrrrr! Kelele za breki zilizochoka zilifungwa pembeni yao ukachomoza uso mwembaba wenye gadhabu kutoka ndani ya lori lile, uliobebwa na mwili nyorodofu ukiwa uliotilia kofia kama ya wacheza gofu.

"Kuna shida gani?" dereva aliongea kwa sauti ya dharau huku akimkazia macho Rajabu. "Tuuu… tuna... shida…" Rehema alijibu kwa sauti ya kukwaruza, akijaribu kumwepusha Rajabu asipigwe na dereva yule aliyeonekana kukerwa na kitendo chake.

Rajabu alisimama kidete na kuanza kuzungumza na dereva kwa unyenyekevu, "Tunahitaji kusafiri kwenda Dar es Salaam. Tunaomba msaada wako Mkuu. Tutakulipa fedha kiasi ukituruhusu tusafiri nawe."

Dereva alimpa kisogo Rehema wakati anazungumza na Rajabu. Alichukua muda kufikiria hoja za Rajabu hadi alipotoa leseni na kumweleza ya kuwa hata yeye ni dereva hodari wa malori ya mafuta hivyo angemsaidia kuendesha gari pale atakapokuwa amechoka. Takribani dakika tano za ulumbi wa Rajabu zilifanikiwa kuwapa ridhaa ya dereva yule. Rajabu alimpa fedha zilizofungwa kwenye bahasha. Dereva alizeweka kwenye mfuko wake wa suruali na kusema, "Haya pandeni haraka twende, lakini safari yangu itaishia Dodoma."

Bila kupoteza muda Rehema na Rajabu walirukia lori kwa upande wa abiria nyuso zao zikiwa zimejaa tabasamu; na baada ya kuitosa leseni ya Rajabu kwenye dashi ya gari, dereva alikanyaga mafuta gari likaanza mwendo.

Safari ilipambwa na masimulizi ya ushujaa, ikiwa ni pamoja na Rehema

kumsifu Rajabu kwa uhodari wake wa kusuka matukio. Walipofika Shelui, Rajabu alishauri waingie kwenye mgahawa mmoja anaoujua wakapate kahawa. Alimuomba Rehema atoe chupa yake ya chai wakaitumie kumchukulia kahawa dereva ili apate kupumzika. Kutokana na uchovu wa barabarani, dereva aliwakubalia ombi lao.

"Haraka nendeni mimi nitapumzika kidogo nyuma kwenye kontena."

Rajabu alimwambia Rehema atangulie ampe nafasi ya kumshawishi dereva akubali kusafiri nao hadi Dar es Salaam. Baada ya dakika tano hivi, Rajabu aliungana na Rehema mgahawani, mkononi kashika ufunguo wa gari. Akasema,

"Nimepanga na dereva kuwa tutakaporudi, nimpokee kuendesha ili apate usingizi kidogo kwa sababu hajalala kwa siku tatu."

Walipata vikombe kadhaa vya kahawa wakaweka nyingine kwenye chupa kwa ajili ya dereva, kisha wakalirudi garini huku wakiwa wanazungumza jinsi kulivyokuwa na watu wengi mle mgahawani licha ya kuwa muda ulikuwa umesonga sana. Rajabu alieleza kuwa mgahawa ule ulikuwa unapendwa sana na madereva wa malori wapitao njia hiyo usiku.

"Hatuna sababu ya kuishia Dodoma," Rajabu alianzisha hoja mpya. "Itabidi tumshawishi mjamaa tuteremke nae hadi Dar."

"*Yeah!*" alikubali Rehema. "Unaonaje tukaufanya ushawishi huu wakati tunampa kahawa? Na jinsi ulivyo fundi wa kuuza maneno, ukimkalia freshi mbona hakishindikani kitu?"

"Hapana, tusimsumbuae kwa sasa. Wacha apumzike hadi tufike Dodoma. Ataingia *line* tu, niachie mimi hii kazi."

Miguu na mikono ya Rajab vilishirikiana vilivyo kuliburuza lori lile mpaka Dodoma. Ilikuwa ni muda sahihi wa kumwamsha dereva wa lori na kuanza mazungumzo ya kuirefusha safari yake. "Wakati anakunywa kahawa tutapiga nae stori za hapa na pale na kuchukua nafasi hiyo kumshawishi achukue *bonus* ya safari. Hakuna namna atachomoka." Rehema aliwaza peke yake huku akiteremka na kuelekea nyuma ya kontena kumuamsha bila kumshirikisha Rajabu ambaye alikuwa anapooza injini kabla ya kuizima.

Mlango wa kontena ulikuwa haujafungwa vilivyo. Alipoufungua alistaajabu kuona katika ule mwanga hafifu kuwa hakukuwa na mizigo mingi mbali na viroba kadhaa! 'Ina maana mzigo mzima wa huyu jamaa ndo hivi vijiroba!' alijiuliza. Alipanda na kuingia ndani ya kontena ili amuamshe. Vidole vyake vikakutana na unyevu unaotelezateleza. Alipounusa, alikumbana na harufu ya uozo. Aliwasha tochi ya simu yake imuwezeshe kuona vizuri, ndipo alipobaini kuwa vidole vyake vimetapakaa damu. Kumulika zaidi kwenye kontena, akaona michirizi ya damu

ikiongezeka kadri inavyozidi kusogea mbele. 'Ameuliwa?' akili ilimruka. 'Yaani hili litakuwa limetokea muda mfupi tu tulipoondoka kwenda mgahawani? Na kama kweli ameuliwa, mwili wake uko wapi?' Wakati Rehema anajiuliza maswali mfululizo, nywele zilikuwa zimesisimka kwa uoga na mwili wake ulikufa ganzi.

Aliganda kwa sekunde kadhaa. Alipozinduka, Rehema aliruka chini na kumfuata Rajabu. Rajabu alielewa taharuki aliyokuwa nayo Rehema alipoiona mikono yake iliyopakaa damu na uso wake ulivyosawijika.

"Amekufa!" ndilo neno pekee lilitoka mdomoni mwa Rehema.

Rajabu aliteremka kwenye gari bila kusema neno, akaelekea eneo la tukio kwa mwendo mchanganyiko wa mbio na hatua ndefu. Macho yake yalionekana kutawaliwa na sintofahamu ya aina moja au nyingine. Alipanda kwenye kontena lililokuwa limeachwa wazi na Rehema ambaye alikuwa anamfuata nyuma. Walipoingia ndani, Rajabu alimulika kila upande akiifuatilia ile damu ilipoanzia. Ndipo walipouona mwili ambao ni tofauti na ule wa dereva aliyewafadhili. Tofauti ilikuwa mwili mdogo wenye kichwa chenye kipara na mfupi kwa kimo.

"Ni nani huyu?" Rehema aliuliza kwa sauti ya kunong'ona akidhani anaongea peke yake lakini sauti yake ilimfikia Rajabu.

Akiwa amezidiwa na tafakuri, Rajabu alikutanisha macho na Rehema akamuuliza, "Ulilikuta kontena likiwa wazi?"

"Hapana, lilikuwa limefungwa na komeo bila kufuli."

"Hawa watakuwa ni wezi, Rehema. Waliiba mzigo wakati tulipokuwa mgahawani, na labda walipokutana na upinzani watakuwa wamemteka dereva wetu wakamweka huyu marehemu ili kututisha au kutuuzia kesi."

Rehema alijaribu kuelewa lakini akili yake ilikataa kupokea mantiki yoyote iliyohusiana na matukio aliyokuwa anayashuhudia. Aliidadisi sura ya Rajabu aone kama yeye alikuwa na ujasiri wa kuwanasua kwenye janga lile lakini alichokiona ni hofu inayoshindana na ile aliyokuwa nayo.

"Rey," Rajab alimwita Rehema kwa jina lililokuwa limezoeleka kwa rafiki zake wakati walipokuwa shuleni. "Sasa tunafanyaje?"

Rehema alitaka kusema jambo, lakini alishindwa. Bado alikuwa anatetemeka kwa hofu asijue anaanzia wapi.

"Pakia kwenye gari tuendeshe hadi nje ya mji. Hapo ndipo tunaweza kujadili tufanye nini." alisema Rajabu, hatimaye.

"Twende tukajisalimishe polisi tuwaeleze kilichojiri, huenda tutapata msaada. Vinginevyo, tutakuwa tunajitia hatiani." alishauri Rehema kutokana na

uzoefu wake wa kufuata taratibu.

“Inabidi tutokomee porini, tutajadili cha kufanya mbele ya safari.” Rajabu alisisitiza huku akimvuta Rehema kutoka upande wa kontena na kurudi naye mbele ya gari. Hakumpa muda wa kififikiri zaidi. Mara walipoingia ndani ya gari, Rajabu aliwasha gari wakaendelea na safari.

Kimya kilitawala katika siti zile mbili. Rajab alikaza macho yake mbele akiwa amezama kwenye mawazo. Rehema alimtazama kwa kuibiaibia, tumbo lake likiwa bado linakata kwa uoga. Walisafiri hadi jua lilipoanza kuchomoza bila kukutana na kichaka walichokuwa wamepanga kukitumia kuyasitiri matatizo yao. Alipoona hali ya hewa inazidi kuwa ngumu, Rehema aliamua kuuliza kama kuna mpango mbadala lakini hakujibiwa. Mishale ya saa ya Rajabu ilisoma saa kumi na mbili asubuhi. Rehema aliona mwendo wa gari ukianza kupungua, hadi Rajabu alipoliegesha kando ya barabara.

“Kuna tatizo?” aliuliza.

“Naenda kuchimba dawa.” Rajabu alijibu kwa mkato huku akishuka haraka kwenye vidato vya kushukia upande wa dereva.

Punde si punde polisi wa usalama barabarani walilisogelea lori wakitaka kujua kulikoni. Moyo wa Rehema ulienda kasi na kudunda kama unataka kutoka. “Hujui kitu. Humjui Rajabu. Utatulia humuhumu ndani.” alijishauri mwenyewe kujipa moyo alipowaona polisi akilisogelea lori.

Zilikuwa zimeshapita takribani dakika kumi bila Rajabu kurudi. “Dawa gani anachimba muda mrefu hivyo? Hili janga peke yangu nitalipeleka wapi?” Rehema alijiuliza maswali yasiyokuwa na majibu. Hatimaye akawaza, “Isije ikawa Rajabu anafanya jambo huko nyuma bila kujua hatari inayotunyemelea.”

“Msichana,” sauti kali ilitoka mdomoni kwa askari polisi mwanamke mara tu mguu wa Rehema ulipokanyaga chini. Aligwaya kidogo kisha akajikaza lakini hakujibu kitu.

“Nini kinaendelea hapa? Mwenzako yuko wapi?”

“Mwenzangu?” Rehema alijidai kutokumuelewa.

“Hujaelewa nini hapo?”

“Hapana, hakuna kitu.”

“Dakika kumi sasa tangia azamie huko porini, hajarudi na wewe unajishusha uende wapi? Mnafanya mchezo ee! Kwani nini ameegesha gari sehemu hatarishi?” maneno yake yalivuruga kila utumbo ndani ya mwili wa Rehema. Alitamani ardhi ipasuke angalau immeze na kumtapikia Igunga.

"Mtaka cha uvunguni sharti ainame kweli, lakini kama kuinama kwenyewe ndiko huku, vya uvunguni na vibaki hukohuko." Rehema aliendelea kuwaza na kuwazua, "Ina maana Rajabu amekimbia zali ama wakati anarudi amewashtukia askari polisi akajibanza? Iwe iwavyo, zigo limenishukia sijui nitaeleza nini." Akiwa katika mparaganyiko huo wa mawazo, polisi alianza kumhoji.

"Hebu nieleze mmebeba nini humu ndani?"

"Wapi? Ee… sijui wenye…we…" Rehema alijibu kwa kubabaika, kichwani akitafuta maneno yatakayomtenganisha na balaa lile lakini mwili wake haukumpa ushirikiano. Mikono ilitetemeka na jasho jembamba likinitiririka akijua kwamba kama polisi wakifungua kontena jela ingemhusu. Wakati huo askari polisi wanne walikuwa wamesimama nyuma ya lori lile wakidai lifunguliwe.

"Mpigie dereva aje kulifungua kontena tulikague," yule askari polisi mwanamke aliamuru.

Rehema alipata wazo, "Samahani, sina namba yake. Mimi niliomba lift tu njiani." alichanganya ukweli na uongo kwa sauti inayoaminika.

Askari polisi mwingine alipanda akalifungua kontena. "Hii ni nini? Uvundo wa kuzimu gani huu?" aliuliza akiwa anamulika kwa tochi ya simu yake kuona kuna nini. "Eh, eh, eh! Hii ni *murder case!*" aliwatahadharisha wenzie, mmoja baada ya mwingine wakapanda na kuingia kwenye kontena. Chini alibakia Rehema na yule askari mwanamke.

"Uko chini ya ulinzi," alisema na kumfunga Rehema pingu mikononi, "utaisaidia polisi."

Kulikwishapambazuka na magari mengi ya polisi yakwishalifika eneo la tukio. Hakukuwa na Rajabu wala dereva aliyetoa lift, bali Rehema tu ambaye hakuwa na fununu ya chochote ya kile kilichokuwa kimejiri.

Kutokana na mazungumzo ya polisi, Rehema alibaini kuwa licha ya kuwa na maiti ndani ya kontena, kulikuwa pia na viroba vya mihadarati.

Akiwa na pingu mikononi, alisafirishwa hadi kituo cha polisi Gairo na kukabidhiwa kwa dada mmoja aliyevalia suti nyeusi, ambaye baadae Rehema aligundua kuwa ni mpelelezi. Askari alimuongoza kuingia kwenye chumba maalum cha mahojiano. Alianza kwa kumuuliza maswali kadhaa, kisha akamtaka aseme yote ambayo alikuwa anayafahamu.

"Potelea mbali, nitasema yote ninayoyajua liwalo na liwe." hatimaye aliamua Rehema.

Alikaa rumande yapata mwezi, wakati polisi wakiendelea na msako wa

Rajabu na genge lake. Rehema hakuyaamini masikio yake ripoti ya upelelezi ilipobainisha kuwa Rajabu, jirani yake waliyecheza na kusoma pamoja tangu shule ya msingi hadi sekondari alikuwa amemgeuza kuwa chambo! Askari polisi walimuonesha picha yake athibitishe kuwa ndiye aliyeondoka naye Igunga. Kumbe maiti iliyokuwa kwenye kontena ilikuwa ya askari mpelelezi aliyekuwa amemwekea mtego dereve wa lile lori lakini Rajabu na mtandao wake walimshtukia wakahakikisha wanammaliza. Hata aliposema anakwenda kuchimba dawa, kumbe alikuwa amewashtukia polisi akaamua *kusepa* na kumuachia Rehema muziki apambane nao.

Pamoja na lawama, Rehema alihuzunika nilipoitazama picha ya Rajabu yenye ujumbe chini: ANATAFUTWA NA POLISI!

# Uyoga

Zahara Tunda

Akiwa na miaka 26 Mariam Kapona, mwanamitindo na muimbaji maarufu jijini Dar-es-salaam, alikuwa na kila kitu ambacho vijana wengi wa kileo walitamani kuwa nacho. Mashabiki wake walizidi kuongezeka kila kona ya nchi hasa alipojiingiza katika tasnia ya uigizaji wa filamu. Yeye alipenda kufanya kile alichohisi ni sahihi kwake, kwa familia yake, na jamii inayomzunguka. Lakini kama usemavyo wimbo maarufu wa kizazi kipya wa 'Usinipangie', hakupenda kabisa kupangiwa.

Licha ya kuwa na kila kitu Mariam hakuwahi kuonekana kuwa na mpenzi; hivyo watu wengi walitamani kufahamu kuhusu maisha yake ya mahusiano. Mara nyingi akihojiwa na waandishi wa habari hawakusita kumuuliza kuhusu maisha yake binafsi. Walitaka kujua inakuwaje msichana mrembo kama yeye kukosa mpenzi wakati ana sifa zote ambazo takriban kila mwanaume anapenda mpenzi wake awe nazo. Hana makuu, mtafutaji na anayajua maisha, yaani '*wife material*' kama wasemavyo watoto wa mjini wakimaanisha mwanamke mwenye sifa za kuwa mke.

Siku moja Mariam alikuwa na mahojiano mubashara na mtangazaji maarufu nchini wa kipindi cha Ndoto Zangu kilichokuwa kinarushwa kuanzia saa 3 hadi saa 5 usiku kwenye Televisheni ya Taifa. Mtangazaji Sabrina aliyejizolea umaarufu kutokana na weledi na umahiri wake katika uulizaji wa maswali ndiye aliyekuwa akikisimamia. Watu wengi walikipenda pia kwa sababu kilikuwa kinarushwa hewani baada ya saa za kazi. Basi siku hiyo karibu kila Mtanzania aliweka stesheni hiyo ili aweze kujua mengi kuhusu Mariam.

Kibao cha Westlife "*I have a dream*", yaani 'Nina Ndoto' kilisikika kwa mbali, kikiwafanya watu wazidi kusubiri kwa hamu ni kipi Mariam ataongea usiku ule kuhusu ndoto zake. Mbali na kusubiriwa kote kule lakini hadi saa 3:30 Mariam alikuwa hajaingia Studio. Baadhi ya watu wakaanza kutoa maoni yao kuhusu kitendo kile kupitia mitandao ya kijamii. Ilimchukua muda Sabrina kuanza kuwajibu watazamaji na kuwaambia kuwa changamoto ya foleni ndiyo imemchelewesha Mariam.

"Jamani tuwe na subira kidogo. Mariam karibu ataingia humu ndani kwa ajili ya mahojiano yetu," alisema Sabrina.

"Mmh! Jamani mbona wanachelewa hivyo? Kesho shule," mwanafunzi

mmoja mwenye shauku ya kusikiliza mahojiano hayo akilalamika.

"Tupate matangazo kidogo tutarudi muda si mrefu kuendelea na mahojiano yatakayorushwa mubashara hapahapa studio. Usiondoke kwenye runinga yako mambo ndio kwanza yanaanza," alisisitiza Sabrina akihamasisha watazamaji.

Punde matangazo ya biashara yakaanza kuoneshwa. Baada ya muda mfupi tu Mariam akaingia kwa mbwembwe. Alikuwa amevaa gauni fupi jeusi na mkanda mwekundu vikisindikizwa na viatu vyeusi vya mchuchumio pamoja na hereni ndefu za fedha zilizotikisika kila alipogeuza shingo kwa madaha. *Viwalo* hivi vilimfanya azidi kuwa mrembo wa kuvutia machoni mwa watazamaji.

"Karibu katika kipindi chetu cha Ndoto Zangu Mariam," alianza Sabrina.

"Nashukuru sana Sabrina na Watanzania wote kwa ujumla, ni matumaini yangu kuwa wote ni wazima na mnataka kujua mengi yanayonihusu. Asanteni na karibuni," aliongea Mariam huku akitoa tabasamu ambalo lingeweza kumfanya mtu asiyeona ahisi kuwa mtu huyo kweli ametabasamu.

Sabrina akaanza kumhoji Mariam maswali mengi yakiwemo yanayohusu historia yake na ya familia yake kwa ujumla. Hakuacha kuchokonoa kuhusu changamoto ambazo aliwahi kukutana nazo katika kutimiza ndoto zake.

"Naitwa Mariam Mathias Kapona. Ni mtoto wa tatu katika familia ya watoto saba, wanawake wanne na wanaume watatu. Dada zangu wote kwa sasa wanaishi nje hivyo ni mimi, wadogo zangu pamoja na kaka yangu ndio tunaishi nchini Tanzania. Baba yangu alifariki wakati mdogo wangu wa mwisho anazaliwa. Alipata ajali kipindi anawahi kwenda kumuangalia mama hospitali. Baada ya kusikia kuhusu kifo cha baba, mama naye akapata mshtuko na kufariki hapohapo, ndipo tukabaki yatima." Mariam akanyamaza na kufuta machozi. Kisha akaendelea na kisa chake ambacho kilianza kuwafanya watazamaji wasikilize kwa makini huku wengine wakilengwalengwa na machozi.

"Eeh! Pole sana Mariam, unaweza kuendelea *dear*, nini kilifuata baada ya wazazi wako kufariki?" Sabrina akamuuliza swali la mwendelezo kama kawaida yake.

"Baada ya hapo nikaanza kuishi na dada zangu tukisaidiana kumlea mdogo wetu. Kipindi hicho nilikuwa nasoma sekondari pale Kisutu, hivyo niliendelea na maisha huku nikijitahidi kwani sikupenda wadogo zangu waje kuteseka." Mariam alinyamaza akanywa maji taratibu.

"Vipi kuhusu mahusiano ulikuwa na kaboifrendi au ndio ulikuwa msomi *msongo*?" Sabrina alimchomekea Mariam maswali ya uchokozi.

"Mmh! Sabrina jamani, *of course*, nilianza kuwa na mahusiano na kijana mmoja anaitwa Daevick, ambaye kwa kweli nilikuwa nampenda sana."

"Eeh! Kipi kilifanya useme ulikuwa unampenda kana kwamba humpendi tena? Na kwa nini mpaka sasa huna mpenzi licha ya kwamba umri unazidi kwenda?" Sabrina akashindilia mwiba mwingine katika kidonda kibichi cha Mariam.

"Daevick alikuwa amenipita vidato viwili. Mimi nilikuwa kidato cha tatu pale Kisutu yeye akiwa kidato cha tano Azania. Tulikuwa tunapendana we acha tu. Mapenzi yetu yalikuwa ya kusaidiana kwa shida na raha lakini tulisema kuwa tusifanye ngono mpaka tutakapomaliza shule na zaidi, mpaka tutakapofunga ndoa.

"Kipindi hicho nilikuwa na rafiki yangu ambaye alikuwa kama pacha wangu tuyelikuwa tunacheza, kula, hata kutembea pamoja. Yeye alikuwa akiishi Tandika na mimi nilikuwa naishi Kijitonyama. Ila umbali wa kwetu na kwao haikuwa sababu kwani kipindi hicho tulikuwa tumeanza kukaa hosteli za pale shuleni. Sakina alikuwa anapenda sana starehe. Licha ya kwamba ndio kwanza alikuwa kidato cha tatu, alipenda sana kwenda kwenye kumbi za starehe. Mara nyingi alitoroka shule kwenda Billicanas au Maisha Club kwenye muziki.

"Kila mwisho wa wiki tulikuwa tukienda ufukwe wa Coco mimi na Daevick bila Sakina kwani sikutaka ajue kama nina rafiki kama Sakina. Basi siku moja tulipokuwa ufukweni Daevick akaniomba nimbusu, kwa kweli sikuweza kwani nilikuwa mwoga sana katika mapenzi. Hapo ndipo Daevick akaniambia huku akiwa amekunja uso, 'wewe mwanamke wa aina gani? Yaani huwezi hata kumfurahisha mpenzi wako, je ningekuomba tukalale wote si ndo ungeenda polisi kabisa?'

"Kusema kweli niliumia sana kwani sikutegemea kama Daevick ambaye tulikubaliana kuwa hatutafanya chochote tukiwa bado wanafunzi ndiye kanibadilikia namna ile. Nilimuomba tuondoke, akanijibu kuwa ningeweza kwenda, yeye alikuwa hajisikii kuondoka na mimi. Nikaondoka. Nilipofika hostel nililia sana kwani nilihisi dunia yote imenielemea.

"Baadhi ya rafiki zangu waliniuliza kulikoni nikawaambia nipo sawa ingawa kwa kweli sikuwa sawa hata kidogo.

"Maisha yaliendelea lakini Daevick alianza kuwa kimya; kila siku mpaka nimtafute mimi. Basi siku moja alikuja hosteli akaniomba msamaha tukaendelea na maisha yetu kama ilivyokuwa awali. Akanifundisha jinsi ya kupiga gitaa kwani alikuwa akipenda sana muziki. Nilipoingia kidato cha nne na Daevick akiwa kidato cha sita, sote tulikuwa tumepania kufanya vizuri katika mitihani yetu ya

mwisho. “Daevick aliondoka kwenda Arusha mara baada ya kumaliza kidato cha sita. Aliporudi, tukiwa bado tunasubiri matokeo ya Mtihani wa Taifa, tuliendelea na mahusiano yetu kama kawaida lakini Daevick hakuwa mchangamfu kama zamani. Matokeo yalipotoka, nilikuwa nimefaulu kwenda Shule ya Sekondari ya Jangwani kuendelea na masomo yangu ya kidato cha tano na cha sita. Hii ilikuwa hatua muhimu ya kuniwezesha kufikia ndoto yangu ya kuwa daktari.” Mariam alinyamaza huku akimuangalia Sabrina kwa jicho la ‘naomba niishie hapa’.

“Eeh! Nini kilitokea mbona wewe sio daktari na kwa nini nyimbo zako nyingi zinahusu mapenzi?” Sabrina alimuuliza Mariam swali juu ya swali.

“Basi niliamua kwenda kumtaarifu Daevick kuwa nimechaguliwa kuingia Kidato cha Tano Jangwani, shule iliyopakana na shule yake ya zamani ya Azania. Akanipongeza kisha akaniambia nisome sana ili nije kuwa daktari kwani ana imani nitakuwa daktari ambaye ana huruma na wagonjwa wake.

“Tuliongea mengi kisha nikaaga na kurudi nyumbani kujiandaa kujiunga na shule yangu mpya. Nilipofika shuleni, badala ya kupangiwa mchepuo wa sayansi nikajikuta nimepangiwa wa sanaa. Niliumia sana ila sikuwa na jinsi. Laiti ningejua mapema kuwa inawezekana kubadilisha michepuo bila shaka ningeomba nibadilishiwe. Ila ndio hivyo tena, sikuwa na uelewa huo wala watu wa kunishauri. Ilinibidi nisome hivyohivyo japo Daevick na ndugu zangu pia walitamani niwe daktari. Pamoja na hayo sikuwaza kama nitakuja kuwa mwanamuziki au mwanamitindo.”

Mariam alinyamaza kidogo, kisha akaendelea na simulizi yake. “Ilikuwa siku ya Jumapili nilipoamua kwenda kwa Daevick bila taarifa. Nilimpelekea zawadi kwa kuwa ilikuwa ni siku ya kuzaliwa kwake. Nilipowasili nyumba ilikuwa kimya sana. Nikapita kwa nyuma karibu na dirisha la chumba chake, nikasita kidogo. Kutoka chumbani nikasikia sauti ya mwanamke akisema, ‘Nadhani sasa ni wakati wa kumwambia Mariam. Nimechoka kuficha ukweli na ukiangalia, tupo kwenye mahusiano kwa muda mrefu sasa.’

“Ile sauti ilikuwa ya rafiki yangu Sakina. Kwa kweli nilihisi kufa lakini nilijikaza kuyazuia machozi kunitoka. Moyo wangu ulikufa ganzi nipomsikia Daevick akimjibu kuwa asiwe na wasiwasi ataniambia muda ukifika. Nilipochungulia dirishani, sikuamini nilichokiona. Walikuwa uchi wa mnyama, Sakina akiwa amelala kifuani kwa Daevick!

“Nilibaki pale nimeganda kwa muda dakika 10 hivi. Hata hivyo, nilipiga moyo konde, nikazunguka hadi mlangoni nikaiweka ile zawadi kwenye kizingiti na kuondoka. Nilijiuliza maswali mengi kichwani! Ni lini na wapi Sakina na Daevick walionana?

"Ndani ya wiki moja nilikuwa nimeshaingia Kidato cha Tano, nikichukua masomo ya Kiswahili, Kiingereza na Kifaransa almaarufu KLF. Bila kutarajia, nilitokea kuyapenda na kuyafurahia masomo haya, lakini ukimya na usaliti wa Daevick ulinikosesha raha. 'Ina maana hakujua kama niliwaona? Au hakuona zawadi niliyomwekea mlangoni?'

"Siku zilipita bila ya Daevick kunitafuta. Na mimi sikumtafuta kwani mapenzi yangu kwake yalikuwa yamekwishaingia dosari; na wala sikutaka au kutamani tena kuwa na mahusiano na mtu mwingine yeyote.

"Miezi ikakatika na siku pia. Nikamaliza Kidato cha Sita. Kipindi hicho dada zangu wote wawili walikuwa wameshakwenda Ughaibuni hivyo, wakanialika niende likizo huko wakati nikisubiri matokeo yangu ya Mtiani wa Taifa. Nikatinga Marekani katika jiji la Chicago jimboni Illinois.

"Huko ndipo nilipokutana na mwanaume raia wa Ghana ambaye nilimpenda nilipomuona tu, kinyume na azma yangu ya kutokupenda tena. Ingawa macho yetu yaliongea sikumwambia kwani kwa mila na desturi zetu za Kiafrika eti ni kitendo cha aibu kwa mwanamke kumwambia mwanaume kuwa anampenda.

"Baada ya wiki mbili yule kijana alianza kunizoea kwa sababu dada yangu alikuwa na mgahawa mkubwa katika mtaa wa Alexandria ambao uliitwa *African Cuisine*. Ulikuwa na vyakula mbalimbali vya Kiafrika na Waafrika wengi walikuwa wanapenda kufika pale kula na kubarizi. Siku moja alinikaribisha kwenye meza aliyokaa, akajitambulisha kuwa anaitwa Raj na yupo Marekani kwa ajili ya masomo. Hata sikutaka kumdodosa asili ya jina lake ambalo nilisoma shuleni kuwa linamaanisha mfalme kwa Kihindi. Bila kusita aliniambia amevutiwa na mimi na anatamani siku moja nije kuwa mke wake. Sikujibu chochote zaidi ya kumuangalia tu. Kidhati nilitamani kuwa naye ila kila nilipofikiria usaliti wa Daevick nilitonesha kidonda cha mapenzi kilichokuwa hakijapona.

"Baadaye Raj aliendelea kuja *African Cuisine* tukajenga mazoea. Siku moja alinialika kwake. Ilikuwa nyumba kubwa yenye vyumba kama sita na bwawa la kuogelea. Kulikuwa na picha zake nyingi na za wazazi wake; na sebuleni kulikuwa na kinanda kikubwa. Raj akaniuliza kama napenda kupiga kinanda, nikamjibu kuwa nilikuwa naweza kupiga gitaa tu, akaahidi kunifundisha kama nikipenda.

"Matokeo ya Kidato cha Sita yalipotoka, nikawa nimefaulu. Dada yangu akanitafutia chuo Marekani kusomea muziki na uwanamitindo. Mpaka hapo nilikuwa sijasikia na sikutaka kujua chochote kuhusu Daevick.

"Nilianza masomo yangu huku nikiendelea na uhusiano wangu na Raj. Alikuwa ni muelewa na mpole. Hakupenda kuniudhi wala kunifanya nihisi

upweke. Ikafikia kipindi akawa anataka tuanze mahusiano ya kimapenzi rasmi." Mariam aliendelea kutiririka. Sabrina alikuwa kimya, maswali yamempotea.

"Nakumbuka ilikua siku ya Jumamosi. Raj akaniomba tutoke tukale chakula cha usiku. Ilikuwa siku yenye upepo mwanana na hali ya ubaridi kidogo. Raj aliagiza mvinyo tukaanza kunywa huku tukisikiliza wimbo wa Lionel Richie wa '*I Call it Love*'—yaani 'Nayaita Haya Mapenzi'. Nilitamani kucheza ila kabla sijamwambia Raj nahisi alijua. Aliinuka, akaninyooshea mkono kuniashiria nimfuate, tukaanza kucheza.

"Baadae nilimuomba DJ kuimba akaniruhusu. Nikaimba wimbo wa Whitney Houston wa '*I will always love you*'—yaani 'Daima Nitakupenda'. Watu walipiga makofi wakaomba nirudie. Nikawaomba msamaha na kuwaambia wimbo ule nilikuwa namuimbia mpenzi wangu Raj.

"Basi tukarudi kwenye viti vyetu tukaendelea kunywa na kula. Baada ya nusu saa meneja wa ule mgahawa akaja kuniuliza kama ningependa kuja kuimba kila siku za mwisho wa wiki kwa malipo ya dola elfu mbili kwa mwezi. Nilikubali bila kusita nikaanza kuimba pale kwa muda wa mwaka mmoja na nusu. Pesa zangu nilihifadhi kwa kuwa sikuwa na matumizi makubwa wakati huo.

"Raj aliniomba anivalishe pete ya uchumba nikakubali; na kuanzia hapo uhusiano wetu ukaingia kwenye kidato kingine. Miezi tisa baadae tulipata mtoto wa kike tukampa jina la Caren. Nilifurahi sana, lakini furaha yangu iliyeyuka ghafla kama moto wa kifuu kwani wakati tunarudi kutoka hospitali tulipata ajali mbaya iliyokatisha uhai wa Raj na mtoto Caren.

"Nilijiona ni mtu mwenye mkosi. Nikaapa sitokuja kupenda tena kwani kila nimpendaye huishia kuniacha na maumivu kwa kudhamiria kama Daevick au kwa kutodhamiria kama Raj.

"Nilichujikia na sikutaka tena kuishi. Dada zangu wakanitafutia mshauri wa saikolojia ambaye alinisaidia kurudi katika hali yangu ya utimamu. Baada ya miezi mitatu nikarudi tena chuoni nikamalizia masomo yangu, nikaanza rasmi kuwa mwanamitindo na mwimbaji. Hatimaye nikaanza pia kuigiza. Ndio maana sipendi kuwa na mahusiano ya kimapenzi. Nayafananisha na uyoga."

"Wapenzi watazamaji muda umetupa mkono. Nadhani Mariam amewajibu kwa nini yuko kama alivyo. Nadhani mmepata kuelewa ni kwa jinsi gani mapenzi yalivyoibua matatizo mengi kwake." alisema Sabrina akavunja ukimya uliotawala kwa sekunde kadhaa.

# Yote ni Mapito

Eliana Swai

Katika mitaa ya 'Desturi', katikati mwa jiji lenye mamilioni ya watu na maisha yenye mseto wa mwanga wa raha na giza la shida, kila siku ilikuwa ni mapambano yasiyokoma kwa Mazito. Akiwa anatembea kwenye mitaa iliyojaa watu, kapu lake la karanga likiwa rafiki yake wa pekee. Jua lilipiga kwa ukali, likiongeza joto la changamoto zake za kila siku. Kila pakiti ya karanga aliyouza ilimpatia kiasi kidogo cha fedha, ambacho kilitosha kwa mahitaji yake ya siku, lakini kivuli cha umaskini kiliendelea kumfuata kila mahali, kama mwandamo usioepukika.

Jioni moja, wakati rangi za machweo zilipokuwa zikichanganyika na mandhari ya mji, Mazito aliketi kando ya kapu lake, ambalo sasa lilikuwa tupu, macho yake yakiangaza kwa mbali, yakipotea katika mwanga hafifu wa taa za mtaani. Mikono yake, iliyokuwa imepata uimara kutokana na kazi ngumu ya siku nzima, ilibeba mapato yake ya siku hiyo. Alijikuta akitafakari kuhusu maisha yake yaliyojawa na jitihada na changamoto zisizoisha.

"Je, hii ndiyo pesa yote niliyonayo, kweli?" alijisemea Mazito peke yake, sauti yake ikitetema kama mwangwi dhaifu katika mji mkubwa, usiojali. Akiangalia noti na sarafu zake chache, alitabasabu na kuendelea, "Siku baada ya siku, ni karanga na senti tu. Huenda siku moja nitajulikana kama *Malkia wa Karanga*, nikivaa taji la siagi ya karanga badala ya dhahabu inayong'ara!" alicheka kidogo akiwaza jinsi ambavyo angetembea kwa madaha mtaani akiwa amevalia joho la malkia lililoshonwa kwa maganda ya karanga.

Ghafla, alisikia sauti ya mtu akimwita, na kumzindua kutoka katika ndoto zake za alinacha. Aligeuka kuona ni nani aliyemvuta kutoka katika dunia yake ya ndoto. Rafiki yake Veuwele, alimsogelea akaketi kando yake na kusema kwa mzaha, "Mazito, nadhani wakati umefika wa kubadilisha jina lako kuwa 'Mepesi' maana unaonekana kuzidiwa na karanga zako!" alicheka kidogo.

Mazito alimtazama Veuwele, macho yake yakiakisi shukrani iliyochanganyika na hali ya kukata tamaa. "Lakini Veuwele, nitawezaje kuvunja mzunguko huu? Inaonekana kana kwamba mitaa hii ndiyo hatima yangu," alisema kwa sauti iliyojaa tashwishi.

Veuwele, akicheka kidogo, alijibu kwa sauti laini lakini yenye uhakika,

“Kumbuka, Mazito, miti mikubwa hukua kutoka mbegu ndogo. Na usisahau, hata karanga ni mbegu, sivyo? Una nguvu ya kubadilisha hadithi ya maisha yako, na labda kuuza kitu kingine zaidi ya karanga siku moja!”

Kadri siku zilivyogeuka kuwa wiki, na wiki kuwa miezi, hali ya Mazito ilizidi kuwa ngumu. Mvua zilikuja, zikageuza mitaa kuwa mito ya matope iliyomeza matumaini yake. Wateja walipungua, na kapu lake la karanga mara nyingi lilienda nyumbani likiwa limejaa kama lilivyoondoka. Njaa ikawa mwandani wake wa kudumu, ikimtafuna anapokuwa amelala kwenye chumba chake kidogo, chenye mwanga hafifu, kuta zikiitikia mwangwi wa matumbo yenye njaa kutoka makazi jirani.

Siku moja, alipokuwa akitembeza karanga, mvua kubwa ilimwagika ghafla, akateleza na kumwaga karanga zake kwenye tope.

Mazito alizitazama, moyo wake ukazama kama karanga zilivyozama kwenye matope.

Mwanamke mzee, ambaye mara kwa mara alinunua karanga kutoka kwake, alimkaribia na kumwekea mkono wa faraja begani. “Mtoto, usikate tamaa. Wakati mwingine unapoanguka unaiona njia vizuri zaidi.”

Usiku ule, chini ya paa linalovuja la chumba chake, Mazito alilala macho. Maneno ya yule mwanamke mzee yakimjia kichwani. Katikati ya zahama ile, mbegu ya wazo ilianza kumea. Wazo lilikua likawa na umbo. Lilikuwa la kuanzisha mtandao wa bustani za mjini ambazo hatimaye zingeleta mapinduzi ya kijani katika jangwa la zege la ‘Desturi’.

# Zawadi ya Mama

Maria Makasi

Kesho Jumapili ndiyo ile siku ya kipekee ya kumpongeza mama yangu, Doreen, aliyeandika historia ya kuwa mwanamke wa kwanza kuwa Rais wa Baraza la Wamiliki wa Biashara za Kimataifa nchini Tanzania. Dunia nzima inapommwagia sifa, mimi nimejikuta niko njia panda, nikitafakari zawadi inayomfaa. Zawadi zote ninazozifikiria zinaonekana kupwaya mbele ya jitihada zake. Kila ninachoweza kumnunulia kinatokana na jasho lake. Ni kama kumrudishia ndege yai alilotaga mwenyewe, mzaha kupindukia!

Hisia kali zinanijia ninapofikiria jinsi mama alivyokuwa nguzo ya maisha yangu. Ni mwalimu wangu, mlezi, mfadhili, chanzo cha kila kilichonizunguka. Kila wazo la zawadi linapoingia akilini linaniachia swali moja kubwa, "Zawadi hii itaushitua moyo wake japo kidogo tu? Je, itaendana na upendo wake usio na kifani kwangu?"

Saa zinasonga na bado jawabu halitaki kupatikana. Nakosa amani kwa maana tayari nyumbani wameshafika bibi na wajomba zangu; wapo sebuleni wanaongea na mama. Naenda kuwasalimu na bila kufikiri naropoka,"Na babu naye atakuja?"

Babu na bibi wameachana muda mrefu. Mama, bibi na wajomba wananiangalia wakiwa wamekunja sura. Nimeshaelewa kosa langu sitaki tena jibu; lakini mama ananijibu kwa mkato. "Nitakuambia baadae kama atakuja au la."

Naondoka kuelekea chumbani kwangu nikiwa nimelowa kwa tahayari.

"Emma?" haujapita muda, sauti ya mama inanitoa kwenye lindi la mawazo.

Namwitikia kwa sauti iliyojaa upendo na utii. Ninarejea sebuleni na kumkuta amekaa kwenye kiti chake pendwa, miguu kaweka juu ya kochi, akipitia orodha ya wageni waalikwa kwenye sherehe ya kesho. Akiwa katika hali ya utulivu na furaha, anagongagonga kalamu yake kwenye karatasi. Kila jina analoligusa linampa tabasamu. Huyu ndiye mama ninayempenda, sio yule ambaye huwa wakati mwingine namkuta akilia machozi, ambaye hayuko tayari kunidokeza sababu ya kilio chake.

"Hebu njoo mara moja mwanangu!" sauti yake inanishtua kutoka kwenye tafakuri zangu. Moyoni najiuliza, "Ananihitaji kwa jambo gani, wakati tumeachana

sasa hivi tu?"

"Niangalizie simu yangu, sijui nimeiacha wapi."

Naingia chumbani kwa mama, chumba cha faraja yangu. Macho yangu yanapepesa juu ya meza yenye rundo la vitu lakini simu haipo pale. Naenda kwenye meza ya kujirembea iliyosheheni vipodozi. Hapana simu. Ghafla, nikasikia mlio wa ujumbe wa simu kutoka chini ya mto! "Aha, kumbe mama naye huficha simu chini ya mto! Nacheka. Huwa ananikataza kufanya hivyo lakini kumbe hata yeye haachani na simu hadi akiwa usingizini!"

Ninapoinua mto, macho yangu yanatua juu ya kitu kingine kilicho pamoja na simu. Ni kijitabu kidogo, chenye jalada chakavu. Nashindwa kujizuia kucheka. Hiki ni nini tena? Mama ameanza lini kupenda vitu vya kale? Nakipuuza kijitabu hicho chenye rangi iliyofifia kiasi cha kutoweza kuitambua rangi yake ya awali.

Kabla sijaondoka, nakikodolea tena macho kijitabu kile, kisha naachana nacho. Naanza kuondoka, halafu nasita. Nasimama na kukitazama tena. "Huenda kinaonekana kutokuwa na thamani kwa nje lakini kina hazina ndani," nawaza. Nakichukua. Kufungua ukurasa za mwanzo, nakutana na mwandiko wa mama. Sasa fikra inanijia, "Kama nitasoma mawazo yake, pengine nitajua zawadi gani itamfurahisha." Wazo hilo linanitekenya, naanza kutabasamu.

Ninapoanza kukisoma tu, simu ya mama inalia. Nakificha kijitabu kile haraka kwenye nguo zangu za ndani ili mama asigundue kuwa ninacho. Baada ya kumpa simu yake, narejea chumbani kwangu. Moyo unanidunda kwa msisimko na udadisi. Naketi kitandani, nakifungua kijitabu upesi nikitaka nikisome haraka na kukirudisha kabla mwenyewe hajagundua kuwa hakipo.

Ni saa tatu asubuhi ninapoanza kusoma mstari wa kwanza.

*Nalia kuponya nafsi yangu…*

Maneno haya yananisukuma kuendelea. Nikijua kwa nini analia, pengine naweza kupata kitu cha kumfanya mama aache kulia kabisa.

Kila mstari ninaousoma unaniacha na maswali mengi lakini pia ulinipatia majibu ya baadhi ya maswali ninayojiuliza kila siku. Baadhi ya aya zinanifanya nilie. Kabla hata sijafika katikati ya kijitabu naitwa kwa ajili ya chakula cha mchana. Jua la utosi linapenyeza mwanga mkali kupitia dirishani. Natoka chumbani nikiwa nimeyagundua mambo ambayo sijawahi kuyafikiria. Naanza kujuta kwa nini nimekisoma kijitabu cha mama. Hata hivyo, nafurahi kujua kuwa kitanisaidia kupata zawadi yake.

Ninatoka chumbani kama kivuli, nikiwa nimejawa na mawazo mchanganyiko. Ninaamua kuwa sitakula na wageni. Nachukua funguo za gari

alilonizawadia mama baada ya kuhitimu masomo, nikiazimia kutafuta kimbilio la amani kutoka kwenye dhoruba itokanayo na kurasa za kijitabu kile.

"Ina maana huli na sisi mchana huu, Emma?"

"Hapana mama, kuna kitu muhimu naenda kufanya."

"Kitu gani zaidi ya kukutana na Sarah? Yaani unaniacha mimi mama yako, bibi na wajomba zako ambao ndio kwanza wamefika kwa ajili tu ya kukutana na huyo rafiki yako?!"

Maneno ya Mama yananipa uchungu kidogo. Najua ni kiasi gani anathamini muda tunaokuwa pamoja ambao hupatikana kwa nadra sana.

"Samahani, mama, si hivyo unavyofikiri. Nakupenda sana. Pia nina hamu ya kuongea na bibi na wajomba zangu lakini kuna kitu cha muhimu nafuatilia. Tutaongea jioni."

"Haya nenda ukasuuze moyo wako." mama ananifanyia utani.

"Na tumbo pia, mama." najibu kwa utani pia, lakini moyo wangu ni mzito kwa mawazo.

Mama anacheka. Najaribu kuficha hisia zangu, naondoka haraka hadi ufukweni, natafuta mahali pa faragha kama ndege anayetafuta utulivu katika tundu lake. Napata mahali pazuri, chini ya kivuli cha mkoko. Nafungua tena kurasa za kile kijitabu. Kila neno ninalosoma linafumbua fumbo linalojengea kwenye picha kubwa ambayo bado haijawa wazi kabisa.

Simu yangu inapolia, inakuwa kama kengele inayovunja tafakuri yangu. Sarah anataka kujua kwa nini sijatimiza ahadi yangu. Napata kigugumizi nikijaribu kubuni sababu, lakini maneno yanakataa kutoka. Sarah anaendelea kuzungumza, akijiuliza na kujijibu mwenyewe, hadi anapochoka na kukata simu. Naendelea kusoma kijitabu, nikitafakari kila neno, nikiwa nimezama katika bahari ya hisia na mawazo.

Hatimaye narejea nyumbani nikiwa nimechoka baada ya kuibeba dunia nzima kichwani mwangu. Watu wamelala lakini mama hajarudi kutoka saluni. Napitiliza moja kwa moja jikoni, na kula harakaharaka kabla ya kuingia kimyakimya chumbani kwa mama na kukirejesha kijitabu chini ya mto nilikokitoa, kisha naenda chumbani kwangu kulala.

Usingizi unanichukua hadi alfajiri. Bado nina mengi ya kufanya kabla ya hafla ya leo. "Nitaanza mapema," najiambia, kisha najiandaa harakaharaka ili nitoke. Navaa suti mpya iliyonunuliwa kwa ajili ya sherehe na kuacha ujumbe kwa mama: 'Nimeenda kuwaona rafiki zangu. Tutaonana ukumbini.'

Yapata saa mbili asubuhi ninapowasili ukumbini ninapokelewa na marafiki wa mama wanaosimamia upambaji. *Msema Chochote* na *DJ* nao wanajaribu mitambo yao. Naongoza moja kwa moja hadi kwa *Msema Chochote*. Nampa ombi langu maalum lakini analipiga chini.

"Matukio ni mengi muda hautoshi *bro*." Najaribu kumbembeleza lakini inashindikana, hivyo naamua kuvuta subira. Muda unavyokwenda ndivyo wageni wanavyoanza kumiminika ukumbini. Baadhi ya rafiki zangu wanawasili mapema hivyo nawafuata niwapokee na kusalimiana nao. Mbali na kuwepo watu wengi kutoka Tanzania pia kuna nyomi ya watu kutoka ughaibuni ambao wamefika kuwakilisha mashirika yao. Punde si punde mshereheshaji anaanza kuita watu waingie ukumbini. Ghafla anakuja mtu ambaye ameagizwa na mama kuniita. Anasema kuwa bibi na wajomba zangu wameshawasili na wanataka kuniona. Mara moyo unapiga "paa"! Nakumbuka baadhi ya maneno niliyoyasoma ndani ya kijitabu kile. Bila kutegemea machozi yanaanza kunilengalenga lakini najikaza nisilie mbele za watu. Mama na rafiki yake Dokta Catherine wamesimama nje wakisubiri kuingia ukumbini. Nawafuata.

Mama ananiagiza nihakikishe bibi na wajomba zangu wamepata mahali pazuri pa kukaa. Kabla sijafanya nilichotumwa msema chochote anawaita familia ya Mama Emma ikae meza kuu. Natamani nikae na marafiki zangu lakini sina budi kukaa nilipopangiwa siku hii ya pekee. Sherehe inaanza rasmi, mama analakiwa kuingia ukumbini kwa midundo, vigelegele na vifijo.

Mwanasheria wa mama anaitwa kutoa utambulisho na wasifu wa mama. Punde si punde babu naye anawasili. Mama anashuka kutoka jukwaani alipoketi na kwenda kumpokea na kumpeleka kukaa meza kuu.

Baada ya risala kutoka kwa watu mbalimbali, kula na kunywa, sasa ni muda wa zawadi. Wageni waalikwa wanatoa zawadi zao kisha wanafuatia wazazi, yaani babu na bibi, halafu na mimi naitwa; mtoto wa pekee wa mama kama inavyoaminika. Moyo unapiga, "paa!" Niliapa kukomesha kilio cha mama baada ya kujua sababu, lakini sasa naona jinsi gani kazi hii ni ngumu.

Nanyanyuka kwa unyonge na kupokea kipaza sauti huku mikono ikitetemeka. Naanza kwa kumpongeza mama yangu. Nasisitiza kuwa sijaona zawadi inayomfaa kutoka kwangu zaidi ya hiyo ambayo nimemuandalia. Naomba ridhaa ya kumpatia mama yangu zawadi hiyo. Watu wote wanaonesha nyuso za shauku ya kutaka kujua nini nilichokiandaa kwa sababu mkononi sijashika kitu. Nasikia sauti miongoni mwa waalikwa zikisema, "mpe tuuuuu!"

Ninapoangaza macho naona watu wametulia tuli na kimya kimetawala.

Nageuka nyuma na kumtazama mama pale jukwaani. Sina jina jingine

nijualo kumuita ila mama tu. Sijui ataichukuliaje hii, lakini napiga moyo konde. Inabidi. Naanza kutoa risala niliyoiandaa. "Mama yangu Doreen Ponela, kama tunavyofahamu ni mtoto wa pili kati ya watoto saba wa bibi na babu yangu." Namtazama tena mama na kumuomba msamaha kwa yale ninayoka kusema.

"Endelea tu mwanangu."

"Mama yangu huwa analia kila mara kwa sababu ya masaibu yaliyowakuta wazazi wake hadi wakafarakana. Baba yake alipitia mengi magumu hadi akafukuzwa kazi kwa kukataa kushirikiana na wala rushwa, matokeo yake, alishindwa kuhudumia familia, akawa mlevi na kuikimbia familia yake. Kinachomsikitisha zaidi mama yangu ni jinsi ambavyo jamii inamfahamu kama mtu mlevi na haikumbuki tena uadilifu wake." Natulia kidogo kuitazama hadhira. Vichwa vyote vimeinamishwa chini. "Kutokana na changamoto alizokabiliana nazo, kutokana na wazazi wake kuishi kila mmoja peke yake hakutamani kuwa na mtoto. Alihofia kuwa huenda yeye pia hataweza kumlea na kumpa furaha mtoto wake kama alivyoikosa kwa wazazi wake." Hapa nasita kidogo, kwani ni mahali pagumu. Nameza funda la mate na kuendelea; "Labda wengine hamjui lakini nimegundua jana kuwa mimi si mtoto wa kuzaliwa na Mama Emma. Ameniasili ili nisikulie katika magumu aliyoyapitia yeye. Nakushukuru sana mama kwa kunichagua, si kunilea tu, bali kunipenda. Sina zawadi ya kukupa ila kuukumbatia upendo wako na kujitahidi kufanya niwezavyo kukilea vema kizazi nitakachokipata na kukulea wewe utakapozeeka."

Mama anashuka jukwaani na kunikumbatia.

"Emmanuel mwanangu," anasema. Ni mara chache mama ananiita kwa jina langu kamili. "Mimi nimechagua kitu adimu lakini nafuu kwangu. Kukupenda wewe ndilo jambo pekee linaloweza kuuponya moyo wangu." Hapa mama ananikumbatia. Baada ya kubaki tumekumbatiana sote tukitokwa na machozi ananishika mkono na kunirudisha meza kuu kuketi, kisha akarudi mahali pake.

Baada ya sisi kuketi, babu anachukua kipaza sauti na kuanza kuongea, "Pole sana mwanangu Doreen kwa masahibu yote niliyokusababishia. Naomba unisamehe."

Sasa namuona mama akijongea taratibu kama kinyonga na hatimaye anaanza kuzungumza "Asante sana mwanangu Emmanuel kwa kuuponya moyo wangu. Asante sana baba, mimi sijawahi kuwa na kinyongo nawe, ila ulimuachia mama majukumu na majonzi makubwa. Yeye ndiye anastahili kuombwa msamaha. Nina mengi sana moyoni ila ninachoweza kusema kwa leo ni kwamba, ukweli huu ulionitafuna kwa muda mrefu umetoka hadharani na sasa najisikia huru. Asante Emma kwa zawadi hii."